# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Tatu – Tarehe 2 Aprili, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kwa njia ya Mtandao)*

Na. 20

**Kukabiliana la Tatizo la Mafuriko – Bukoba**

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU** aliuliza:-

Mafuriko yanayotokea katika Mji wa Bukoba husababisha uharibifu mkubwa wa chakula, mali, barabara na hata kusababisha vifo kwa watu na mifugo; mafuriko hayo husababishwa na Mto Kanoni kujaa mchanga na takataka

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaondolea kero ya mafuriko kila mwaka ikiwemo kusafisha na kuongeza kina cha Mto Kanoni?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA**) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bernadetha Kasabago Mushashu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chanzo cha uchafuzi wa Mto Kanoni unaosababisha mto huo kujaa mchanga na taka ngumu zinazopelekea wakati wa masika maji kujaa na kuleta athari za mafuriko kwenye makazi ya watu, ni kuwepo kwa shughuli za kibinadamu pembezoni na ndani ya mto zikiwemo; ujenzi wa nyumba, ujenzi wa karo za maji taka, kilimo (mashamba), ujenzi na utumiaji wa mazizi na vyoo, ufuaji, uogaji na uoshaji wa magari na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Bukoba imeanza kuchukua hatua za muda mfupi kwa kupiga marufuku na kuondoa shughuli zote za kibinadamu zinazofanyika ndani ya mto kama zilivyobainishwa hapo juu, pamoja na kuhakikisha eneo la hifadhi ya mto kisheria, linasafishwa.

Aidha, hatua nyingine ambazo Halmashauri inaendelea kuchukua ni pamoja na kuondoa miti yote isiyokuwa rafiki wa mazingira iliyokuwa imepandwa ndani ya Mto Kanoni na kupanda miti rafiki wa mazingira, kufuatilia ubora wa maji ya mto na kutoa elimu ya uhifadhi wa mazingira kupitia redio, mikutano ya hadhara, semina na makongamano. Halmashauri ya Manispaa ya Mji wa Bukoba inaendelea kuwahamasisha wananchi kujitolea kupanda miti ili kuhifadhi kingo za mto na uondoaji wa mchanga unaosababisha kupungua kwa kina cha mto kunakosababisha mafuriko wakati wa masika.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mto wa Kanoni kwa sasa umejaa sana mchanga na kina kimepungua sana, kwa watu wenyewe itakuwa si kazi rahisi kuondoa mchanga na zitahitajika fedha nyingi

sana; pamoja na hatua zilizoainishwa kwenye jibu la swali ambazo ni za muda mrefu:-

Je, ni kwa nini Serikali isiwasaidie sasa hawa watu wanaohangaika na mafuriko kila mwaka kwa kutoa fedha kiasi za kuanza kusafisha mto huu angalau mara moja kwa mwaka?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, awali yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Benadetha kwa kufuatilia kwa kina suala hili na kutupatia taarifa za kina kuhusu changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikiashia Mheshimiwa kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu na inajali wananchi wake. Hivyo, Serikali inalichukulia kwa uzito suala hili na tunawasiliana na mamlaka husika ikiwemo Halmashauri ya Bukoba Mjini kuona namna bora na ya kudumu ya kutatua changamoto ya kujaa mchanga katika Mto Kanoni ili kuondoa kero ya mafuriko ya mara kwa mara.

Na. 21

## Hitaji la Maji Safi ya Kumwagilia kwa Ajili ya Wakulima wa Mbogamboga- Dar es Salaam

**MHE. ZAINABU M. AMIRI** aliuliza:-

Mboga za majani ni lishe bora kwa afya ya binadamu na wakulima wengi wa mbogamboga hasa Jijini Dar es Salaam wanatumia maji yasiyo salama kwa ajili ya kumwagilia na huenda maji hayo yana kemikali zinazoweza kupelekea mbogamboga hizo kudhuru afya za wananchi badala ya kuziimarisha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia maji safi na salama wakulima hao wa mbogamboga?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mboga za majani ni lishe bora kwa afya ya binadamu na wakulima wengi wa mboga hizi waliopo Jiji la Dar es Salaam hutegemea Bonde la Mto Msimbazi kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao. Hata hivyo, Mto Msimbazi unaendelea kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kiuchumi na kijamii ikiwemo kilimo cha mbogamboga kando ya mto huo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutoa elimu kuhusu hifadhi ya vyanzo vya maji na kutekeleza mipango na shughuli mbalimbali kwa ajili ya kulinda mazingira ya mto huo yasiharibiwe.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa mradi wa kuboresha Bonde la Mto Msimbazi ili kukabiliana na changamoto zitokanazo na uharibifu wa mazingira katika mto huo. Mradi huu unalenga kupunguza athari za mafuriko, kudhibiti mmomonyoko wa udongo unaosababishwa na shughuli za binadamu kando ya mto huo, kujenga uwezo wa jamii inayozunguka Mto Msimbazi kuendelea na shughuli za kiuchumi pasipo kuathiri mto, kupanda miti kwa ajili ya hifadhi ya mazingira ya mto, kuweka mkakati wa udhibiti wa taka ngumu katika mazingira ya Mto Msimbazi na kujenga mazingira wezeshi kwa wajasiriamali wadogo kuendeleza shughuli zao pasipo kuathiri mazingira ya mto huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuboresha mazingira ya Bonde la Mto Msimbazi, tunategemea kwamba uchafuzi wa mazingira katika mto huo utapungua. Hata hivyo, Kifungu cha 57 cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kinazuia shughuli za kudumu na ambazo kwa asili yake inaweza kuhatarisha au kuathiri vibaya utunzaji wa bahari au kingo za mto na mabwawa katika eneo la hifadhi mita 60 kutoka vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, aidha, sheria hii inampa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya usimamizi wa Mazingira kuandaa mwongozo wa matumizi endelevu wa eneo hilo. Kwa muktadha huo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeandaa rasimu ya mwongozo wa mita 60 wa kuhifadhi vyanzo vya maji. Rasimu hii inaainisha matumizi endelevu ya eneo la mita 60 kutoka vyanzo vya maji ikiwemo shughuli za kilimo kando na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Zainabu Mndolwa Amiri kwamba Serikali itaendelea kuboresha Sera, Sheria na Kanuni ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo na usimamizi thabiti wa mazingira ya nchi yetu. Aidha, ni matumaini yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge watakuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha wananchi kuzingatia sheria zilizopo katika kufanya shughuli za maendeleo ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuhifadhi mazingira na kuboresha ustawi wa jamii.

Na. 22

**Hitaji la Mawasiliano ya Simu ya Uhakika – Sikonge**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Baadhi ya minara ya simu ya *Vodacom, Airtel, Tigo* na *Halotel* katika Kata za Kipili, Kilumbi, Kiloli, Kitunda, Kisanga, Mole, Kiloleli na Ipole haifanyi kazi vizuri kwani mtandao katika Kata hizo ni mdogo sana na hivyo wananchi hawapati huduma nzuri ya mawasiliano licha ya uwepo wa minara hiyo. Aidha, katika Kata za Nyahua, Igigwa na Ngonjwa hakuna kabisa mawasiliano ya simu:-

(a) Je, ni lini Serikali itawapatia mawasiliano ya uhakika wakazi wa Sikonge wanaoishi kwenye Kata zenye minara ya simu lakini isiyokamata mtando vizuri?

(b) Je, Serikali itawapatia lini mawasiliano ya simu wananchi wa Sikonge ambao wanaishi kwenye Kata ambazo hazina kabisa minara ya mawasiliano ya simu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imetoa ruzuku kwa ajili ya ujenzi wa minara ya mawasiliano katika Wilaya ya Sikonge katika Kata za Kiloli, Igigwa, Kipanga, Kipili na Kitunda kwa kushirikiana na *TTCL* na VODACOM kupitia miradi ya mawasiliano ya awamu ya kwanza na awamu ya tatu.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Igigwa, Serikali kupitia Mfuko ilitangaza zabuni na kupata mtoa huduma *TTCL* ambaye ameanza maandalizi ya ujenzi wa mnara katika kata hiyo. Kwa upande wa Kata za Nyahua na Ngonjwa, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote itazijumuisha kata hizi katika Mradi wa Mawasiliano Vijijini awamu ya tano ndani ya mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* itafanya ukaguzi wa ubora wa huduma za mawasiliano kwa kushirikiana na watoa huduma kulingana na viwango vya ubora vilivyowekwa kwa mujibu wa Kanuni za Ubora ili kuhakikisha wananchi wanapata mawasiliano ya uhakika kwa maeneo yenye usikivu hafifu.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa Serikali kujibu swali langu Na. 22 vizuri. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; mnara wa *Airtel* uliojengwa kwenye Kata ya Kipili, Kitongoji cha Madoletisa ambao haujawashwa kwa miaka miwili sasa na mnara wa *Vodacom* kwenye Kata ya Kilumbi ambao nao haujawashwa kwa miaka miwili hadi sasa: Je, ni lini itawashwa ili wananchi waanze kufaidika na huduma za mawasiliano?

Mheshimiwa Spika, je, Miradi ya Mawasiliano Vijijini iliyomo kwenye Mpango wa Maendeleo wa 2019/2020 ambayo orodha yake ipo kwenye randama pia kwenye kijitabu cha taarifa ya Wizara ya Julai 2019, itatekelezwa lini?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, mnara uliojengwa katika Kitongoji cha Madoletisa ni kweli ni wa Kampuni ya Simu ya *Airtel*. Mnara huu ulijengwa kama mnara wa kupeleka mawimbi ya simu kwenda katika minara mingine ya mbali *(Transmission Site).* Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* uliliona tatizo la mnara huo ambapo unatumika kama *transmission site* bila kutoa huduma kwa wananchi waliopo Madoletisa na kuiagiza Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Airtel* wauwekee vifaa vya *radio* ili mnara huo pia utumike kutoa huduma za mawasiliano kwa wananchi. Tumewasiliana na *Airtel* ili wakamilishe kazi ya kuwapelekea wananchi mawasiliano mara moja ndani ya mwezi huu wa Aprili, 2020.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Mawasiliano Vijijini kwenye Vijiji vya Igigwa, Migumbu, Nyahua na Tumbili kutoka Kata ya Igigwa, Vijiji vya Ipole, Makazi, Udongo na Ugunda kutoka Kata ya Ipole, Vijiji vya Kanyamsenga, Kiloleli na Mtakuja katika Kata ya Kaloleli, Vijiji vya Imalampaka na Mibono katika Kata ya Kipanga pamoja na Kijiji cha Kiyombo kutoka Kata ya kipili, havikupata watoa huduma katika zabuni ya mwezi Julai, 2019. Miradi hiyo itatangazwa tena mwezi Juni, 2020.

Na. 23

**Serikali Kupeleka Fedha Maporomoko ya Kalambo**

**MHE. AIDA J. KHENAN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka fedha kwenye kivutio cha maporomoko ya Kalambo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maporomoko ya Mto Kalambo yapo katika Msitu wa Hifadhi ya Mazingira Asilia Kalambo yenye ukubwa wa hekta 41,958. Hifadhi hii ni muunganiko wa misitu miwili; Msitu wa Mto Kalambo na Msitu wa Hifadhi wa Maporomoko ya Mto Kalambo. Kutokana na kuwepo kwa maporomoko hayo, eneo hili lina bioanuai nyingi. Kwa kuzingatia umuhimu wa eneo hilo, mwaka 2019, Serikali ilipandisha hadhi msitu huo kwa Tangazo Na. 127 kuwa Msitu wa Mazingira Asilia.

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania *(TFS),* mwaka 2016 ilianza kuboresha miundombinu katika Maporomoko ya Kalambo ili kuwezesha watalii kuvifikia kivutio husika kwa urahisi, ikiwa ni pamoja na kujenga ofisi sita, kutengeneza njia za kutembelea wageni *(walk trail)* na kujenga ngazi katika maporomoko ya Mto Kalambo ambapo hadi sasa takribani ngazi zenye urefu wa mita 450 zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, aidha, kazi ya ujenzi iliyoanza mwaka 2018 ambayo inahusisha ujenzi wa jengo la ofisi, ngazi zenye urefu wa mita 514, vyoo na geti inayofanywa na kampuni iitwayo *Green Construction Limited* inaendelea kufanyika katika maporomoko hayo na kazi hii inatarajiwa kukamilika ndani ya mwaka huu wa 2020.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha mazingira ya utalii katika eneo hilo, Serikali itahamasisha sekta binafsi ili zijengwe nyumba za kulala wageni, kumbi za mikutano na eneo la kuhifadhi wanyamapori hai *(zoo)* ili kuweka mazingira rafiki kwa watalii.

Na. 24

**Uchakavu wa Kituo cha Polisi Malindi-Unguja**

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB** aliuliza:-

Kituo cha Polisi cha Malindi kilichopo Unguja ni kituo cha kihistoria na cha mfano, lakini kituo hicho tangu kimejengwa na wakoloni hakijawahi kufanyiwa ukarabati na kwa sasa kiko taabani:-

(a) Je, ni lini Kituo hicho kitafanyiwa ukarabati?

(b) Je, ni bajeti kiasi gani inahitajika kwenye ukarabati wa kituo hicho?

(c) Je, Serikali haioni kuwa kituo hicho kitavunjiwa hadhi yake ya kihistoria?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jengo linalotumika kama Kituo cha Polisi Malindi ni moja ya majengo ya zamani yaliyojengwa enzi za mkoloni ambayo yanasimamiwa na Idara ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ambayo inapata msaada kutoka Shirika la *UNICEF.* Jeshi la Polisi linashirikiana na wataalamu wa Idara ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kuona ni namna gani ukarabati wa jengo hilo utafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Uhifadhi na kuendeleza Mji Mkongwe.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya ukarabati wa jengo hilo inatarajiwa kufanyika hivi karibuni baada ya makubaliano ya wataalamu wa Jeshi la Polisi na wataalamu wa Idara ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda historia ya jengo hili taratibu na kanuni za Idara ya Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe zitafuatwa na kutekelezwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge naomba tukae, ngoja niweke mitambo sawasawa hapa maana sasa ni teknolojia tu baada ya kuweka mitambo sawasawa *sanitizer* kwanza na nyinyi mkumbuke *sanitizer* Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo. Katibu!

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Majadiliano yanaendelea naendelea na orodha kama nilivyoletewa na kambi za vyama vyetu na machifu *weep*, kwahiyo naanza na Mheshimiwa Edward France Mwalongo na wakati Mwalongo anaanza niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge unapaswa kukaa kwenye kiti chako tu, kuhama hama kwenda kwenye viti vya watu wengine ni kutengeneza tatizo. Kwa hiyo, mjitahidi kadri muwezavyo kubaki kwenye viti vyenu na ukiwa na nafasi ya kuongea utaongea kwenye *mike* yako tu ili mwenzako naye aweze kuongea kwenye *mic* yake mwenyewe ni nyakati za mabadiliko kidogo hizi tuzingatie.

Mheshimiwa Mwalongo tuendelee na atafatiwa na Mheshimiwa Kamishna Mary Pius Chatanda.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wa hotuba ya ofisi yake. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, na Serikali

yake kwa ujumla jinsi wanavyofanya kazi tumeona katika miaka yote minne iliyopita Serikali yetu imefanyakazi nzuri tumepata mafanikio makubwa sana maendeleo yameonekana nampongeza sana Mheshimiwa Rais na Serikali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiendelea kuipongeza Serikali niipongeze sana Serikali kwa janga hili ambalo sasa linatukabili la *corona* Serikali ina jitahidi kutoa elimu inajitahidi kukabili tatizo hili na imeandaa kila aina ya misaada kwa wananchi nikuombe sana niombe sana sasa Serikali ikiwezekana iwaandae wananchi zaidi juu ya hali halisi ya corona ilivyo duniani na watanzania waambiwe bayana kabisa kwamba hali hii ikiendelea kuwa mbaya itabidi tukae ndani. Hivyo kila mtu akae akijua kwasababu hii ndiyo hali ya dunia ilivyosasa kwamba kule ambako corona imechachamaa watu wote sasa wanakaa ndani si vibaya kwa Serikali yetu kutamka hivyo kwamba watanzania tujue kwamba kama hali itaendelea kuwa mbaya tutakaa ndani ili kuhakikisha kwamba tunaepukana na tatizo hili la *corona*.

Mheshimiwa Spika, lakini wako wadau wanajitahidi sana kutusaidia kutoa elimu kwa wananchi ni mpenzi sana kusikiliza *Radio One* kwa kweli wanajitahidi kweli kweli *Radio One* kutangaza kutoa muda wao wa asubuhi zaidi ya masaa matatu wanazunguka mitaani wakielimisha wananchi. Jana nimeshuhudia mtangazaji anaongea na mtu wa daladala, mtu wa daladala anasema nina maji nilikuwa na sabuni lakini sabuni yangu imeibiwa mtangazaji anatoa fedha yake mfukoni anampa mtu wa daladala kwamba nunua sabuni nyingine ili kusudi abiria wako waendelee kupata huduma. Kwa kweli ni jambo ambalo linaonekana vyombo vya habari vimehamasika na wananchi wengi wamehamasika. Kwa kweli naipongeza sana *Radio One* kwa hilo waendelee kutoa elimu kwa wananchi na vyombo vyote vya habari viendelee kutoa elimu.

Mheshimiwa Spika, nikiacha hiyo habari ya ugonjwa wa corona, nije kwenye hoja ya Waziri Mkuu tuna tatizo kubwa sana la maji kama nchi lakini sasa ni takriban

tunakwenda huu ni mwaka wa tano tumekuwa hapa Bungeni tukiambiwa miji 26 itapewa fedha ya kutengenezewa miradi ya maji na huu ulikuwa ni mkopo toka India miaka mitano inakwisha toka tunaanza Bunge hili tumekuwa tukiambiwa miji 26 itapewa fedha miji 26 mara muambiwe sijui kuna sijui kuna *no objection* sijui mara nini yaani tunaweza kusema ni hadithi tu zimekwenda mpaka tumefika leo tunafika mwaka wa tano hakuna maji kwenye miji 25 na wananchi wanaendelea kutudai maji na sisi tumekuwa tukiahidi na Serikali imekuwa ikituahidi.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri Mkuu atakapokuwa anahitimisha hoja yake atuambie kwamba hii miji 26 ambayo tuliambiwa itapewa maji, ikiwemo mji wa Njombe ni lini sasa itapewa maji na kama hiyo ya India imeshindikana kwa sababu kama jirani ameshindwa kumpa mwanao chakula mwenye mtoto si umpe chakula mwanao? Au utaacha mtoto afe tu eti kwasababu jirani aliahidi atampa chakula. Kwa hiyo, nafikiri tubadilishe utaratibu tuendelee na utaratibu kama nchi tuipe maji hii miji kwasababu maji ni uhai, maji ni afya na maji ni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nipongeze sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi nzuri kubwa anayoifanya ya kurithisha ujuzi. Kazi hii ya ujuzi ni kazi muhimu sana vijana wengi sasa wameanza kupata ujuzi ninachokiomba kwenye idara ile inayoshughulika na ujuzi ipanue nafasi iende mpaka kwenye nafasi za fani za kilimo, fani za ufugaji kwa sababu kilimo na mifugo ndiyo itaajiri watu wengi nimeona wanatoa kwenye ufundi wa magari, umeme, na nini hivi yaani katika vijana tulionao katika nchi hii hao mmewasaidia vijana wa mjini lakini vijana wa vijijini watasaidiwa kwa kupelekwa kwenye fani za kilimo na fani za mifugo tutakuwa tumewasaidia vijana wengi wa vijijini kupata ujuzi na tutumie vyuo vingi zaidi tusitumie vyuo hivi vitatu tu Don Bosco, DMI, DTI hapana tuende vyuo vingine.

Mheshimiwa Spika, iko *private sector* ina vyuo vingi tu ambayo inaweza ikasaidia kutoa ujuzi huu. Kwa hiyo, niombe sana hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu mliangalie na msaidie

vijana wengi zaidi ili kusudi wapate ujuzi kwa sababu ujuzi pekee ndiyo utawafanya vijana wa nchi hii kuweza kujiajiri na kuweza kufanya kazi katika ulimwengu huu unaokwenda sasa watanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, nimeona katika hotuba ya Waziri Mkuu akizungumza habari ya benki ya kilimo. Benki ya kilimo imefanya kazi nzuri miaka mingi tumekuwa tukilalamika sana juu ya benki ya kilimo lakini kwa sasa benki ya kilimo inaonekana imefanya jitihada kubwa sana binafsi nimemuona Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Kilimo akipita kwa wadau mbalimbali na wananchi mbalimbali kuhamasisha na kuangalia miradi ambayo wanaweza wakakopeshwa na benki

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iendelee kuisimamia hii benki na benki yenyewe iendelee kujituma zaidi kushuka chini kwa wakulima wa kawaida kama vile anavyofanya Mkurugenzi wao basi watumishi wote ndani ya benki ile wafanye hivyo kwamba wawatembelee wananchi waone mahitaji ya wananchi wakulima ni nini. Lakini mara nyingi nimekuwa nikisimama hapa mbele yako nikilalamika sana juu ya matrekta, matrekta mengi wanayokopeshwa watanzania ni mabovu, matrekta mengi wanayokopeshwa watanzania hayakidhi haja ya kilimo tunaletewa katika nchi matreka ambayo hayana sifa. Taasisi zote zinazoleta matrekta zinaleta matrekta zinaleta matreka ambayo kwa kweli uimara wake na ubora wake ni chini sana. Kwa hiyo, niombe sana Serikali ilione hilo.

Mheshimiwa Spika, na mwisho kabisa ni suala la UKIMWI, tatizo la UKIMWI ni kubwa sana lakini ukubwa wa tatizo hili, sisi watanzania ni kama vile tumeufumbia macho. Kiwango chetu cha kutoa elimu kiende kwenye taasisi zilizochini kwa mfano halmashauri mimi ni mjumbe wa kamati ya Ukimwi lakini unakwenda pale halmashauri unakutana na watu ambao ni wajibu wao kutoa hiyo elimu lakini hawajui chochote hawatoi elimu na wala hawana *data* zozote niombe Serikali ilione hilo jambo liende lisimamiwe mpaka ngazi ya chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa ni mfuko wa UKIMWI *ATF* hatuna mfuko, tunao mfuko wa UKIMWI lakini Serikali haichangii hatuna tozo mahala ambalo linasaidia kuingia kwa ajili ya mfuko wa UKIMWI, tunategemea kupata huduma ya dawa hizi za Ukimwi *ARV* kutoka kwa wafadhili. Leo hii wafadhili wanapambana na *corona* na inawezekana *corona* ikawabana sana wakaendelea kuhudumia watu wao tu sisi ambao tunategemea msaada kutoka kwao tutakwama na tusipokuwa na *ARV* maana yake sasa watanzania tutaanza kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali iweze kuhakikisha kwamba inatafuta tozo yoyote ambayo watanzania tutachangia kwa ajili ya mfuko wa UKIMWI ili kusudi tuwe na mfuko wetu wa kujitegemea kuliko kutegemea wafadhili ambao leo hii mfadhili mkubwa ni Marekani, Marekani leo ana corona 200,000 na wanaendelea kupambana sasa atatukumbuka sisi kweli. Kwa hiyo, hii ni hatari sana kwetu na niombe sana Serikali iangalie hilo namna gani tutafanya tupate tozo ya aina yoyote ile iwe ni maalum kwa ajili ya masuala ya UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana kwa fursa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Edward Frank Mwalongo kwa mchango wako sasa nilikwisha mtaja Mheshimiwa Mary Pius Chatanda Kamishna na atafatiwa na Mheshimiwa Khadija Nassir.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu aliyoiwasilisha jana.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu lakini nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu mwenyewe, Mawaziri na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Serikali kwa namna ambavyo kwa kipindi cha miaka

minne wamefanya kazi kubwa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo makubwa yamefanyika hakuna mtu ambaye anaweza akapinga juu ya mambo makubwa ambayo yamefanyika mwenye macho haambiwi tazama mambo yanaonekana na wananchi wetu huko vijijini kwenye miji yetu wanaielezea vizuri Awamu hii ya Awamu Tano kwamba mambo makubwa yamefanyika katika kipindi kifupi namshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na watendaji wote wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikupongeze na wewe mwenyewe katika kipindi chote hiki cha miaka minne kuelekea huu wa tano, umekuwa kiongozi bora wa kutusimamia na kutuongoza katika Bunge lako hili Tukufu umekuwa ni mtu mbunifu tumekuwa tumekutana kwenye vikao vyetu vya Tume ya Utumishi wa Bunge ulianzisha hili na kutueleza hili suala la Bunge Mtandao mimi wakati huo unalielezea nilikuwa sikuelewi lakini kadri tulivyoendelea na nilivyokuja kuona sasa haya mambo ndiyo nikajua haa! Huyu kaka yangu kumbe mambo aliyokuwa anayazungumza ni mambo makubwa yenye manufaa kwa nchi yetu kwanza kwa kupunguza matumizi ya fedha katika vitendea kazi hususan makaratasi na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakushukuru tunakupongeza sana sana sana kwa namna ambavyo umekuwa ukitusimamia na kuhakikisha tunapitisha bajeti ndani ya Bunge hili ambazo zimekwenda kufanyakazi za utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, niungane na Watanzania wenzangu juu ya gonjwa hili la *corona*. Ugonjwa huu ni mbaya kwa bahati mbaya kulikuwa na ugonjwa huo mwingine ambao mwenzangu ametoka kuuzungumzia wa UKIMWI ulikuwa unaonekana wanasema ugonjwa huu umekaa sehemu mbaya huu hauna sehemu mbaya ni mbaya moja kwa moja unaua tuendelee kuwaelimisha wananchi wetu ili waendelee kuzingatia maelekezo

wanayotoa viongozi wetu hususan Rais wetu, Waziri Mkuu, Waziri wa Afya yale maelekezo wanayoyatoa basi wananchi wetu waendelee kuyazingatia ili kusudi yaweze kutusaidia tuweze kuwa salama.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo tukiwaacha wananchi wetu hawa bila kutoa maelekezo bila kuwasaidia kutoa elimu tutapoteza Taifa letu. Wako watu wanafanya mzaha na jambo hili, hili jambo halina mzaha wala dhihaka hata kidogo tunahitajika tuendelee kufanya kazi kubwa hasa kwenye maeneo kwa mfano kwenye stendi. Kwenye stendi za mabasi bado tatizo hili la kuwa karibu karibu msongamano wa watu bado hatujafanikiwa sana. Kwenye maeneo ya masoko bado hatujafanikiwa sana pamoja na kwamba watu wakifika kuna maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kunawa maji wengine wanapitiliza hawanawi. Kwa hiyo, ni vizuri tukaendelea kuwaelimisha wananchi wetu waweze kutambua juu ya gonjwa hili kwamba ni gonjwa hatari kila mmoja ajitambue akae mbali na wenzake ili kusudi aweze kujisalimisha kwa maana kukiepuka kifo.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Serikali kama nilivyosema imefanyakazi kubwa lakini bado baadhi ya maeneo bado tunahitaji kuendelea kuyasimamia ili kusudi wananchi wetu waweze kunufaika kwa mfano suala la maji Waziri Mkuu nikupongeze ulikuja Korogwe ulifanya mkutano Korogwe kubwa ambalo ulilisikia kwa wananchi wa Korogwe lilikuwa ni suala la maji.

Mheshimiwa Spika, niishukuru Wizara ya Maji kwamba wametupa vimiradi midogo midogo lakini bado havijakamilika kwahiyo niombe kwa kuwa nipo katika ile miji 28 ya fedha za mradi wa India basi niombe basi ile miradi midogo midogo waikamilishe ili iweze kuwasaidia wananchi wakati wanaendelea kusubiri huu mradi mkubwa. Kwa hiyo, ni ombi hili kwa wenzetu wa Wizara ya Maji waone ni namna gani sasa watatusaidia angalau kukamilisha ile miradi midogo ambayo tuliyo nayo ili kusudi wananchi waendelee kupata maji wakati tunasubiri ule mradi mkubwa wa fedha zile za India.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la afya, Wizara ya Afya ina vyuo vya Maendeleo ya Jamii pale Korogwe nina Chuo cha Uuguzi. Chuo kile kwa bahati nzuri kilijengwa jengo la utawala ambalo linavyumba kwa ajili ya madarasa lakini toka limejengwa lile jengo kwa awamu ya kwanza ni miaka 15 halijawahi kutengewa fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo lile. Sasa kwa sababu tunazungumzia haya masuala ya afya, masuala haya ya ugonjwa wa Corona na vijana wetu wanasoma katika kile chuo, ningeiomba Serikali waifikirie sana kile chuo cha uuguzi pale Korogwe angalau kuweza kukitengea fedha kiweze kukamilika na kiweze kuanza kufanya kazi yake vizuri kama ambavyo ilikuwa imekusudiwa. Wananchi wanashindwa kuelewa kwa sababu jengo lile ni miaka 15 sasa halijawahi kutengewa bajeti kwa hiyo niombe sana Wizara ya Afya ione umuhimu wa kukipatia fedha chuo kile cha afya.

Mheshimiwa Spika, suala la mkonge Mheshimiwa Waziri Mkuu nichukue nafasi ya kukushukuru sana na kukupongeza sana sana kwa kazi kubwa ambayo umetusaidia. Mkoa wa Tanga sisi uchumi ni mkonge, Tanga ukiizungumza ilikuwa ni mkonge lakini sasa umeamua kwa makusudi kabisa kwa maana ya Serikali kuturudishia heshima ya Mkoa wa Tanga kwa kurudisha suala la mkonge umesimamia yale mambo ambayo yalikuwa yakilalamikiwa na wakulima wadogo wadogo na sasa umeelekeza kwamba wale wakulima wadogo wadogo waendelee kupewa maeneo ili waweze kulima mkonge ambao kwa kweli wakishakuwa wamelima huu mkonge kwa vyovyote vile utawasaidia sana kuwainua kiuchumi mkoa wa Tanga ulianza kudorora kutokana na mapato ambayo tulikuwa tunayapata sana kutokana na mkonge kwa hiyo tunakupongeza sana kwa kazi kubwa ambayo umeifanya Mwenyezi Mungu akubariki kwa sababu wananchi wa Tanga wataendelea kukumbuka sana na wanaendelea kukuombea kwa Mwenyezi Mungu ikiwezekana urudi bila kupingwa huko kwenye Jimbo lako ili kusudi uendelee na mapambano haya katika kutusaidia katika haya masuala yanayohusiana na mkonge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliona kwa siku ya leo angalau niweze kuchangia haya machache nashukuru sana naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mary Chatanda, Kamishna wa Tume ya Huduma za Bunge nimeshakutaja Mheshimiwa Khadija Nassir na Mheshimiwa Mwambalaswa atafuata.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi kwanza kabisa nipende kuungana na viongozi wote ambao wameweza kutoa pole kwa Taifa letu na kwa dunia nzima kwa ajili ya hili janga la *corona*. Lakini pia nitoe pongezi kwa Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikikabiliana na hili janga.

Mheshimiwa Spika, pongezi pia kwa Serikali ya Awamu ya Tano kwa jinsi ambavyo imeweza kujipambanua kufanya mageuzi makubwa sana ya kimaendeleo katika sekta mbalimbali.

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza mambo tofauti tofauti ambayo kama nchi na Serikali tumeweza kuyafikia. Hotuba hii imeeleza ukuzaji wa fursa za ajira kwa vijana, lakini pia imeeleza vizuri uboreshaji wa miundombinu kwa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa. Hotuba hii pia imeeleza ufufuaji wa shirika ndege, ufufuaji wa mali za ushirika, ulinzi wa rasilimali zetu za nchi, ukarabati wa miundombinu ya elimu, uboreshaji wa huduma za afya na maji, upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa mijini na vijiji.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya niliyotaja na mengi ambayo sijayataja yanakwenda sasa kutekeleza moja kwa moja azma ya kuchochea uchumi wetu kwenda sasa kuwa uchumi wa viwanda. Baada ya pongezi hizo sasa niweze kwenda moja kwa moja kwenye mchango wangu na nitaanza kuelezea ukuzaji wa fursa za ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza hapa namna ambavyo imeweza kubuni uzalishaji wa ajira ambazo ni rasmi

na zile ambazo sio rasmi, lakini takwimu ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameitoa kwenye hotuba yake inaonesha kwamba ajira ambazo sio rasmi ni nyingi sana nchi kuliko zile ambazo ni rasmi. Vile vile tunafahamu ajira ambazo sio rasmi zinahitaji mambo mawili makuu; la kwanza mafunzo wezeshi, lakini pia vitendea kazi baada ya vijana kupatiwa mafunzo ambayo Serikali imeanza kuyatoa.

Mheshimiwa Spika, nafahamu Serikali ina Mfuko wa Maendeleo kwa Vijana na umekuwa ukifanya vizuri sana, lakini kutokana na uhitaji kuwa mkubwa Mfuko huu umeanza kuelemewa kwa mahitaji ambayo kama nchi tupo nayo. Sasa kwa kuzingatia hayo nina ushauri ambao nitatoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza, Serikali iweze kupunguza masharti kwa taasisi za fedha ili vijana ambao wataweza kupatiwa yale mafunzo waweze kupata mikopo ya kuweza ku-*practice* yale masomo ambayo watayapata na kuweza kujiajiri. Tunafahamu tulifanya marekebisho ya Sheria za Taasisi za Fedha ambayo yamekwenda sasa kufuta huduma ya *VICOBA* na zile taasisi ndogo ndogo ambazo mitaani zilikuwa zinawasaidia vijana na akinamama. Sasa tunaomba vijana watakapotoka kwenye zile *incubation programmes* waweze kupata angalau hata kama sio benki za biashara, benki ya maendeleo ambayo itaweza kuwapatia mikopo kwa masharti naafuu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa pili, kumekuwa na msongamano na uhaba wa vyuo vya stadi za kazi, sisi kama vijana tumelia sana hapa Bungeni angalau kila wilaya iweze kuanzisha Chuo cha *VETA* na kama wilaya hazitaweza basi angalau hata mkoa. Vyuo hivi ndio ambavyo vinakwenda sasa kutoa zile stadi za kazi ambazo tunazihitaji katika kukuza au kufikia ule uchumi ambao tunaita wa viwanda. Sasa hapa tumeona vyuo ambavyo vinatoa stadi hizo za kazi ni vichache nchini, lakini pia msongamano umekuwa mkubwa. Naomba Serikali iweze kulichukua hilo na kuweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, la tatu, Serikali iweze kuwa na takwimu ya vijana ambao wana vipaji maalum kwa hizi stadi

za kazi. Pia serikali iweze kuwa na takwimu ya vijana ambao tayari wameshapewa mafunzo ya kujiajiri. Kwa kufanya hivyo tutaweza kuona sasa ile elimu inashuka kwa jamii ambazo vijana inawazunguka, lakini pia tutarahisha kwa Serikali katika kuhakikisha kwamba vijana ambao hawana ajira wanaweza kupata hizo taaluma ambazo zinahitajika.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kwenye hili, napenda kutoa ushauri kwa Serikali angalau iweze kufikiria namna ya kutoa *intensive internship programs* kwa wale wanavyuo ambao wamemaliza. Tumekuwa na changamoto ya vijana kukataliwa katika ajira kwa kigezo cha uzoefu. Kwa kufanya hivi tutawawezesha sasa waajiri waweze kuwa *comfortable* kutuajiri sisi vijana ambao tunatoka chuoni moja kwa moja kwa sababu tayari wanakuwa na uhakika tumepata mafunzo ya kutuwezesha kuingia kazini vizuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo nitakwenda moja kwa moja kuongelea hali ya uchumi.

Mheshimiwa Spika, tumeona hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeongelea ongezeko la ukuaji uchumi, nawapongeza sana Serikali kwa hilo na niwapongeze Serikali kwa usimamizi mzuri wa ukusanyaji wa mapato. Pia niwapongeze Serikali kwa kuandaa mfumo mzuri wa ukusanyaji mapato. Kwa hayo mawili ndiyo *results* ambazo tunaziona sasa hivi. Vile vile kwenye hili ningependa kushauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali ifanye jitiahada ya kuangalia walipakodi wapya; tumekuwa tukiwakamua walipa kodi wale wale wa zamani bila ya kuangalia kwamba kila mwaka Serikali ina uwezo wa kukusanya walipakodi wapya na wakaweza kuingia katika kuchangia pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili, ningependa Serikali ione namna kuweza kuwatambua wajasiliamali ambao hawana ajira rasmi na kwa nchi hii ndio wengi. Tukiweza kuwatambua tukawapa elimu, tukaweza pia kuwashirikisha katika ukuzaji huu wa uchumi, nadhani watakuwa tayari na wao kuweza

kuunga mkono jitihada za Serikali na wao wakaweza pia kuingia katika kukuza pato la nchi.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuna wafanyabishara wengini na wajasiliamali ambao sasa hivi wamekuwa wakitumia ukuaji wa teknolojia katika kufanya biashara zao yaani *online business* na wana *make money* kuliko hata hawa ambao wameweza ku-*estabilish* biashara zao kwenye hii *proper arrangement.*

Mheshimiwa Spika, nchi zote duniani wafanyabiashara wakubwa ambao wamechipukia ni wale ambao wameweza kuona fursa katika ukuaji wa teknolojia. Nasema hivi sio kuwabana au kuwaminya, lakini naamini wao na mimi na sisi wengine Watanzania tupo tayari katika kushirikiana na Serikali kukuza pato la Taifa. Sasa tutakapowawekea *protection*, tutakapowaona na kwamba na wao ni *part* ya watu ambao wapo tayari katika kushirikiana na Serikali wataweza kuwa wa msaada mkubwa sana katika kukuza uchumi wa nchi, pia tutaweza kuwaona miongoni mwetu na wao pia wataweza kufaidika katika hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Spika, ya mwisho?

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Nassir kwa mchango wako. Nilishamtaja *Senator* Mwambalaswa atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo ipo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimwa Waziri Mkuu kwa kuwasilisha hotuba yake ya bajeti kwa umahiri mkubwa sana. Pia napenda kuungana na wenzangu kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ambayo amefanya kwa miaka minne hii. Serikali hii mtu atabeza atafanya nini lakini kazi waliyofanya ni wamefanya mapinduzi. Mapinduzi ambayo mtakapomaliza hii kazi nchi yetu hii itaingia kwenye uchumi wakati. Mungu awabariki muendelee kupiga mzigo namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia naomba niungane na wenzangu kwanza kukushukuru wewe, pamoja na uongozi wote wa Bunge, Naibu Spika, Katibu wa Bunge na viongozi wengine, kwa tahadhari ambayo mmeichukua hapa Bungeni kuhusu ugonjwa huu wa *corona*, nawashukuru sana sana. Mmetukinga Wabunge na Wafanyakazi wa Bunge, tuchukue tahadhari kubwa kwa sababu ugonjwa huu upo.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kuishukuru Serikali, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Afya kwa maelekezo ambayo wanatupa na wanawapa wananchi kuhusu ugonjwa huu, nawashukuru sana. Nawaomba wananchi wa Chunya, wananchi wa Mkoa wa Mbeya na Watanzania, tufuate maelekezo ambayo viongozi hawa wanatupa. Tuyafuate kweli kweli uongojwa huu upo na unaua. Nawaomba sana yote ambayo wamesema tuyatuate kwa umakini sana.

Mheshimiwa Spika, nataka katika hayo ambayo viongozi wetu wametupa niongeze kimoja kidogo nacho nisimu ya mkononi. Nawaomba sana simu ya mkononi kuanzia sasa ibaki yako wewe mwenye simu usiseme shika mwenzangu shika kidogo angalia *clip* hii hapana, ibaki kwako mwenyewe kwa sababu nayo inaweza kuwa njia ya kuambuakiza. Unaponawa mikono unatumia *sanitizer* chukua kitambaa cheupe safi na simu uisafishe kwa sababu nikwambie mimi nakuapia Watanzania tungekuwa tunashika dini zetu kama tunavyoshika simu, moto wa huko ungeishia

kuchoma mahindi, nakwambia kweli kabisa. Kwa hiyo naomba niongezee hapo kwamba tuwe makini sana na simu, simu yako ibaki yako, usimpe mwenzie, aangalie *clip* au apige salio limeisha, ubaki nayo na uisafishe mara kwa mara.

**SPIKA**: Waheshmiwa Wabunge mmemsikia *Senator* ushauri wake? Simu ibakie yako na watanzania pia kwa ujumla hasa wanawake wanapenda simu za wenzao. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwambalaswa endelea.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisaidia na kuniongezea uzito kwenye hoja hii. Nikiongelea hilo la simu Mheshimiwa Rais wetu katika ushauri wake ameongezea kwamba tutubu kwa Mwenyezi Mungu, tumfuate Mwenyezi Mungu tutubu dhambi zetu. Ukiona huko Italia wanateseka sasa hivi, wanaoana wanaume kwa wanaume, mtu jitu zima linamwingia mtoto wa miaka mitato wakati watu wakubwa wapo chungu nzima, ni dhambi ambazo Mungu amekasirika.

Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu nikiwa katika hilo niende kwenye kitabu cha Mungu. Nachukua Biblia watu nasikia wanasema bibilia, hapana, ni Biblia, katika wafalme wa zamani mfalme wa zamani mwana wa Daud. Baada ya kutawazwa kuwa mfalme alifanya vitu vingi vizuri *unique*.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza aliendа kuteketeza sadaka kumshukuru Mwenyenzi Mungu na Mungu akaongea naye akamwambia nikupe nini? Akamwambia unipe maarifa na uelewa ni waatawale watu wako vizuri. Hakuomba nguvu za kijeshi hakuomba utajiri, Mwenyenzi Mungu kampa vyote kampa hekima, kampa nguvu za kijeshi kampa na utajiri.

Mheshimiwa Spika, cha pili, alimjengea Mungu nyumba nataka nianzie hapo. Sasa ukienda kwenye kitabu cha Mambo ya Nyakati wa pili nianzie sura ya saba, aya kumi na moja baada ya Suleiman kumjengea nyumba Mungu. Hivyo basi, Suleiman akaimaliza nyumba ya bwana na

nyumba ya mfalme na yote yaliyomwingia Suleiman moyoni mwake ayafanye mwa bwana. Bwana akamtokea Suleiman usiku akwamwambia nimesikia uliyoyaomba na mahali hapa nimejichagulia kuwa nyumba ya dhabihu anasema Mungu sasa na Suleiman.

Nikizifunga mbingu isiwe mvua, tena nikiamuru nzige kula nchi au nikiwapelekea watu wangu tauni kama *corona* nikiwapeleka watu wangu tauni ikiwa watu wangu walioitwa kwa jina langu watajinyenyekesha nakuomba na kunitafuata uso na kuziacha njia zao mbaya, basi nitasikia toka mbinguni na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tumuunge Mheshimiwa Rais ametuambia hili tumrudie Mungu tuache dhambi ugonjwa huu utapita. Baada ya hilo naomba ningelee hilo ambalo wachimbaji wangu wa dhahabu wadogo wadogo wa Chunya wamenituma.

Mheshimiwa Spika, kwanza wachimbaji hawa wanaishukuru sana Serikali kwa kuweka soko la dhahabu pale Chunya, soko lipo vizuri, linaenda vizuri, wachimbaji wanapata pesa yao, Serikali inapata pesa yake na halmashauri inapata pesa yake. Sasa hii tafrani ambayo imetukuta sasa hivi wachimbaji wadogo wamekaa na dhahabu mkononi hawana kwa kuuza kwa sababu *broker* wa pale Chunya ni wale wenye mitaji midogo midogo na kwa kuwa sasa hivi ndege haziendi nje, kwa hiyo kwamba anunue dhahabu akauze Dar es Salaam arudi kununua tena hawana uwezo huo. Naiomba Serikali iingilie kati, hili kuna dhahabu nyingi sana zipo mikononi mwa wachimbaji wadogo wadogo naomba tuchukue hatua *interim period,* ijue aidha benki ziwakopeshe wale *brokers* au benki kuu iende kununua *in the interm period* ili wananchi wetu waende kufanya biashara kama kawaida.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nimeona kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kufufua kilimo na ushirika. Naongelea ushirika kwa kifupi, nimeshukuru sana nilipoona Serikali imemtuma TAKUKURU kwenda kukagua ushirika nchi

nzima, nimefurahi sana. Kwa sababu ushirika ndio umeua kilimo upo wapi ushirika wa zamani *KNCU,* upo wapi ushirika wa Nyanza *Co-operative* wa zamani, upo wapi ushirika wa Bukoba au wa Mbeya? Viongozi wa ushirika wameua ushirika, kwa hiyo umeua kilimo chetu. Nimefurahi sana kwamba Serikali imeliona hilo, imeanza kulishughulikia. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri wakomae sana katika hili, vilevile kumuachia *COASCO* yeye ndiye anakagua ushirika, hapana, naomba akague lakini na *CAG* naye aende kukagua ili kujiridhisha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, ahsante *Senitor.* Nilishakutaja Mheshimiwa Anatropia Theonest na atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Hadji Mponda na Mheshimiwa Ibrahim Raza. Mheshimiwa Anatropia hayupo! Mheshimiwa Hadji Mponda.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi ili nipate kutoa mchango wangu. Kabla ya hapa naomba tumshukuru Mwenyenzi Mungu aliyetujalia uhai mpaka tunakuwa na mazingira ya kukusanyika hapa pamoja na majanga mbalimbali tunawatumikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, niungane mkono na wenzangu walioanza na nakumbuka mwezi Novemba, 2015 Mheshimiwa Rais alikuja humu na wengine waliondoka. Hotuba ya Mheshimiwa Rais ilikuwa *so impressive,* ilikuwa na matumani makubwa sana na tunaona kwa miaka mitano yametekelezwa. Kwa hili tunampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli na kundi lake la Baraza la Mawaziri kwa kweli wametutendea haki, sina haja kutamka wametekelezaje ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo sisi tulienda kuahidi Watanzania tutawafanyia nini kwa miaka mitano, kwa kweli kwa kiasi kukubwa yamefanyika, pongezi sana kwa Serikali waetutendea haki. Sasa sisi wengine wa CCM tunatembea kifua mbele, maana yake sisi wa Morogoro

tunasema *manta* hofu maana yake tunatembea bila wasiwasi, tunaenda Oktoba hii tuna hakika tunawafyeka tena.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita zaidi kwenye hotuba hii ibara ya 43 mpaka 45, ni kwamba tumeendelezwa kupitia Dira ya Taifa kwamba ifikapo 2015 tutaingia uchumi wa kati, uchumi unaowezeshwa na viwanda. Hotuba aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkuu imeleeza, imenyooka moja kwa moja na hata ukiangalia Mpango wa Maendeleo wa 2020/2021 na hata bajeti imesisitiza na imetengeza vile vipaumbele vinne mojawapo ni kuwezesha uchumi wa viwanda ili twende huko katika Dira ya 2025.

Mheshimiwa Spika, hivi viwanda tunavyovizungumzia vikubwa vingi vinatokana na mazao ya kilimo na mifugo. Hali ilivyo kama tunataka twende huko kuwezesha hivyo viwanda ni lazima tuwe kilimo cha biashara na mojawapo ya sifa za kilimo cha biashara ni lazima muwe na miundombinu ya uhakika na usafiri na usafirishaji. Ni lazima muwe na maji, maji haya kilimo kinahitaji maji, tusitegemee ya mvua za Mwenyenzi Mungu, maji ya skimu za umwagiliaji. Tatu, tunahitaji nishati ili kuchakata mazao yetu, kuongeza thamani, na la nne ni soko la uhakika. Serikali naona wanatupeleka huko, lakini balaa la mwaka huu, maana mwaka huu ni changamoto kidogo, maradhi upande wa pili tuna mvua nyingi sana ambayo imeharibu miundombinu ya barabara na madaraja.

Mheshimiwa Spika, mfano tu ni barabara ambayo inapita katika ukanda mkubwa wa uzalishaji ambapo Serikali wamepeleka Mradi wa *SAGCOT* ambayo inaanzia Mikum – Ifakara – Lupilo – Malinyi - Kilosa Mpepo – Londo – Lumecha - Kitanga - Songea. Barabara hii ikiwezeshwa itatufikisha tunakokwenda kwenye uchumi wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja na ameona barabara hiyo, naipongeza Serikali wameanza hatua ya kuifanyia kazi kwa vitendo maana CCM inafanya kazi kwa vitendo. Mmeweka mkandarasi kile kipande cha

kilometa 70 kuanzia Mkamba - Ifakara, sasa ni mwaka wa pili, wa tatu mkandarasi yule anasuasua. Kila tukijiuliza hatupati majibu, Serikali tuambieni tatizo liko wapi, anatuchelewesha huyu na ndiyo maana upande wa pili wanapata ajenda. Tunakwenda kwenye uchaguzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu mwangalieni huyu mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkimaliza kipande cha kuanzia Ifakara mmeahidi mnakwenda kipande cha Ifakara – Lupilo - Malinyi - Songea, barabara hii ni muhimu sana. Kama tunataka kilimo cha biashara barabara hii ndiyo itawezesha kupeleka mazao haya kwenye soko na vilevile ndiyo itakuwa kivutio. Kilimo cha biashara tusitegemee hawa wakulima wetu wa kawaida wadogo wadogo, tunahitaji wawekezaji na mwekezaji hawezi kuja kwenye maeneo ambayo hakuna usafiri wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeahidi mara nyingi sasa ni wakati muafaka muanze kujenga barabara hiyo nayoizungumzia ambayo ina tija kwenye mwelekeo wa kumfanya Mtanzania aingie kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025 na wala siyo mbali. Habari njema bado tunaye Jemedari, mtu anayethubutu, Dkt. John Pombe Magufuli ndani ya miaka mitano atatufikisha huko kwenye uchumi wa kati 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, sipendi kuzungumzia huu ugonjwa mpya ulioingia ambao unasababishwa na Virusi vya Corona. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya UKIMWI na Madawa ya Kulevya. Tunaipongeza Serikali wamepokea ushauri wetu, wameufanyia kazi lakini kuna mambo mawili, haya naendelea kusisitiza kama wajumbe wenzangu walivyosisitiza tusije tukachanganywa na huu ugonjwa mpya, bado UKIMWI ni tishio.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka iliyopita bajeti ya kudhibiti ugonjwa wa UKIMWI tunategemea fedha kubwa kutoka kwa wafadhili, karibu mpaka asilimia 98. Sasa ifike wakati pamoja na changamoto hizo, tena habari ambayo

siyo njema tayari baadhi ya wafadhili wamepunguza msaada huo wao kwa asilimia 23.

Mheshimiwa Spika, niombe kwenye bajeti hii tuanze kuwekeza kwenye vita dhidi ya UKIMWI kwa fedha zetu za ndani angaliu asilimia 75. Tumelizungumza sana suala hili sasa tumefikia mwisho na Kamati inavunjwa lakini mtakuja mtukumbuke. Kama tusipowekeza kwenye vita dhidi ya UKIMWI kwa pato la ndani na huyu adui mwingine wa Corona aliyeingia ndiyo tutazidi kuchanganyikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kwenye UKIMWI ni Mfuko wa UKIMWI *(ATF).* Mfuko huu tunauzungumzia lakini bado una changamoto na sisi tumependekeza ikiwezekana wekeni tozo au kwa sababu ninyi mna wataalam tafuteni vyanzo vingine, vinginevyo huu Mfuko utabaki kuitwa Mfuko lakini hauna fedha, Mfuko maana yake ni fedha.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza sana kwa kunipa nafasi hii na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge ambao wako katika kumbi mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukumbi wa Msekwa niseme kwamba tunawatambua na tuko pamoja. Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wote kukumbuka kubonyeza pale kwenye *tablet* yako kwamba nipo, muhimu sana kwa ajili ya mahudhurio yetu.

Nilishamtaja Mheshimiwa Ibrahim Raza atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika,nichukue nafasi hii adhimu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi jana alivyotueleza namna ofisi yake ilivyokuja na mkakati wa bajeti hii ya mwaka 2020/2021. Mimi nipongeze Wizara zote zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kazi kubwa wanayofanya kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kwa kweli kwa miaka minne hii, tunakwenda mwaka wa tano (5) Wizara zote zilizo chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu zimefanya kazi kubwa sana akiwemo yeye mwenyewe Mheshimiwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amekuwa na kiungo mzuri sana katika kumshauri na kumsaidia Rais wetu Mheshimiwa John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sijakushukuru wewe, Kiti chako pamoja na Naibu wako kwa kuweza kutuongoza sisi Wabunge kwa kipindi cha miaka mitano. Kwa kweli kazi mliyoifanya ni kubwa, sisi Wabunge tunakushukuru sana tunakuombea maisha marefu wewe na Naibu wako, Mungu akupeni afya na umri na *Inshallah* Mungu awarejeshe tena katika jengo hili mwaka huu wa 2020. Amen. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipongeze Wizara zote ambazo zimetekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini nizipongeze sana Wizara ya Madini na Wizara ya Nishati. Kwa kweli katika kipindi hiki kidogo Wizara ya Madini imefanya kazi kubwa sana katika kubadilisha sheria zetu za ukusanyaji wa mapato. Kwa muda mfupi sana Wizara hii ya Madini imeweza kutuingizia mabilioni ya fedha katika uuzaji wa dhahabu, tanzanite na almasi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kusimamia hilo na vilevile nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri ambaye anasimamia Nishati, kwa kweli leo Watanzania kwa asilimia kubwa sana wanapata umeme mpaka vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile niipongeze Wizara ya Mambo ya Ndani kwa habari njema waliyotulea kwamba wamenunua mashine ya kuweza kutengeneza kadi za *NIDA* ambayo ime-*cost8.5 billion* na itaweza kutengeneza kadi za *NIDA* 9,000 kwa muda wa saa moja. Kwa kweli niipongeze

sana Serikali ya CCM ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije sasa katika suala hili la Corona. Corona ni janga la kimataifa na kila ukisikiliza taarifa za habari ni Corona tu sasa hivi. Nipongeze Serikali zote mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jinsi walivyochukua jitihada ya kuweza kusimamia masuala haya ya Corona na kuwaelimisha wananchi kwa ujumla na wale ambao wanaingia nchini.

Mheshimiwa Spika, nataka kumshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye ndiye anatuongoza na ndiye mshauri wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Kipindi hiki Watanzania wengi wanatumia maji, kila nyumba, mtaa na kila unapokwenda wanatumia maji. Maji yale pengine hata huyo mtu ambaye hana lakini anasaidiwa na mtu mwingine anaambiwa chukua ndoo ya maji hii nawia mikono.

Mheshimiwa Spika,mimi natoa ushauri lakini Serikali ndiye mwenye maamuzi ya mwisho. Ushauri wangu ni kwamba Serikali isamehe kodi ya miezi mitatu katika sekta ya maji kwa sababu sasa hivi kila mahali maji yanatumika. Kwa hiyo, ushauri wangu hii miezi mitatu Serikali isamehe kodi kwa wale wote ambao wanatumia maji akiwepo mtu wa chini mpaka mtu wa juu. Hii itatusaidia, watu watapata kidogo matumaini ya kuweza kuwasaidia wengine maji zaidi ya ndoo moja kwa sababu sasa hivi nyumba ambayo ilikuwa inatumia ndoo mbili ya maji au tatu kwa siku, sasa pengine inatumia ndoo zaidi ya kumi au kumi na tano.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu mwingine kwa Serikali yetu ya CCM, naomba sana kwamba labda hali ikizidi kuwa mbaya basi Serikali ichukue hatua ya kuweza kutuambia kwamba saa mbili za usiku ukiingia ndani mpaka alfajiri saa 12 ndiyo uweze kutoka kwenda kufanya shughuli zako za kiuchumi. Ikiwa hali itazidi kuwa mbaya, huu ni ushauri pia mzuri, wenzetu nchi nyingi duniani wameshaanza kwenda kwenye *lock down.* Hata juzi Dubai, Mascat na nchi nyingine za Ulaya ambazo tunazijua za Italy, Spain, London na nchi

nyingine zimekwenda katika *lockdown* kabisa *twenty four hours.* Mimi ushauri wangu iwe ni kuanzia saa mbili za usiku mpaka asubuhi saa 12, hii itasaidia kupunguza haya matatizo ya Corona. Huu ni ushauri.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ni naomba Jeshi la Polisi na Uhamiaji wawe makini sana katika hizi njia za panya. Watu watakuwa wanatoka nchi za jirani kuja huku Tanzania wakisema Tanzania Corona bado haijafika asilimia kubwa, watakuja kutuambukiza sisi. Watu wanapita njia za panya, kwa hiyo, Jeshi la Polis na Uhamiaji wawe makini sana katika hizo njia za panya wasije wakatuumiza huku kwa sababu sasa hivi huko nchi za jirani wameshaanza kuchanganyikiwa na masuala ya Corona.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli huu ndiyo ushauri wangu na kabla sijamalizia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli kila Mtanzania ni shahidi wa anayoyafanya Mheshimiwa Rais kupitia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Mimi nataka niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge humu ndani tusiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. IBRAHIM HASSANALI MOHAMMEDALI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ibrahim Raza, ahsante sana kwa mchango wako. Nimekwisha kutaja Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyowasilishwa na Waziri Mkuu hapa Bungeni. Na mimi

nitaanza mchango wangu kwa kujielekeza katika ugonjwa huu wa Corona.

Mheshimiwa Spika, watu wamekuwa na mitizamo kwamba ugonjwa huu siyo wa kutisha sana ukilinganisha na ugonjwa mwingine kama UKIMWI, kansa na magonjwa mengine. Hata hivyo, ni ukweli kwamba ugonjwa huu wa Corona unatisha sana kuliko magonjwa mengine kwa sababu ya njia ya uambukizaji wa ugonjwa wenyewe na unatishia uhai wa binadamu na umesababisha vifo vingi katika mataifa mbalimbali ulimwenguni tena kwa muda mfupi sana.

Mheshimiwa Spika, bado hatujaona jitihada za dhati za Serikali za kuhakikisha ugonjwa huu unadhibitiwa. Tumeambiwa na wataalamu na tumeona kwamba tunawe mikono, kwa kweli tunajitahidi kunawa mikono hata Watanzania wananawa sana mikono popote walipo. Tumeona shule na vyuo vimefungwa na mambo mbalimbali ikiwemo makongamano, semina, michezo mbalimbali vyote zimeahirishwa ili wasipate maambukizi haya ya Corona.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni hatua moja lakini bado hatujaona hatua nyingine katika maeneo yenye misongamano mikubwa mfano *stand* za mabasi, mabasi yanayotoka mikoani yanaingia kwenye miji mikubwa, kwenye mabasi kuna misongamano na tumeambiwa ugonjwa huu unaambukizwa kwa njia ya hewa. Sokoni tunakoenda bado kuna misongamano mikubwa sana. Kwenye magereza yetu kuna misongamano, magereza yetu yamejaa kupitiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukumbuke pia tuna *cell* zetu polisi ambazo wahaalifu kila siku wanaingizwa. *Cell* za polisi kwa utamaduni uliopo zinajaza wahalifu kupitiliza na hawapimwi. Mfano muhalifu akipatikana leo wala yeye hatawekwa kwenye chumba kingine cha karantini kwa siku 14 halafu achanganywe na wahalifu wengine kwa sababu hatuna hata hivyo vyumba vya kuwahifadhi katika vituo vyetu vya polisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,ndiyo maana nikasema hatua za awali zilizochukuliwa kukabiliana na ugonjwa huu bado hazitoshi, tunahitaji jitihada kubwa sana za kukabiliana na ugonjwa huu kwa sababu ya namna ambavyo unaambukizwa na jinsi ambavyo tumeona katika nchi za Ulaya, Marekani na China watu walivyokufa. Siyo huko tu, tujiangalie hata katika *block* ya Afrika Mashariki jinsi ambavyo ugonjwa huu umeweza kuuwa watu wengi.

Mheshimiwa Spika, kwa nini bado nasema Serikali inahitaji kujipanga sana kwenye ugonjwa huu wa Corona? Tuna maabara moja tu ambayo ndiyo inapima na kutoa majawabu ya watu walioathirika na virusi hivi vya Corona. Maabara hii ipo Dar es Salaam tu, hata hapa Makao Makuu ya nchi haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunajiuliza, kama mfano ikitokea kuna mgonjwa katika Wilaya ya Tanganyika labda kule Katavi au Kigoma mpaka sampuli iletwe Dar es Salaam itolewe majawabu, kama mtu huyu hajawekwa karantini huko aliko, kwa kweli tutakuwa tunajiweka kwenye wakati mgumu kama nchi. Serikali iliyopo madarakani nyie mmejipambanua kama ni Serikali wanyonge lakini tutawaonaje mkiwatetea wanyonge hawa wa Tanzania katika janga hili kubwa la Corona ambalo linauwa watu kwa upana mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tunahitaji kupata majibu na Serikali ituambie. Binafsi nilitegemea tulipoanza Bunge hili Serikali ingetuletea mkakati wa kina na wa dhati wa namna gani wanaenda kupambana na ugonjwa huu wa Corona. Tunajiuliza kama nchi hivi ongezeko likiwa kubwa, mpaka jana tumeona wagonjwa wamefika 20, tulikuwa na wagonjwa 13 leo wamefika 20. Tunajiuliza kama idadi hii ya maambukizi itaendelea kuongezeka, hivi tuna vitanda vya kutosha vya kulaza wagonjwa hawa? Tuna madawa ya kutosha kusaidia kama ambavyo wanafanya kwenye nchi nyingine, tunajua dawa haijapatikana lakini angalau kutibu katika zile hatua za awali? Je, tuna mashine za kutosha za kusaidia kupumua kwa wagonjwa hao? Kwa sababu

tumeambiwa ugonjwa huu unashambulia mfumo wa upumuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunajiuliza hivi tuna madaktari na manesi wa kutosha wa kuhudumia kama janga hili likiongezeka? Leo tuna upungufu wa asilimia 52 ya watumishi wa afya hapa nchini. Je, idadi hii ikiongezeka, hatuombi iongezeke kila mtu hapa anatishika kwa sababu ugonjwa huu ukija haijali wewe ni CCM, CHADEMA, CUF, Muislam au Mkristo, yeyote yule unaweza kumpata. Ugonjwa huu hauchagui mtu lakini tunajiuliza ni kwa namna gani Serikali mmejipanga tuone jambo hili linadhibitiwa kama ambavyo nchi zingine wameweza kudhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi na sijui kama Serikali mnakiri kwamba ugonjwa huu ukiendelea hapa nchini ni kwa hakika uchumi unakwenda kuanguka. Hili siyo la kubisha, uchumi wa nchi na wa mtu moja moja unaenda kuporomoka.

Mheshimiwa Spika,nitoe mfano, sekta ya utalii, mimi natoka Wilaya ya Karatu, tuna hoteli za kitalii 58, leo hoteli zinafungwa, wafanyakazi wanarudi majumbani, wengine wanarudishwa hakuna kazi tena mpaka pale ambapo hali itatengamaa. Hoteli hizo zinategemea watalii wengi kuja na watalii wetu wengi wanatoka nchi za nje na hawaji kwa sababu huko kwao tayari hali ni mbaya. Je, hapa hatujagusa uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa taifa?

Mheshimiwa Spika,lakini leo tunapoanza tu kujadili bajeti ya nchi kwenye sekta ya utalii tu Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro katika mwaka 2018/2019 inaingiza shilingi bilioni 143, kwa hali hii ya Corona hizi fedha tunaenda kuzipata? Hatuwezi kuzipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, je, hapa hatujagusa uchumi wa mmoja mmoja na uchumi wa taifa? Leo tunapoanza hata kujadili bajeti ya nchi, kwenye Sekta ya Utalii tu, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro katika mwaka 2018/2019 inaingiza

shilingi bilioni 143. Kwa hali hii ya *Corona* hizi fedha tunaenda kuzipata? hatuwezi kuzipata.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Waziri wa Fedha, lazima atuletee mpango wa haraka hapa Bungeni wa namna gani ya kukabiliana na suala la uchumi wa nchi na uchumi wa mtu mmoja mmoja hasa kutokana na janga hili la *Corona. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tusijifunze tu, tuangalie katika nchi za karibu tu hapa, kwa sababu kuna watu wanaosema kwamba tusitazame nchi zilizoendelea; Italy, Marekani na kadhalika. Hapana, hebu tutazame wenzetu wa jirani; Kenya na Uganda kwa hatua ambazo tayari wameshazichukua. Mfano tu mmoja, leo benki za Kenya zimetoa unafuu wa mikopo kwa siku karibia 90 kwa watu wao. Serikali ya Kenya imewataka wenye nyumba wawape nafuu wapangaji wasilipe kodi kwa kipindi fulani. Hii ni kwenda kumsaidia mtu mmoja mmoja kutokana na hali iliyoko. Sasa sisi kama Serikali ya hapa, watuambie wamejipangaje na jambo hili? Hili jambo halihitaji mzaha wowote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hapo hapo kwenye kuwasaidia wapangaji, tunashangaa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; kwanza mnakataza msongamano, yeye anaenda Mwenge, anaenda Ubungo, anakusanya watu, anaongea, anasema sijui naye anaanza kuongea na wenye nyumba wasamehe wapangaji. Hivi kweli tuko *serious*? Tumesema tufute misongamano yote kila mahali, kiongozi unaenda unakusanya watu.

Mheshimiwa Spika, halafu tunajiuliza, yeye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salam ndio amekuwa msemaji wa nchi hii? Suala la kuangalia namna gani wenye nyumba wanatoa unafuu kwa wapangaji, mimi nadhani lichukuliwe na Serikali lifanyiwe na...

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia, nilidhani sisi Wabunge tungekuja na mapendekezo kwa Serikali badala ya kuitegemea Serikali peke yake ndiyo ifikirie halafu ije na

mpango fulani. Pamoja na Serikali kutakiwa ikifirie, ije na mpango, lakini nasi tuwe tunapendekeza.

Nilikuwa nawaza tu, hili la kusema kwamba Serikali itoe amri, mwenye kajumba kake basi apangishe bure, sijui kama una nyumba yako halafu ipangishwe bure kwa sababu Serikali imesema, sijui kama... hebu weka sawa kidogo hili, maana yake, nilikuwa namwona Mheshimiwa Lema, maana yeye ni tajiri wa nyumba nyingi, sasa anasita hapo. Itakuaje hapo?

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nadhani hujanisikia vizuri, sijasema hivyo na nimeshauri kwamba Serikali ijifunze kwa majirani zetu katika *bloc* ya Afrika Mashariki jinsi wanavyofanya na tuangalie na sisi hali ya kwetu ikoje. Ndiyo maana nikashauri kwamba Waziri wa Fedha naye atuletee mpango wake kwa jinsi gani tunaenda kuangalia uchumi wa nchi utakavyoporomoka na hatua gani zitachukuliwa kwa uchumi wa nchi na kwa uchumi wa mtu mmoja mmoja. Ndicho nilichosema. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo ukatoa mfano kwamba Kenya imesema nyumba sijui imefanyaje.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Si unaona lilivyo gumu. Haya endelea Mheshimiwa Cecilia. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kingine ambacho Serikali inapaswa kukifanyia kazi na kuchukua ushauri huu, kama tatizo litaendelea, ni kwa kiasi gani kama nchi tuna hifadhi ya chakula? Huo nao utakuwa ni mtihani mkubwa sana kwa sababu tunaelewa hali ya watu wetu. Watu wetu ni wa kwenda asubuhi...

**SPIKA:** Mwaka huu chakula kingi sana. Hata kabla Serikali haijasema, kingi kweli kweli! Hata Dodoma hatuombi chakula mwaka huu.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama unasema kingi, basi Serikali ituletee taarifa hapa Bungeni kwamba ni namna gani inaweza kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula kama hali ya maambukizi ya ugonjwa wa *Corona* itaendelea na ugonjwa wagonjwa wataendelea wengi? Sasa hilo litakuwa la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema hayo kwa sababu tunaelewa watu wetu ni wa kwenda sokoni leo akanunue kitu kidogo apate riziki, siku iende kesho hivyo hivyo. Sasa kama ikifikia hatua wagonjwa wataongezeka, maana yake lazima tutaenda *lockdown.* Kama tutaenda kwenye *lockdown,* namna gani watu hawa tunahakikisha kunakuwa na chakula cha kutosha?

Mheshimiwa Spika, Serikali yoyote duniani panapotokea majanga na milipuko, jamani kitu cha kwanza ni mwananchi. Uhai na afya ya mwananchi, mengine ndiyo yanafuata*. (Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Naambiwa tayari. Malizia hiyo sentensi yako ya mwisho.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali, bado Watanzania wanahitaji majibu na mikakati ya dhati, Serikali iwaambie Watanzania kwamba namna gani inaenda kukabiliana na ugonjwa huu wa *Corona?*

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso. Naona Mheshimiwa Cecilia alikuwa anasisitiza, "ikitokea *lockdown,"* tunaombea Mungu kwamba ipishilie mbali hiyo

*lockdown* isitokee na naelewa kwa nini inazungumziwa *lockdown* ili kukwepa uchaguzi wa Oktoba, uchaguzi uko pale pale. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiea Amina Mollel. Watu wanataka *lockdown* ili uchaguzi uahirishwe, hakuna. Ratiba iko pale pale. Mheshimiwa Amina endelea*. (Makofi/Kicheko)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nakushukuru sana. Awali ya yote nitoe pole kwa Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC),* Waandishi wa Habari na wapenzi wote ambao wanafahamu kazi kubwa inayofanywa na Waandishi wa Habari kwa kifo cha Mwanahabari nguli hapa nchini Marin Hassan Marin. Hakika ni pigo kwetu wote na ni pigo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Marin anafahamika kwa jitihada zake katika kuhabarisha Umma wa Watanzania. Binafsi kama miongoni mwa niliofanya naye kazi, imeniuma sana. Niliingia *TBC* mwaka 2008 baada tu ya kumaliza Chuo Kikuu, Marin Hassan alinipokea na alinifundisha usomaji wa habari. Kwa kweli kwangu mimi pia, moyo wangu unalia kwa maumivu. Ombi langu ni kuiomba Serikali imuenzi Marin Hassan Marin kwa mchango wake mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na janga hili la ugonjwa wa *Corona* mwanamuziki Michael Bulton katika wimbo wake wa "*Learn on Me*," anasema kwamba *sometimes in our lives we have all pain, we all have sorrow*, lakini katika yote hayo anasema kwamba daima kuna kuwa na kesho. Nami naamini kwamba katika ugonjwa huu wa *Corona* Mwenyezi Mungu atatujalia na tutavuka salama. Taifa letu kupitia jemedari Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kazi aliyoifanya, ugonjwa huu ukija, naamini kabisa kwamba utatikisa. Kwa pamoja tumwombe Mwenyezi Mungu ili ugonjwa huo upite.

Mheshimiwa Spika, katika ugonjwa huu kweli tahadhali imetolewa, lakini siku zote nakwenda mbele zaidi hasa kama mwanamke mwenye ulemavu nawaangalia watu wenye ulemavu; je, elimu imewafikia vya kutosha? Kwa

mfano, tumeweka tahadhali kwamba kila mmoja wetu aweze kunawa. Je, kwa yule mtu asiyeona na hakuna watu pale wanaoweza kumsaidia, je, ataweza kujikinga na tahadhari hii?

Mheshimiwa Spika, siyo hao tu, hata viziwi huko mitaani, hawafahamu. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali na ninaishauri kuona umuhimu pia kwamba twende sote kwa pamoja kuhakikisha elimu inayotolewa hakuna anayeachwa nyuma ili basi maambukizi haya yasije kuwa athari kubwa pia kwa watu wenye ulemavu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina nakubaliana na wewe kuhusu elimu, ni muhimu sana. Maana wako watani zangu fulani wanauliza, hiyo *sanitizer* wanakunywa vijiko vingapi? Kwa hiyo, elimu ni muhimu sana. Endelea Mheshimiwa Amina Mollel*. (Kicheko)*

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwa kweli ninaipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Jemedari, *legendary* Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ndani ya miaka minne aliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, pia nampongeza Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Baraza lako la Mawaziri, kazi kubwa mmefanya. Wewe pia nikupongeze kwa moyo wa dhati kabisa kwa kazi kubwa uliyoifanya. Mimi ndani ya miaka minne nimejifunza na kushuhudia mambo mengi katika Bunge hili yakifanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nakupongeza wewe; na hasa nilipofika kwa mara ya kwanza, sikuwahi kupanda ghorofa ya nne na mara nyingi nimekuwa nikisumbua. Nakumbuka katika mojawapo ya bajeti nilishika shilingi huku kusema kuhusu lile jengo la utawala na ukaahidi kwamba litawekwa *lift.*

Mheshimiwa Spika, wewe ni mtendaji na unaposema, kinafanyiwa kazi. Hongera sana, kwa mara ya kwanza hatimaye niliweza kufika ghorofa ya nne kwa sababu wakati mwingine mbali ya wasaidizi, kuna mambo ambayo inabidi tufuatilie sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa nini naipongeza Serikali hii? Naipongeza kwa sababu nimezungumza mara kwa mara humu ndani, kwamba tangu tumepata uhuru, kwa kweli masuala ya watu wenye ulemavu yalikuwa nyuma sana na kipaumbele changu mimi katika Bunge hili tangu nimeingia, ukiniuliza; namba moja ni walemavu, namba mbili ni walemavu na namba tatu ni watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii ya Waziri Mkuu, kupitia kwa Jemedari wetu hatimaye alikuwa na jicho la ziada na kuhakikisha kwamba ndani ya Baraza la Mawaziri kunakuwa na mtu mwenye ulemavu ambaye pacha wangu Mheshimiwa Ikupa ninakupa pongezi kwa kazi kubwa uliyoifanya katika kuhakikisha kwamba unawashauri Mawaziri wenzako, unaishauri Serikali na mara kwa mara tumekuwa tukiwasiliana na kuziwasilisha kero mbalimbali ambazo leo hii ninajivunia na kusimama kifuambele kwamba yamefanyiwa kazi. Hongera sana kwa hilo, Bunge litakukumbuka na Watanzania watakumbuka*. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fungu Na. 65 linahusu masuala ya watu wenye ulemavu. Katika Bunge la 2017, Februari 2, niliishauri Serikali juu ya kitengo cha watu wenye ulemavu. Vilevile Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu leo hii nasimama hapa na kusema ahsante kwa Serikali yangu kwa kuwa yote haya yamefanyiwa kazi. Naomba tu sasa badala ya kuwa kitengo, hatimaye sasa ije kuwa Idara kamili katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2017 nilishauri pia kuhusu Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu kwa sababu haukutengewa fedha. Ninaposimama hapa leo hii ninatoa ushuhuda kwamba mfuko huu kazi nzuri imefanywa na umeweza kutengewa bajeti.

Mheshimiwa Spika, tarehe 14 Novemba, 2017 niliuliza swali na kuitaka Serikali kuleta Mkataba wa Marrakesh. Mkataba huu unawawezesha watu wenye ulemavu, wasioona kuweza kupata kutafsiri, yaani vitabu na majarida mbalimbali yatakayowawezesha wao kupata elimu. Ninaposimama hapa mwaka 2019 Mkataba huu wa Marrakesh uliletwa na hatimaye Bunge hili likaupitisha. Naipongeza sana Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016 katika Wizara ya Afya nalileta marekebisho ya kifungu cha Sheria nikiwataka, nanukuu: "Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali wa mwaka 2016 ambao katika bodi itakayoteuliwa na Mheshimiwa Waziri na kwa sababu nafahamu changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu, kifungu cha 7, nilipendekeza kifungu cha 3 kiletewe mabadiliko...

*(Hapa kengele iilia kuashira kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Amina.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Naomba nimalizie tu kwa kusema kwamba Serikali hii imefanya kazi kubwa sana, ninaipongeza sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza kwa kuwa na jicho la ziada na kuweza kutoa ushirikiano mkubwa kwa Mheshimiwa Ikupa na hatimaye naye ameonesha kwamba kuwa na ulemavu siyo kulemaa, watu wenye ulemavu tunaweza.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana sana Mheshimiwa Amina Saleh Mollel kwa mchango wako. Niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kupitia *tablets* zenu, wale wote ambao mko humu ndani na ambao wako katika kumbi nyingine kwamba mnaweza mkaendelea kuchangia kwa maandishi, mkituma kupitia utaratibu tuliojiwekea kwenye

*tablets* zenu na taarifa zote zitamfikia Mheshimiwa Waziri Mkuu. Wakati watakapokuwa wanajibu siku ya mwisho, mahitimisho hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na wasaidizi wake, basi hoja zenu zitazingatiwa na zile za kimaandishi pia kwa wale ambao hamtapata nafasi ya kusema au wale ambao mmepata nafasi ya kusema lakini kwa vile muda ni mdogo, kuna mambo mengine ambayo ungependa kwa nyongeza pia yafike, basi fanya hivyo. Maandishi yote hayo yataingia pia katika Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard).*

Mheshimiwa Vedasto Ngombale, atafuatiwa na Joseph Mbilinyi. Karibu Mwenyekiti wa *LAAC*.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili basi nami niweze kuchangia katika hotuba ya mtani wangu Waziri Mkuu. Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa wasilisho zuri la jana, ameonesha umahiri mkubwa, Watanzania wameelewa vizuri na wameelewa utendaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nianze na wazo la kuzitaka Halmashauri kwamba mapato yake ya ndani, zile asilimia kumi zigawanywe kwa akina mama, vijana na watu wenye ulemavu na likapitishwa kuwa sheria. Ni jambo jema sana na Halmashauri nyingi sasa zimeanza kutekeleza vizuri ingawa zipo ambazo zimeanza kukwama, zinaanza kuzalisha madeni. Ukiwauliza kwa nini mnafanya hivyo? Kati ya sababu wanazozisema ni pamoja na kwamba wanakosa vikundi sahihi vya kuvipelekea fedha hasa katika asilimia mbili.

Mheshimiwa Spika, ziko Halmashauri nyingine mapato yake ya ndani ni makubwa sana. Asilimia mbili kwenda kwa walemavu inafikia wakati kwamba wanakosa sasa walemavu waliopo kwenye vikundi ili waweze kupata zile fedha matokeo yake wanashindwa kupeleka zile fedha. Sasa naomba hili Serikali waliangalie kwa makini, kwa sababu vinginevyo upo uwezekano walemavu uwezo wa kuwaweka kwenye vikundi ni mgumu na wanashindwa kupata hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwamba kama hivyo ndivyo, basi walemavu wana yale mahitaji yao maalum kulingana na aina ya ulemavu waliokuwa nao; na mpaka sasa hatujawa na utaratibu maalum wa kuhakikisha mahitaji hayo yanapatikana.

Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel, nilitegemea unasikiliza, hoja muhimu hii. Endelea Mheshimiwa Vedasto.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, kwa mfano, katika maeneo ya vijijini walemavu wa ngozi hawana uelewa wa kwamba kuna mafuta maalum kwa ajili ya kuboresha ngozi zao. Hawajkui lolote, hawajui kabisa na Serikali haijatenga na hatujawa na fungu maalum la kuhakikisha hawa walemavu wanapata elimu, lakini ikiwezekana wanapata hayo mafuta.

Mheshimiwa Spika, viungo bandia vinauzwa kwa bei ya ghali sana. Ikitokea mlemavu anataka kupata kiungo bandia cha mguu, ni bei ghali sana na Serikali haijawa na mpango maalum. Ila shime sikio, fimbo nyeupe, kama hivyo ndivyo, naishauri Serikali ije na waraka maalum kwamba kama wanashindwa kupeleka zile asilimia mbili kwa vikundi vyote, basi hizo fedha zitumike ili wawanunulie walemavu mahitaji maalum kulingana na aina ya ulemavu waliokuwa nao. Hii itakuwa ni msaada sana kwa walemavu. Naomba hilo lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine nizungumzie vitambulisho vya wajasiriamali. Serikali ilikuja na utaratibu huu wa vitambulisho vya wajasiliamali na vikagawiwa kwa wajasiriamali kwa mchango wa shilingi 20,000/=. Hivi karibuni kumekuwa na utaratibu ama kusitisha au Serikali kama haijaeleza nini sasa kinafuata, lakini katika baadhi ya maeneo kwa mfano kwangu mimi pale Kilwa Kaskazini maeneo ya Somanga maeneo mengine, watendaji wamewanyang'anya wajasiriamali vitambulisho ambavyo tayari wameshanunua.

Mheshimiwa Spika, ni mbaya sana Wajasariamali wamenunua vitambulisho Watendaji wanakwenda kuwanyanganya vitambulisho bila hata kuwarejeshea na hawatoi maelezo ya kina kwa nini wanaamua kuchukua vile vitambulisho. Naomba Serikali ifuatilie hilo kwa sababu vinginevyo kunakuwa na mkanganyiko miongoni mwa wananchi, na wananchi wanaiona kama Serikali imewahadaa jambo ambalo nafikiri hilo liwekwe vizuri ili wananchi inapotokea tena Serikali ikija na *program* ya aina hiyo waipokee na waone tija ya jambo kama hilo kufanyika.

Mheshimiwa Spika, tuzungumzie suala la maafa, Ofisi ya Waziri Mkuu ndio inashughulikia mambo ya maafa na majanga. Nichukue nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka huu umekuwa ni mwaka wa Majanga na maafa na kutokana na mvua zilizokithiri, tuna mafuriko kule kwangu maeneo ya Njinjo, kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na sasa hivi Mto Rufiji umefurika kwa hiyo tuna matatizo, tuna matatizo makubwa ambayo Ofisi ya Waziri Mkuu inatakiwa iangalie kwa kina.

Mheshimiwa Spika, na kati ya jambo ambalo limejitokeza ni pamoja na kuharibika kwa miundombinu ya Serikali ikiwemo Shule, Vituo vya Afya, kitu ambacho au jambo ambalo linapelekea kwa mfano katika Tarafa ya Njinjo shule nne miundombinu yake imeharibiwa kabisa na maji mpaka leo tunavyozungumza kuna zaidi ya wanafunzi elfu tatu hawana sehemu ya kusoma, niombe Serikali iliangalie jambo hili kwa uharaka kuhakikisha watoto wale wanapata sehemu ya kusoma kwa sababu hili ni janga na suala la kupata elimu ni jambo la muhimu nani haki ya watanzania wote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ungezitaja ingekuwa vizuri zaidi kama unazikumbuka hizo shule.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, kuna Shule ya Msingi Njinjo, kuna Shule ya Msingi Ndende, kuna Shule ya Msingi Msitu wa Simba na Shule ya Msingi Wenje, hizo shule haziwezi tena kutumika ninaomba sana Serikali iwaangalie wananchi wa Jimbo la Kilwa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jingine nizungumzie Vita ya Majimaji nahii marazote ninavyochangia hotuba ya mtani wangu Waziri Mkuu lazima niseme hili kwa sababu ndio kilio cha watu wa Kilwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu watu wa Kilwa wanaomba kwa kuwa Vita ya Majimaji imeanza Kilwa, wanaomba sana Serikali itenge bajeti ya Sherehe ya Vita ya Majimaji kama ambavyo inafanyika Songea na sisi watu wa Kilwa tupate hiyo haki. Wanaomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu nafikiri mtani wangu utakuwa umenisikia. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nizungumze suala la Corona, suala la Corona Waheshimiwa Wabunge mbalimbali wamezungumza Serikali imechukua hatua ni jambo jema...

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

## TAARIFA

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Vedastus pokea kutoka kwa Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Naomba nimpe taarifa jirani yangu kwamba vita vya Majimaji vilianzia Rufiji katika Kijiji cha Tawi sio Kilwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Namuona *Chief Whip* nae ameniandikia hapa kwamba vita vya Majimaji vilianzia Songea na sio Rufiji wala Kilwa. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa sijui nani ataamua ugomvi huo, Mheshimiwa Vedasto endelea.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya ndugu yangu Mchengerwa siipokeu kwa sababu yeye anajua kwamba Vita ya Majimaji ilianzia Kilwa katika Kijiji cha Nandete na Majemedali wake anawafahamu kama kina Ngulumbalio, Mandali, Ndimio Machela na wengine wakina Kinjekitile Ngwali na wengine. Kwa hiyo, hiyo inafahamika na tunavyo vitabu na hatuna haja, Mheshimiwa

Jenista analifahamu hilo kwa hiyo naomba hilo tuliache, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu alizingatie hilo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nazungumzia suala la korona kama ambavyo...

**SPIKA:** Kwa hiyo Kinjekitile alikuwa Mngindo!

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Alikuwa Mngindo na alikuja Kilwa kama mganga wa kienyeji.

**SPIKA:***Okay (Makofi/Kicheko)*

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Yah! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Corona imezungumzwa na niipongeze Ofisi yako ya Bunge kwa hatua ambazo tulichukua kwa ajili ya kuzuia lakini naomba suala la Corona lipate uhalisia. Kama wewe, Wabunge wako umewaelekeza kuchukua tahadhari kule kwa wananchi bado mambo hayajakaa sawasawa kuna mikusanyiko ya hovyo, ya holela naomba Serikali ikaze uzi kidogo. Hatuna sababu mpaka leo kwamba mabaa tunayo yanaendelea tu kiholela holela, hatuna sababu kwamba ukienda feli kwa mfano hata usafiri wetu na namna tunavyosafiri bado hatujakaa vizuri.

Mheshimiwa Spika, niiombe Serikali ikaze uzi kidogo kwa sababu vinginevyo tusipoziba ufa tutakuja kujenga ukuta hali itakuwa mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, jingine nizungumzie suala la Bima ya Afya kwa wote. Miaka mitano tunamaliza tuliahidiwa hapa Serikali italeta Muswada wa Sheria wa Bima ya Afya kwa wote lakini mpaka sasa hivi Serikali ni kama inasuasua. Wananchi wa Tanzania wanapata shida sana kwa sababu ya kutokuwa na uhakika wa namna ya kupata huduma ya matibabu. Serikali ije na Muswada wa Sheria kwa ajili ya Bima ya Afya kwa wote sijui kwa nini Serikali inalega lega nafikiri hili lingefanyika basi wananchi wangekuwa na uhakika wa kupata huduma ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kipato cha mwananchi wa kawaida akipata maradhi yoyote uwezo wa kumudu matibabu kwa fedha za mfukoni ni ngumu sana lakini tukumbuke ya pia, *CHF* imefeli imeshindwa lazima tuwe na mpango mwingine. Mheshimiwa Jenista naomba ujitahidi utuletee huo Muswada wa Sheria ili basi tuhakikishe tunawapatia wananchi wetu huduma ya uhakika ya matibabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedasto asante sana.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Spika, asante sana nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, nilishakutaja Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na utafuatiwa na Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, na Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa ajiandae.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa hii ni bajeti ya mwisho katika miaka mitano. Naomba nimpongeze sana Mwenyekiti wa CHADEMA na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Mbowe kwa Uongozi wake imara wa kujenga upinzani *credible* na sio upinzani magumashi pamoja na yote anayokutana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nawapongeza Wabunge wenzangu wote wa CHADEMA tuliovuka, ambao hatukuunga mkono kwa sababu tumevumilia sana miaka mitano hii Awamu ya Tano haikuwa rahisi, siasa zilikuwa zinahusika na magereza kushambuliwa, kupigwa risasi na mambo mengine mengi tu ambayo tumeweza ku-*survive* mpaka hapa tulipofika kwa kweli nawapongeza sana Wabunge wenzangu kwa kuvuka uvuli wa mauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la Corona lipo chini ya Waziri Mkuu, naomba nianzie huko. Kwanza lazima tuelewane hapa, suala la Corona sio suala la kiimani ni suala la sayansi. Na ndio maana hata Papa mwenyewe, mimi ni

mkatoliki amefunga Vatican na Italy yote hawaendi kanisani hata *St. Peters Basilika* ambapo kila jumapili maelfu kwa makumi ya maelfu ya watu duniani kote na Waitaliano wanasali pale juzi Papa amesali peke yake kwa sababu ya kuchukulia umakini wa suala hili. Hili suala sio la kiimani na imani tunayo kwa mfano sisi Wakatoliki tuna imani lakini tunaamini sayansi na ndio maana kila unapokuta Kanisa Katoliki lazima utakuta shule ya Chekechea na Zanahati kwa sababu tunaamini katika Sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Corona ni *pandemic*, wakishasema kuna *epidemic*, ilianza kama *epidemic*saa hizi inaitwa *pandemic* hakuna suala la kutishana hapa, ni suala la ku-*discuss* kwa kina. Corona inaua na itaua mamilioni, ndivyo wanasayansi wanasema hivyo tusipochukua hatua. Tushirikiane kukabili na hili, tusilete siasa kwenye hili na niwapongeze sana Zanzibar kwenye hili Zanzibar wamechukua hatua sana wamefanya vizuri sana, unamuona pale yule Waziri wa Afya, yupo *on point* kila time kujaribu ku *update* hali ya mambo inavyokwenda. Corona sio tatizo la Ummy Mwalimu na Wizara ya Afya, maana yake watu Ummy, Ummy, Waziri wa Fedha anahusika, Waziri wa Biashara anahusika Waziri wa Uwekezaji anahusika kwa sababu biashara zinakufa.

Mheshimiwa Spika, BOT wako kimya tu kwa hiyo tunaangalia tu upande wa vitanda matibabu tutakufa ni kweli huko tupo ovyo lakini njia pekee ya kuidhibiti korona kwa nchi maskini kama sisi Tanzania ni kudhibiti isisambae. Sasa nyinyi mnasema mbona hamwagi nini ile ham*sanitize* miji, kama Arusha, mgonjwa wa kwanza tulitakiwa tuone hata yale magari ya polisi basi yale ya washawasha, wekeni dawa yamwage maji mitaani, mnasubiri mpaka muwamwagie maji CHADEMA wazee! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, m-sa*nitize* miji angalau ile ambayo imeanza kupata shida ndugu zangu, hiyo ndio njia ya pekee ya ku-*contain* ili isisambae sana, Ikisambaa sana hatuwezi *ventilators* tunazo mia moja na hamsini tu. Tunavyoambiwa tunazo mia moja na hamsini tu, wakati Jiji la New York

wanahangaika zifike laki moja na nusu, sisi kama Taifa la watu milioni hamsini na saba tunazo mia moja hamsini tu, Itakuwa balaa hapa. Spain wanafikia *time* wanasema wazee wa miaka themanini wasipewe vitanda vya ICU kwa sababu vitanda vimeisha hapa tutatumia vigezo gani au kukata, shika laki mtoe Sugu muweke Mheshimiwa Jenista na kadhalika, kwa sababu tutafanyaje. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala la korona ni *serious,* hata kama sisi sio UK hata kama sisi sio Italy, hata kama sio US lakini tuangalie wenzetu wa sub-Sahara wanafanya nini, sub-sahara in Africa, Kenya. Basi tusiwaambie wenye nyumba wasitoze kodi kwamba nyumba nyingi hapa ni za watu binafsi na ni masikini wanategemea hizo kodi kusomesha watoto. Lakini watoto si hawaendi shule, elimu si bure, *okay* tusifike huko tuweke unafuu kwenye yale ya Serikali, hii Serikali si ina hela hii mara ya mwisho Mheshimiwa katuambia tuna akiba ya dola za kutumia miezi sita. *Where is that money, bring that money* tupange bajeti hela ya bajeti ya Mwenge, bajeti ya Mwenge haitoshi kwenye corona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haitoshi watu wanapanga bajeti za kufa mtu, bajeti kubwa na mikakati. Kenya Serikali inatoa miongozo, umeme, maji hivyo ni vya Serikali. Mseme bwana tuko vizuri nchi hii tajiri umeme, maji iwe bure kwa wananchi ili kuwaletea unafuu kuanzia sasa ili pale anapopanga ule mchango wa LUKU, mchango wa maji usiwepo tutakuwa tumewapa unafuu wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mabenki Kenya yamesitisha marejesho ya mikopo kwa biashara na makampuni. Hili sio suala la wananchi maskini, hili suala ni la kitaasisi, Mheshimiwa Dkt. Mpango *this is yours* na BoT, sitisheni wekeni breki kwenye marejesho kwa sababu bila hivyo hizi biashara zitakufa Corona inakuja kupita Mungu anatusaidia tutashindwa kunyanyuka kwa sababu hakuna biashara itakayonyanyuka na Serikali haiwezi kuajiri watu wote na itakuwa shida sana kwetu sisi sote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sugu naona kila jambo una *copy and paste* from Kenya.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, hapana nitakupa mfano wa Ghana Serikali ipo *serious*, Ghana imesema wananchi kuanzia Jumapili hii wote wakae ndani Taifa zima linaenda kupimwa kwa sababu huwezi kujua ukubwa wa tatizo bila vipimo. Hii hapa mnasema eti tuko ishirini, ishirini tupime humu tu Bungeni hata mimi mwenyewe sioni kama niko *guarantee* na niko salama.

**SPIKA:** Tunaposema Mheshimiwa Sugu, hiyo unayosema Ghana wanasema watu wote wakae ndani ili Serikali ya Tanzania unayosema watu wote wakae ndani ili Oktoba uchaguzi kule Mbeya uhairishwe, hiyo sasa ndio tunasema haiwezekani.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwenye uchaguzi nakuja, naomba tu utunze muda wangu.

**SPIKA:** Muda wake muutunze. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Muutuze muda wangu, kwenye uchaguzi nakuja, tuko vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naongea habari hizi *serious* sana, nyakati kama hizi zinaitwa *defining moments.* Nyakati kama hizi ndio *leadership* inapimwa, tutoke tuonyeshe *leadership* watanzania wanatuangalia. Kwa sababu hawa watu wanatushangaa kwamba aaah korona wanasema tunanii mbona wao wapo Bungeni eeeh! Kwa hiyo, lazima humu ndani tuwaonyeshe kwa nini tuko Bungeni, tujadili vitu vya kuokoa maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kauli yake kuwa uchaguzi utakuwa huru na wa haki, umezungumzia uchaguzi nakuja huko. Uchaguzi uwe huru na wa haki Mungu atupunguzie makali ya Corona ili tufike salama Oktoba, Mungu atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ili kutuhakikishia kwamba uchaguzi huu uwe huru na wa haki Rais achukue hatua chanya ku-*support* kauli zake. La msingi kabisa ili wadau wa uchaguzi, wa ndani, wa nje, wa kimataifa maana yake uchaguzi ni suala la wote, wadau wawe na imani nae wawe na imani na kauli yake kwa kuanza kabisa tunataka Tume huru. Tume ambayo watendaji wake watawajibika kwa tume na sio kwa mteuzi ambaye ni Rais. Tume ambayo yenye kinga na ulinzi wa kikatiba ya ajira za wale watendaji wa Tume kama ilivyo kwa majaji, kama ilivyo kwa *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Isiwe rahisi kumchomoa Mtendaji Mkuu wa Tume hajatangaza tu hajamtangaza Sugu kesho hawi Mwenyekiti wa Tume, *that isvery bad.* Kuhusu Mbeya na Uchaguzi Mkuu kule tunasema hivi, Tume huru bila Tume huru lazima tutoboe mradi wananchi wametupa kura. (Makofi))

Mheshimiwa Spika, *by the way* Mbeya mimi hamjawahi kunipa kwenye *silver plat*. Uchaguzi wangu wa 2010 alikufa mtu mmoja kwa ajili ya kulinda kura, uchaguzi wa 2015 vilema watatu wengine mpaka leo nawahudumia. Uchaguzi huu na maisha yalivyokuwa magumu sijui mtatuzika wangapi Mbeya hata Corona inaweza ikawa na nafuu lakini sio kuchakachua uchaguzi huu kwa kigezo chochote kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana yake nawaona tu sasa hivi hawasemi tena kama kule Mbeya, hawasemi tena Sugu hashindi wanasema Sugu hatatangazwa, utafikiri nimewahi kutangazwa wakati nimelala nyumbani. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka Tume huru, yenye uwezo wa kuteua wasimamizi na watumishi wake yenyewe isiteuliwe, na haya maelezo yote haya tumeiweka kwenye hotuba ya KUB lakini pia yamo kwenye barua yetu tuliyomuandikia Mheshimiwa Rais kumpa mapendekezo ya tunaenda vipi Oktoba baada ya sisi kutoka Mwanza kwenda kuonesha kitambaa cheupe kwamba tupo tayari kwa maridhiano nilikuwepo kwenye ile...

**SPIKA:** Mheshimiwa Sugu, samahani kidogo kuna taarifa nadhani ni Naibu Spika au ni nani taarifa, malizia Mheshimiwa Sugu. *(kicheko)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kama chama tumeandika barua kwa Mheshimiwa Rais mpaka leo haijajibiwa kutoa mapendekezo yetu, tunaenda vipi kwa amani kwenye uchaguzi wa Oktoba. Msisitizo wake na msingi ukiwa Tume huru. Kama Tume huru na haki basi turuhusiwe katika sehemu ya hizo haki turuhusiwe kupinga matokeo ya Rais Mahakamani. Mbona matokeo ya Mbunge tunapinga, ile mwaka 2010 yule alinipinga nikamtuliza na Mahakamani mwaka 2015, hakupinga kabisa kwa sababu kura zilikuwa ni nyingi mno. Mwaka 2020 hata njia ya Mahakamani hamtaiona nyinyi kwa Mbeya Mjini,hamtaiona hata njia ya Mahakamani. *(Makofi/Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa Mheshimiwa Spika.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunataka tume huru tunataka sheria, Marekebisho ya Sheria za Uchaguzi, tunataka marekebisho ya Sheria za Uchaguzi…

**SPIKA:** Kengele imeshagonga tayari Mheshimiwa Sugu.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:**…ili Rais nae akichakachua tumshitaki Mahakamani kwamba amechakachua uchaguzi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mchengerwa utafuatiwa na Mheshimiwa Osca Rwegasira Mukasa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza niweke kumbukumbu sawa kuhusu hili ambalo limezungumzwa na ndugu yangu Mheshimiwa Vedasto kwamba vita vya Majimaji vilianzia Rufiji katika Kata

ya Mbwala, Kata ambayo inapakana na Vijiji vya Kilwa na eneo hili la Nandete ambalo amelisema ni Vijiji vilivyopo Rufiji, Nandete pamoja na Tawi. Lakini pia ikumbukwe hata huyo mpiganaji Kinjekitile Ngwale alinyongwa katika mti uliopo pale Muholo ambao umeng'oka hivi karibuni tu, kwa hiyo, vita hii ilianzia Rufiji haikuanzia Kilwa naomba niweke kumbukumbu sawa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa, kuna mwangwi inanipa tabu kujua taarifa hii inatoka wapi!

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Kuchauka.

**SPIKA:** Aaaah! Mheshimwa Kuchauka Mbunge wa Liwale.

**T A A R I F A**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumzia vita ya Majimaji. Muasisi wa vita ya Majimaji ni Kinjekitile Ngwale, Mngindo, na wakati ile vita inaanza Kinjekitile Ngwale alikuwa Iringa anaendelea kukusanya majeshi huku nyuma wanakijiji wa Kijiji cha Nandete walikwenda badala ya kupalilia mashamba ya pamba walifyeka pamba zote ndipo Wajerumani wakaja na nguvu wakaanzisha ile vita wakati Kinjekitile Ngwale bado yupo Iringa. Kwa hiyo, nimpe taarifa kwamba ile vita ya Majimaji ilianza Kilwa na chanzo chake ni wakulima walipokwenda kufyeka pamba badala ya kupalilia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimwa Spika, taarifa hii siipokei kwa sababu vita ya Majimaji ilishaanza mapema na Kinjekitile alitafutwa kwa kuwa alikuwa mganga tu wa kienyeji, lakini yeye hakuwa muasisi wa vita hii.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:**Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa kuna taarifa, endelea Mheshimiwa Muhagama. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba nimpe taarifa babu yangu Mheshimiwa Mchengerwa kwamba Kinjekitile Ngwale alikuwa mganga wa kienyeji aliyewadanganya wapiganaji wa vita kwamba maji yanaweza kupunguza makali ya risasi na ndiye aliyesababisha tushindwe ile vita ahsante. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa. *(Kicheko)*

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii naipokea imekaa vizuri. Pamoja na hotuba nzuri iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu iliyosheheni matumaini na ujenzi wa Tanzania mpya, nina imani kubwa sana kwamba vipaumbele vya Taifa letu sasa vimeimarisha hali ya ujenzi si wa Taifa peke yake bali ya ujenzi wa wazalendo wapya. Vipaumbele hivi ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu amevitoa visingefanikiwa kama Taifa hili lisingelikuwa na Jemedari Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Joseph Pombe Magufuli ambaye yeye kwa uchapa kazi wake, uhodari wake amechangia kwa kiasi kikubwa sana Taifa letu sasa pengine kesho, keshokutwa linaweza likawa ni Taifa ambalo linajitegemea lenyewe.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imejikita katika mambo mengi hususani katika kilimo, afya, miundombinu, maji, umeme, mafuriko pamoja na eneo hili la *Corona* na mambo mengine mengi. Tuwaombe tu Watanzania kuhusu eneo hili la *Corona* kwamba ni vyema Watanzania wakafuata ushauri unaotolewa na Wizara ya Afya, lakini pia ushauri unaotolewa na Kamati zilizoundwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kamati za Maafa za Mikoa pamoja na zile za Wilaya. Kwa hiyo Watanzania waaache viburi, Watanzania waache ujuaji namna pekee ya kuwaokoa Watanzania ni kufuata maelekezo yanayotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, hakuna namna nyingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba imekuwa nzuri sana kama ambavyo nimesema Mheshimiwa Waziri Mkuu amegusia eneo hili la mafuriko. Ikumbukwe tu kwamba Rufiji hakuna mvua hata moja inayonyesha, mvua zinanyesha Nyanda za Juu Kusini, pia ikumbukwe tu kwamba eneo kubwa la Rufiji liko kwenye bonde, kwa hiyo maji yote ya mvua na maji ya kwenye mabwawa mbalimbali hapa nchini yanakuja Rufiji na hii imepelekea robo tatu ya Rufiji yote sasa iko kwenye maji. Mafuriko haya hayakuanza juzi japokuwa nitambue mchango mkubwa wa Ofisi hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu lakini lazima tukiri kwamba wataalam wetu walichelewa kutufikia Rufiji na hiki kwa kweli ni kilio cha wananchi wetu wa Jimbo la Rufiji.

Mheshimiwa Spika, tatizo ambalo naliona si lingine isipokuwa sababu kubwa ni Fungu 37 hatukutenga fedha kwenye hichi Kitengo cha Maafa hakuna fedha na badala yake tunategemea zile Ofisi za Maafa za Mikoa na Wilaya. Niiombe pengine Bunge kwa kuwa sasa eneo hili Mbunge wa Jimbo ndio anawajibika kuwahudumia wananchi na ikumbukwe nchi hii ni ya wananchi na mfariji namba moja kwa wananchi ni Serikali, hii ni kwa mujibu wa Ibara ya Nane ya Katiba ambayo inasema nchi ni ya wananchi. Basi, tuwaombe Wizara kuangalia uwezekano sasa wa kutenga fungu kwenye hili Fungu la maafa ili wataalaam wetu pale ambapo wanasikia taarifa za maafa iwe rahisi wato kutufikia.

Mheshimiwa Spika, japokuwa zaidi ya familia 20,000 zimekosa makazi, zimekosa vyakula, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ilituletea baadhi ya vitu ambavyo kwa kweli ni vichache hususan kwenye eneo hili ambalo lilikuwa eneo la maafa. Walituletea ndoo ambazo zilikuwa tupu nadhani unaweza kuona wananchi wa Rufiji wanachohitaji ni faraja hawahitaji ile huruma ambayo pengine wanapaswa wasifanye kazi hapana wanachohitaji ni faraja kidogo ambayo pengine Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inasema tunacho chakula cha kutosha kwa zaidi ya asilimia 110, hii haijapata kutokea toka nchi yetu imepata uhuru. Vyakula vilivyopo leo hii ni zaidi ya asilimia 110, naamini ofisi hii haishindwi kuja

kutuletea hata kama vyakula vikikosekana, hata mbegu za msaada ili tuweze kupanda pale maji yanapokuwa yametulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mafuriko yameleta maafa makubwa katika kila sekta kwa mfano vipo vituo vya afya ambavyo vimezingirwa na maji na vingine havifai kabisa. Eneo la maporomoko ya mto yamekikumba Kituo cha Afya cha Muhoro, tayari ofisi yetu ya Wilaya Ofisi ya Mkoa tumekwishaandika barua TAMISEMI kuweza kuomba fedha za dharura ili wananchi wetu waweze kujengewa kituo cha dharura kwa sababu eneo hili la Muhoro lina wakazi zaidi ya 25,000.

Kwa hiyo niombe Ofisi ya Rais TAMISEMI, watakapokuja kufunga hapa watuambie iwapo kama kuna fedha hizi za dharura ambazo tunatambua kwamba zipo waangalie uwezekano wa kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, leo hii wananchi wa Muhoro wanakosa matibabu, japokuwa tunatambua kwamba maji yameanza kuondoka taratibu, japokuwa yapo mabwawa mengine ambayo yemefunguliwa hivi karibuni, maji haya yanaweza kuchukua muda mrefu kwa kuwa mafuriko ndio kwanza yataanza mwezi huu mwezi wa nne kule kwetu Rufiji. Kwa hiyo tuwaombe Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa fedha za dharura kuweza kuona uwezekano wa kuwaangalia wananchi wetu wa Kata ya Muhoro kwa kutoa fedha hizo ili tuweze kujenga kituo kuwahudumia wananchi zaidi ya 25,000 ambao kwa leo hawana hawapati huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, mafuriko yameathiri ikiwa ni pamoja na mradi wetu wa kuzalisha umeme mradi ule wa Mwalimu Nyerere. Tunapata kigugumizi wakati mwingine pale ambapo tunamtafuta Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kumweleza maafa ya mafuriko kwenye mradi huu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi hajawahi kufika Rufiji kupitia barabara ambayo mradi huu unaelekea. Barabara kubwa inayotumika ni barabara ya Kibiti kuelekea Mroka lakini Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi hajawahi kufika Rufiji kupitia

barabara hii, pengine anasubiri Mheshimiwa Rais akiwa anakwenda yeye ndio aje Rufiji kupitia barabara hii. Hata nilipozungumza naye alisema amewaagiza wataalam wake kupeleka vifaa kupitia Morogoro. Vifaa hivi vinatoka Mtwara Dangote, inawezekana vipi vitoke Dangote vipite Pwani, vipite Dar es Salaam viende kwenye mradi wa umeme.

Mheshimiwa Spika, mradi huu wa umeme kama kweli Taifa letu limedhamiria ukamilike wakati Mheshimiwa Rais wetu Magufuli akiwa madarakani, basi ni vyema wataalam hawa wakafika maeneo haya, barabara hii...

**SPIKA:** Ni barabara unayoongelea Mheshimiwa?

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, ni barabara ya Kibiti - Mroka. Barabara ya Kibiti - Mroka imeharibika na magari makubwa yameharibu barabara hii hata mafuriko ya mwaka 62 barabara hii iliendelea kupitika lakini leo hii barabara hii haipitiki, inachukua masaa 10, barabara hii inahitaji tu utatuzi...

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa unapata taarifa toka kwa Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa Mbunge anayeongea Mheshimiwa Mchengerwa mjukuu wangu kwamba mvua zilizonyesha ni mvua za *return period* ya miaka 100. Wakati tunaanza mradi wa kujenga Bwawa la Nyerere mkandarasi alipewa barabara tatu; barabara ya kwanza ni hiyo Kibiti - Mroka, njia ya pili ilikuwa ni kwenda na *TAZARA,* anakwenda mpaka eneo la Fuga na tuliimarisha na ile barabara ya kutoka Fuga kwenda kule, nayo imeimarishwa vizuri, lakini barabara ya tatu ilikuwa ni ya upande wa Morogoro na yeye amekuwa anatumia zaidi ile barabara ya kule kwa Mheshimiwa Mchengerwa kwa sababu ni kweli ni fupi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mvua zilizonyesha kuna kipande cha mita 200 ambacho kuna bwawa lipo eneo lile, limeungana na mafuriko ya Mto Rufiji na kile kipande kina maji ya kina cha mita mbili, kwa hiyo hakuna namna yoyote gari linaweza likapita. Kwa hiyo, mkandarasi sasa hivi atapita Fuga au atapita njia iliyoko kule upande wa Morogoro. Kwa hiyo nilitaka kumpa taarifa kwamba hii ni *nature* ambayo hatuwezi kufanya chochote kwa akili ya kawaida ya mwanadamu. Naomba avumilie tu Mheshimiwa Mchengerwa baada ya mafuriko kupita na barabara ile kukauka basi hatua nyingine zitafanyika.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, tunachoomba Mheshimiwa Waziri apite kwenye hii barabara ajionee. Hii barabara miaka yote toka mafuriko ya 1962 mafuriko ya 1974, mafuriko ya 1998, 1988, 2018 barabara hii iliendelea kupitika, leo hii wananchi wangu wanatumia masaa 10 kupita barabara hii, mimi mwenyewe nimepita, yako matrekta yanapita pale kinachohitajika ni kifusi tu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la aibu kwenye mradi huu, mradi unatekelezwa Rufiji, waathirika wa kwanza watakuwa ni Warufiji, lakini cha kushangaza Mkurugenzi wa Kinondoni anaomba *service levy* ya utekelezaji wa mradi. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aeleze hapa, mradi huu uko Rufiji, unatengenezwa Rufiji, Warufiji ndio watu wa kwanza kuupokea kupitia Mbunge wao, lakini mpaka leo *service levy* haijalipwa Rufiji, watu wa Kinondoni wanaitaka *service levy*,. Angalia ajira 3,300 Warufiji waliajiriwa ni 200 kati ya ajira 3,300, tukiuliza ni upande wa nishati, hatupati majibu; tukimuuliza mkandarasi yeye ameweka watu tu, kwa hiyo athari zakwanza za mradi huu zitawakuta wananchi wa Rufiji na sisi ndio watu wa kwanza kuupokea mradi huu hatuna tatizo hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye *Hansard* hotuba yangu ya mwaka mwezi Novemba, 2016, nilipambana na Mheshimiwa Waziri Muhongo aliyekuwa Waziri wa Nishati wakati ule kuomba utekelezaji wa mradi

huu tunachoomba Warufiji wapate haki hata kama kidogo; hatuna nishati, hatuna madini, hatuna *Tanzanite,* tuna mradi huu, hiki ndio kitu pekee tulichonacho. Tunachoomba Wizara hizi mbili ziwaangalie Warufiji kwa sababu ndio watu wa kwanza utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa. Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa nilikwishakutaja na atafuatiwa na Mheshimiwa Almasi Athumani Maige.

**MHE. OSCAR R. MUKASA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa namna ya pekee kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa afya na uhai na tunaendelea kumwomba atusaidie kwenye hili dhoruba ambalo linaikumba dunia kwa sasa. Napenda pia nichukue nafasi hii kwa kuendelea kuwashukuru wananchi wa Biharamulo kwa kuendelea kuniamini na kuniunga mkono kwamba tunaendelea kufanya shughuli za maendeleo. Tatu niipongeze Serikali; Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli; Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia; Waziri Mkuu, Mheshimiwa Majaliwa; na Mawaziri wote kwa kazi nzuri. Kazi ni nzuri, ni wazi hakuna mtu anaweza akamaliza matatizo yote duniani kwa miaka mitano. Kwa hiyo tunachoangalia hapa ni hatua imepigwa na imepigwa kwa kiasi gani, kwa hiyo nawapongeza kabisa tumesikia hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeainisha kabisa kazi zilizofanyika.

Mheshimiwa Spika, mahususi kwa Biharamulo lakini pia inagusa Taifa zima, naipongeza Serikali kwa ule mpango wa kuja na miradi ya kimkakati kwenye halmashauri. Sisi Biharamulo ni moja ya halmashauri za Wilaya ambazo tulifaidika na jambo hilo na tumepata mradi wa ujenzi wa maegesho ya maroli kwa sababu pale Nyakanazi njiapanda ya kwenda Kigoma, Rwanda na Kahama ni mradi mkubwa sana maegesho ya maroli na stendi kubwa ya mabasi na soko, mradi mzuri sana. Hata hivyo, napenda kutoa wazo hapo kwamba awamu inayofuata hebu Serikali tujikite

kwenye wazo zuri la miradi ya kimkakati, hebu tutumie mashirika kama haya ya hifadhi kama ya *NSSF* na mengine, kuyaunganisha na halmashauri ili sasa miradi hii iwe, sawa ipo ya upande wa huduma, lakini sasa twende kwenye upande wa uzalishaji, kwa sababu ukiangalia stendi ya mabasi na maroli ni mradi wa huduma, halmashauri itapata kipato, lakini tukienda kwenye miradi ya uzalishaji nafikiri tutafungua fursa zaidi.

Mheshimiwa Spika, Biharamulo ni kitovu cha wafugaji na mnakumbuka vita ya hifadhi na wafugaji *center* mojawapo ilikuwa ni Biharamulo, tuna wafugaji wengi na sasa hivi baada ya hii kampeni ya kuondoa wafugaji hifadhini, wafugaji bado hawajapata namna sahihi ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi. Kwa hiyo hii miradi ya kimkakati, tukiyaunganisha na haya mashirika ya hifadhi ukatumia hiyo fursa ukatengeneza kitu ambacho kinabadilisha ule ufugaji wao unakwenda kibiashara zaidi, nafikiri kuna nafasi pale tutatoka kwenye huduma tunaenda kwenye uzalishaji, kwa hiyo nawapongeza Serikali lakini ni vizuri tukaenda mbele zaidi tukaongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nigusie pia ugonjwa wa *Corona* maana yake ndio suala la sasa, ni vizuri kuligusia kidogo. Nianze kwa kujaribu kuweka kumbukumbu sawa, nimemsikia Mheshimiwa Sugu akiunganisha imani na sayansi, nataka kuseme tu kwamba, sayansi ni zao la elimu na elimu ni moja ya mapaji ya Roho Mtakatifu, kwa hiyo sayansi na elimu ni matokeo ya imani. Sasa kinachosemwa hapa sio kwamba watu kuwa na *laissez faire,* watu wajae Kanisani bila utaratibu, lakini pia sio kwamba kama wengine wamefikia hali ya kufunga Makanisa na sisi tufunge, hata kama hatujafikia, sisemi hatujafikia lakini tuipe nafasi Serikali na Serikali wafanye kazi yao ya ku- *control,* ku- *balance* vizuri *panic* na *laissez faire,* nafikiri ndio kazi kubwa ambayo Serikali tunatakiwa kufanya.

Mheshimiwa Spika, kwenye *Corona* hapo hapo pia ningemwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, nampongeza sana kwa kazi nzuri inayoendelea sana kabisa, lakini hebu kama

alivyosema tujaribu kuwashauri kuliko kuwashambulia na kuwawekea presha, naomba tuongeze kidogo nguvu kwenye ile *multisectoralapproach* ya kupambana na *corona* kwamba sio suala la afya kama ambavyo Mheshimiwa Waziri Mkuu ndio amelichukua.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Serikali kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu ilizuia ilifunga shule ambayo ni hatua ya awali nzuri kabisa, lakini hivi tunavyoongea kuna mahali watoto wanakwenda kufanya masomo ya ziada *tuition*, sasa hilo ukimsubiri Mheshimiwa Waziri wa Afya utachelewa, kuna Wakuu wa Mikoa tuwaambie wafanye kazi yao , kuna Mawaziri wanaohusika wafanye kazi yao, wazuie hiki kitu. Hatua ya kwanza wameshafunga shule, watu waelewe kwamba tumefunga shule ili kuwaondoa watoto kwenye hatari kwa sababu wao sio rahisi kufuata maelekezo, lakini sasa kama huko nyuma watu wanawapeleka kwenye masomo ya ziada, ina maana hata hii jitihada ya kwanza ya kufunga shule unaipunguzia nguvu yake.

Mheshimiwa Spika, ushauri kwa Serikali nzima *of course* kupitia Wizara ya Afya, sasa hivi nimeona kwenye Mtandao hapa wasilisho zuri kabisa la Wizara ya Afya linaonyesha ramani ya *case* zetu ziko wapi, wapi una wale *contacts* unaotafuta kwa wingi vizuri kabisa Dar es Salaam, Arusha, Kagera na Zanzibar, maana yake ni kwamba tunatarajia kwa ramani hii Dar es Salaam na Arusha nguvu ya kupamba tuisikie ni tofauti kuliko kwingine kwa sababu hatuwezi kufanana. Kwa hiyo tujaribu namna ya huu mtawanyiko wa ramani ambao tunaupata kutoka kwa watalaam tusaidie kufanya mambo yetu kwa kusukuma kwa ngazi ya utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nizungumzie kidogo namna ya kutumia rasilimali kidogo tulizonazo kwa tija kubwa zaidi. Najua Serikali tunafanya hivyo kwenye maeneo mengi, lakini kuna eneo moja ambalo ningeomba nilisemee. Nilipata fursa ya kwenda Chuo Kikuu cha Teknolojia Nelson Mandela Arusha, Chuo Kikuu kile tofauti na Vyuo Vikuu vingine, Vyuo Vikuu vingine vyote kazi yake ni ile *academic excellence* yaani ubora kwenye taaluma lakini

Chuo Kikuu kile zaidi *academic excellence* wanakwenda kwenye ubunifu, wanafanya ubunifu kila *Master'sdegree* inayotoka pale au *Ph.D* lazima itoke na ubunifu wa jambo fulani ambalo linakwenda kutatua tatizo kwenye jamii, lakini wanakwama kwenye pesa za uwatamizi wa ubunifu huo.

Mheshimiwa Spika, vile vile wanakwama kwenye namna gani tunaweza tukachukua ubunifu uliofanyika pale kuuleta kwenye mazingira ya viwanda na mazingira ya sera ili ubunifu huo utumike kwa Taifa zima; kwa mfano, wana ubunifu wameufanya wa teknolojia inaitwa *non filter,* Mtanzania kijana ametengeneza chombo cha maji kinachuja uchafu wote, sasa ameshindwa kuchuja chumvi, lakini uchafu mwingine wote wote anauchuja na maji yanaweza kuwa safi na salama na wamepata tuzo ya *WHO* na kwingineko wanatambulika kidunia. Sasa tutafute namna ya kimfumo ambapo sisi watunga sera tunaweza kuwa tunakwenda kule kuwa na *appetite* ya kujua kule kuna nini na kuchukua kuingiza kwenye sera. Kwa mfano hili la maji lina faida kwa Wizara ya Afya na kwa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, kuna utafiti hapa unaonyesha vifo vya watoto kwenye nchi za Afrika Mashariki vimepungua, lakini vingepungua zaidi endapo tungekuwa tumeshughulika kwa kiwango kikubwa zaidi tulichonacho sasa kwenye habari ya maji ya kunywa ya watoto na vitu kama hivi. Pia ninao utafiti mwingine wa watu wa maji wanasema mpaka sasa hii *informal access* ya maji ni kubwa zaidi kuliko *formal.* Kwa hiyo huyu mtu mwenye teknolojia hiyo Nelson Mandela ukimtengenezea mazingira watunga sera tukaenda, tukawa *appetite* ya kwenda kuchukua ubunifu na kuingiza kwenye sera, watu wengi zaidi hata kama sio wote watapata fursa ya kupata maji salama ya kunywa na kutumia na hivyo itakuwa kazi ya wanasayansi ni kufanya ubunifu, sisi ni kuchukua na kutengeneza mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tukiwa na chombo *independent* kidogo kinaongozwa labda na Rais mmoja mstaafu ambaye bado ana nguvu ya kukimbiambia, kina Makatibu Wakuu wawili wa nguvu, kina Wabunge wawili,

watatu, halafu Spika labda ni mlezi, kinatengeneza *appetite* ya kwenda kwa wabunifu kuchukua mambo ya kupandisha kwenye *policy*, basi itatusaidia sana na nchi hii itabadilika na kutumia rasilimali kidogo tulizonazo kwa ajili ya kupata matoke makubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Oscar Rwegasira Mukasa. Sasa nimuite Mheshimiwa Bobali nilikutaja Mheshimiwa Almasi Maige kwanza, Mheshimiwa Almasi Maige halafu Mheshimiwa Bobali, halafu Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Nchi katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza naomba nitoe shukurani na najua wewe mara nyingi unasahau kwa sababu unawahudumia wengi, unawasaidia wengi. Mimi umenisaidia sana kufika hapa nilipo, ulikuwa chachu ya mimi kugombea Ubunge kutoka katika Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Katiba nikukumbushe wakati Wapinzani walipokataa hati ya Muungano na wakawa tatizo kubwa sana na hata mlipotupa Hati ya Muungano, Wapinzani wakasema imefojiwa, mimi nilishawishi nichangie kutoka katika lile kundi la 221 na nikasema mimi na mtu mmoja wa upinzani wanipe hiyo hati tuipeleke Ubalozi wa Marekani tukaangalie tu wino kwa sababu walikuwa na uwezo wa kusoma wino wa miaka kabla ya kuzaliwa Nabii Issa, watuambie tu huo wino umeandikwa lini wakati marehemu Karume yupo au baada ya kufariki marehemu na ikawa ndiyo maziko ya suala la Hati ya Muungano iliyofojiwa, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika,tangu nimeingia hapa Bungeni huu ni mwaka wa nne, umenisaidia mambo makubwa mawili. Kwanza nilileta Muswada Binafsi wa Sheria ya Sekta ya Ulinzi.

Kwa kweli ulinisaidia sana, uliupokea Muswada ule ukafanyiwa kazi na Bunge na mapendekezo yakaenda Serikalini, Serikali wakauchukua Muswada huo watauleta kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani. Hiyo ni kumbukumbu ya mambo uliyonisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hivi karibuni nimekuletea Hoja Binafsi ya kutaka lugha ya Kiswahili itumike kama lugha ya kufundishia. Bunge limeifanyia kazi na kuniandikia mimi tena nilipeleke suala hilo au hoja hiyo kwanza ipate maoni ya Chama change. Chama changu wanalifanyia mchakato hoja hii na baadaye wataniarifu itakuwaje. Haya ni mambo makubwa sana kwangu mimi na nitakuwa nimeweka alama kubwa katika Bunge lako kwa msaada wako. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais na hasa kwa matendo yake makubwa ya kusaidia nchi hii kuipeleka mbele katika miaka mitano ambayo amekuwa Rais na kitaifa lakini pia katika Jimbo langu amefanya mambo makubwa sana. Ameniletea maji kwenye vijiji vyangu vyote karibu asilimia 48, umeme wa *REA,* kituo cha afya, hospitali ya Wilaya, kituo cha *VETA* shilingi bilioni 5 na ananijengea Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi katika Kata yangu ya Magiri, Kijiji cha Malampaka. Mambo haya siyo madogo, namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kitendo chake cha kuishi ndani ya mambo aliyoyafikiria Mheshimiwa Marehemu Baba wa Taifa hasahasa misingi ya Azimio la Arusha na mimi ninalo. Hili hapa ndiyo Azimio la Arusha ambalo lipo na kila nikilisoma hili linanikumbusha mambo yangu ya miaka 1965 nilipotembea kilometa 50 kuunga mkono Azimio hili. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuliamsha dudu hili la Azimio la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwenye mambo muhimu ya kuchangia katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza nimshukuru Waziri Mkuu kwani yeye ni tofauti na Mawaziri

Wakuu wote niliowafahamu. Nakiri kwamba nimefanya kazi na Mawaziri Wakuu waliopita lakini Waziri Mkuu huyu ni muungwana, mpole lakini anayependa watu.

Mheshimiwa Spika, hata nilipokuwa nalalamikia tumbaku ndani ya jengo hili na hata nilivyofanya kosa la kwenda kumshtaki kwake Waziri wa Kilimo hakuchukua hatua yoyote mpaka alipokwenda Tabora kuthibitisha niliyoyasema na baadaye akachukua hatua nzuri sana na tukauza tumbaku. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ni mtu wa watu, anapenda wanyonge, amefanana sana na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,pia nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, huyu binti wa Kingoni, mweupe maana sisi Wanyamwezi watu weupe, mara anikatishe tamaa aniite baba, mara aniite kaka, akikumbuka mambo yangu ya zamani kwamba nilikuwa Rais wa Afrika ananiita bosi, mara aniite mzee hata sijui ananiita nani sasa. Namshukuru sana kazi maana zake ni nzuri sana na ameongoza Wizara hii kwa nguvu sana. Mimi jina langu kwake na roho yangu nyeupe ni mtani wangu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika,lakini pia ana Mawaziri wadogo wawili...

**SPIKA:** Nataka kumwambia tu Mheshimiwa Jenista, Wanyamwezi hawazeeki.

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Ni kweli kabisa. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Maige. *(Kicheko)*

**MHE. ALMASI A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniongezea hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niwashukuru Mawaziri wadogo wawili, ndugu yangu Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa. Hawa nimewajua mimi nikiwa Mwenyekiti wa Waajiri Tanzania.

Mheshimiwa Spika,katika mchango wangu nitachangia mambo ya kazi na ajira lakini pia mambo yanayohusu tozo zile za *SDL.* Nianze na suala la kazi na ajira. Sisi waajiri na naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni mwajiri na ni Mkandarasi Daraja la Kwaza, bado tunategemea kwamba Serikali itafanya mpango wa kupunguza *SDL* kutoka asilimia 4.5 iliyopo sasa mpaka asilimia 2 kulingana na watu wengine walioko huko Duniani hasa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulikuwa tumepanga kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kazi na Ajira kurekebisha sheria za kazi ambazo zimepitwa na wakati. Sheria hizo hazikurekebishwa na mapungufu yake tunayaona sasa. Wakati huu imetokea Corona tunafunga biashara, tunafanya watu wasiende makazini lakini hakuna nafuu kwa mwajiri, tunaendelea kulipa mishahara na hii tunaona kwamba siyo sahihi. Kama ingekuwa sahihi basi kwenye hili la *force majeure* kwa maana ya jambo lililotokea nje ya waajiri na wafanyakazi ilitakiwa tupewe nafuu wote wawili.

Mheshimiwa Spika, lipo suala la Vyuo vya Ufundi Stadi (*VETA),* mimi na wenzangu waajiri tunaamini kwamba bado Vyuo vya Ufundi Stadi *(VETA)* kuendelea kuwa chini ya Wizara ya Elimu ni makosa. Mwanzo iliwekwa vile kwa sababu tulikuwa tunatafuta hela za mikopo ya wanafunzi sasa hivi tunakusanya hela zinakwenda kwenye *central account,* kwa hiyo sababu ile imekufa, siyo muhimu tena. Tunaomba *VETA* kwa sababu ni Vyuo vya Ufundi Stadi vinafundisha wafanyakazi wetu ambao wako chini ya Wizara ya Kazi na Ajira virudishwe tena chini ya Wizara ya Kazi na Ajira kwa maana hakuna sababu ile kubwa iliyokuwepo ya kukusanya hela kwa ajili ya mikopo kwani hela zinakwenda kwenye *central account.*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee Mfuko wa Fidia. Mfuko wa Fidia ulipoanzishwa tuliunga mkono na ulikuwa na wigo wa matawi mawili tu kwamba utakusanya tozo kwa waajiri wa umma yaani *public* na sekta binafsi. Sasa sisi tukawashauri kwamba hapana wapanue wigo ili waajiri

wenye kazi za hatari na zenye madhara walipe zaidi halafu waajiri wenye kazi salama na hazina madhara walipe kidogo kwa mfumo huo huo kwamba wale wa *public* na wale wa binafsi.

Mheshimiwa Spika, tulifanya stadi Waziri aje na matokeo ya stadi hiyo ilisemaje. Sisi Waajiri tunaamini kwamba ni muhimu sana sana kuwe na sababu ya kupanua wigo ili hela nyingi zikusanywe kwa sababu ya kufidia wafanyakazi wetu watakaoumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwishoni nina ukakasi. Uwakilishi ndani ya Bunge letu katika muktadha wa ajira na kazi ni wa utatu na utatu huu unasajiliwa na kusimamiwa na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* ambao ni wa Serikali, Waajiri na Wafanyakazi. Nauona huu uwakilishi katika Bunge lako kwa theluthi mbili. Naiona Serikali chini ya Waziri Mkuu na Mawaziri wake, nawaona wafanyakazi, Majimbo mawili ina maana Wabunge wawili walioingia humu Bungeni kupitia wafanyakazi lakini siwaoni waajiri.

Mheshimiwa Spika,najua tulipotokea siku za nyuma ilitakiwa iwe hivi kwa sababu waajiri ndiyo waliokuwa mabepari na makabaila na tulitaifisha mali zao lakini yameshapita hayo, tusiendelee kuganga yaliyopita. Hivi kwa nini hivi sasa kusiwe na uwakilishi wa waajiri humu ndani? Kasoro itakuwa nini? *Iam thinking loudly,* tatizo ni nini kuweka uwakilishi wa waajiri?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kwa kweli naunga mkono mambo yote yatakayoongelewa katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Wizara ya Kazi na Ajira.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Almasi Maige. Nilishakutaja Mheshimiwa Hamidu Bobali lakini Mheshimiwa Frank Mwakajoka ampishe Dada yake kwanza Mheshimiwa

Anatropia yeye atakuja baadaye kidogo. Mheshimiwa Hamidu.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii.

Mheshimiwa Spika,awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema. Pia nitoe pole kwa Wanachama wenzangu wote wa Chama cha Wananchi *CUF* kwa kuondokewa na Katibu Mkuu wetu Mheshimiwa Maalim Khalifa. Nikupe pole wewe pia najua ni mtu uliyefanya naye kazi muda mrefu hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, nianzie na suala la Corona. Nilitaka tu niongezee kitu kimoja na naunga mkono hoja yako kwamba tuishauri Serikali. Ushauri wangu mimi ni kwamba Serikali iongeze ulinzi kwenye zile hoteli zilizotengwa kwa ajili ya watu wanaowekwa karantini. Kama kuna wageni wanaingia kutoka nje wanapelekwa kwenye hoteli tupeleke na Jeshi la Polisi na vyombvo vingine vya ulinzi tusiachie wale walinzi wa hoteli.

Mheshimiwa Spika,ziko taarifa kwamba wamekuwa hawakai siku zote wanaondoka. Kama hizi taarifa ni za kweli basi kuna haja ya kuchukua hatua zaidi na hatua zenyewe ni kuzilinda zile hoteli. Ukiangalia wenzetu wa Uganda, Rwanda majeshi yao ndiyo yanalinda zile hoteli kwa sababu hili jambo ni la kiusalama na sisi tunapaswa kuzilinda hizi hoteli ambazo hawa watu wanaotoka nje wanawekwa pale karantini, tusiwaachie tu wale walinzi binafsi za hoteli zile. Kwa hiyo, mimi ushauri wangu ni huo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia liko jambo lilizungumzwa hapa; suala la Corona hata sisi kwenye dini ya Kiislamu, mimi ni Muislam limezungumzwa namna gani ya kuchukua hatua yanapokuja magonjwa ya kuambukiza. Iko hadithi sahihi kabisa ya Mtume Muhammad (S.A.W)kwamba unapowafikieni ugonjwa wa tauni basi msiruhusu wageni waingie. Tumezuiwa pia kwa mujibu wa hadithi hii kwamba

tusiruhusu wageni waingie kwenye vijiji vyetu au kwenye maeneo yetu unapokuja ugonjwa wa tauni.

Mheshimiwa Spika,nadhani ugonjwa huu una viashiria vya kufanana na ugonjwa wa tauni. Ikibidi kabisa, inapobidi kabisa, ushauri ni kwamba bora tubaki wenyewe ili tuchukue hatua madhubuti za kudhibiti kuenea ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, huo ulikuwa ushauri wa namna gani tunaweza tukaenda katika kukabiliana na ugonjwa huu wa *corona.*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni maafa ya mafuriko. Mkoa wetu wa Lindi umekumbwa na kadhia hii ya mafuriko na mimi kwenye eneo langu la Jimbo la Mchinga limekumbwa sana, Jimbo la Mheshimiwa Waziri Mkuu limekumbwa na kadhia hii na Majimbo mengine ya wenzangu. Kwa bahati mbaya maji yote yanayotoka Jimboni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu yanaishia kwenye Jimbo langu kwa sababu mwenzangu yuko Mgharibi, mimi niko Mashariki, yale maji yale yote ya mito ile mingi iliyokuwa kule Jimboni Ruangwa basi yanaingiza maji yake pale kwangu, kwa hiyo, hali ya barabara ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika,kwa bahati mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Utawala na TAMISEMI, nafahamu kilichopo kwenye *TARURA*, pesa ya *TARURA* ni ndogo kabisa. Kwa adha iliyotokea mwaka huu kuna haja Bunge lifanye maamuzi ya kuiongezea *TARURA* fedha. Kile kiasi kilichowekwa pale ambacho nakijua ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,kwa mfano, barabara zilizopo katika Jimbo la Mchinga pekee ambazo zimeharibika *completely* hazipitiki kabisa, kwa mujibu wa taarifa za *TARURA* zinahitaji shilingi bilioni 5,892,000,000 ili ziweze kufunguliwa. Kwenye kikao cha *RCC* tulichokifanya wiki tatu zilizopita pale Lindi, Mkoa wa Lindi pekee tunahitaji fedha ya dharura ipelekwe *TARURA* zaidi ya shilingi bilioni 62, ndiyo barabara ziweze kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, hivi tunapoongea, barabara za Jimboni kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nyingi zimefungwa.

Barabara ya kutoka Jimboni kwangu pale Milola - Ruangwa imejifunga kwa sabbau ya mafuriko; barabara ya kutoka Kilwa - Kilanjelanje - Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu imejifunga na barabara nyingine nyingi. Kwa hiyo, Mkoa peke yake tunahitaji zaidi ya shilingi bilioni 60 tuweze kufungua barabara hizi.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu Wizara zote, suala la fedha kwenye *TARURA* mwaka huu tuliangalie kwa sababu tatizo la mafuriko ni nchi nzima sasa hivi, watani zangu Wandengereko pale Rufiji wana malalamiko makubwa na hata juzi nilisema hapa hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, naomba suala la mafuriko na bajeti ya *TARURA* mwaka huu ikiwezekana tuongeze ile *parcentage* kutoka silimia 30 kwa 70 angalau tufike 40 kwa 60 lakini ile asilimia 30 haitaweza kabisa kushughulikia matatizo haya. Tutamlaumu Waziri Mheshimiwa Jafo, kila Mbunge hapa atasimama hapa atasema lakini kiasi cha pesa ni kidogo hakiwezi kutosheleza mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni uwezeshaji wa Vituo vya Utafiti vya Kilimo. Kumekuwa na magonjwa mbalimbali yanajitokeza katika mazao ya wakulima. Nitazungumzia ufuta ambapo kwa sasa ni kama zao kubwa la biashara kwa Mkoa wa Lindi. Sisi tunafahamika, Tanzania sasa ni karibu nchi ya tatu kwa kuzalisha ufuta mwingi duniani na mwingi unatoka Mkoa wa Lindi. Mwaka huu ufuta unapambana na magonjwa mbalimbali. Kila Kijiji ukipiga simu ufuta mara unanyauka, unafanya nini; ukizungumza na watu wa Naliendele shida ni bajeti. Kwa hiyo, naendelea kusisitiza Wizara ya Kilimo lazima itenge fedha za kutosha kupeleka kwenye Vituo vya Utafiti vya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,sambamba na ufuta, nilizungumza mwaka uliopita suala la minazi kwamba kwenye maeneo mengi inakauka. Kila siku natoa kilio hiki, natolea mfano Kisiju kulikuwa na minazi mingi imekufa, pale Lindi maeneo ya Ng'apa, Milola, Mchinga, Nangalu na maeneo mengine ambayo yalikuwa na minazi mingi sana sasa hivi kumetokea ugonjwa wa kunyauka minazi. Nazi ni chanzo cha mafuta

na ni kiungo kizuri, hasa sisi watu wa Pwani kupika wali bila nazi haujakamilika. Kwa hiyo, naomba sana Serikali walichukulie jambo hili *very seriously,* nazi zinaingiza kipato kwenye nchi kwa sababu zinaleta biashara kwenye Halmashauri zetu. Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kwa kiwango kikubwa sana inategemea kipato chake kutokana na kodi inayotokana na nazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo suala la korosho. Mwaka juzi Serikali iliamua kuingilia kati ununuzi wa zao la korosho. Napozungumza mpaka sasa kuna fedha shilingi bilioni 32 za msimu wa mwaka juzi wakulima wa korosho hawajalipwa.

Mheshimiwa Spika,nashukuru jana nimepata taarifa kutoka Lindi kwamba kuna fedha shilingi bilioni 10 zimepelekwa kwa ajili ya kupunguza deni lile. Naomba fedha za wakulima za msimu wa mwaka 2018/2019 zipelekwe kwa wakati ili wakulima wale waweze kulipwa madeni yao. *Imagine*, fedha za mwaka 2018 mpaka leo hawajalipwa na hawa ni wakulima masikini kabisa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Biashara ananisikiliza lakini pia Wizara ya Fedha, kwa sababu watu wa Wizara ya Kilimo ukiwafuata wanasema tatizo bado hatujapewa fedha kutoka Wizara ya Fedha. Shilingi bilioni 32 wakulima wa korosho msimu wa 2018/2019, naomba walipwe fedha hizi. Nimepata taarifa ambazo zina ahueni kwamba mmepeleka shilingi bilioni 10 malizieni shilingi bilioni 22 zilizobaki ili wakulima hawa waweze kupata fedha yao stahiki.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine na nadhani litakuwa la mwisho, niishukuru Serikali lakini pia nishukuru uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa kuhamisha eneo la Jimbo la Mchinga kututoa kwenye iliyokuwa Halmashauri ya Lindi Vijijini na kutupeleka Manispaa. Kuna watu walibeza wakati naijenga hoja hii, nilijenga hoja mara nyingi sana kwamba tuna haja ya sisi kuondokana na wenzetu wa Jimbo la Mtama tubaki kwenye eneo letu la Jimbo la Mchinga ama tupelekwe

Manispaa kwa sababu ndiyo tupo karibu nao, jambo hili watu walifikiria haliwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,nashukuru mwezi wa Oktoba, Mheshimiwa Rais alifanya maamuzi ya kulitoa Jimbo zima la Mchinga kulihamisha kutoka Lindi Vijijini na kutupeleka Manispaa ya Lindi. Tunashukuru sana, sana, sana na hiki kilikuwa ni kilio chetu na kwa nini tunalia? Mheshimiwa Rais aliongelea vizuri siku ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wewe ni Mbunge wa siku nyingi humu unafahamu siku za nyuma namna Wabunge wa Majimbo hayo ya Mchinga na Mtama walivyokuwa wanalumbana. Kwa hiyo, mgogoro ule ulituambukiza hata sisi tuliopo sasa, wakatunyang'anya na Hospitali ya Wilaya akina Mheshimiwa Nape hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa uamuzi wa Mheshimiwa Rais kutupeleka Lindi Mjini Manispaa tunauunga mkono. Kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mchinga tunamshukuru na tunampongeza kwa uamuzi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bobali, hiyo uliyomalizia hata sijaielewa vizuri kufurahia kwenda Manispaa lakini Jimbo si linabaki palepale?

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Jimbo liko palepale.

**SPIKA:** Ahaa, hapo sawa, maana Jimbo letu hilo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Anatropia nilikutaja atafuatiwa na Mheshimiwa Kiteto Koshuma halafu ndiyo Frank Mwakajoka.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nami nisiwe mbali na wasemaji wengi kuongelea juu ya janga la *Corona.* Kusema ukweli sisi

kama Serikali Kivuli hatujaona *initiative* za kutosha, siwezi kusema hakuna ambacho kinafanyika lakini *initiative* zilizopo bado zinatutia mashaka iwapo changamoto itakuwa kubwa, kama nchi za wenzetu, je, sisi tutasalimika? Kama Italia, Hispania wanalia na China wameumia sisi tutasalimika?

Mheshimiwa Spika, tunaamini bado kuna njia ambazo zinapaswa kuwa za nguvu zaidi. Siyo kwamba watu wapigwe, walazimishwe kuingizwa ndani, walazimishwe kufungwa lakini bado kuna *mechanism* ambapo Serikali inaweza ikasaidia kama ambavyo wanafanya Rwanda. Unaweza ukasema Rwanda ni mfano mdogo mzuri wa *initiative* zinazofanyika.

Mheshimiwa Spika,naamini bado tuna nafasi ya kufanya kitu kabla janga hili halijawa kubwa *unless* tuendelee kuamini kwamba hamna kitakachotokea. Lazima twende na *global trend*, kama tunaona *challenge* ni kubwa sisi tunajiandaaje? Waswahili wanasema ni afadhali ujue Mungu yupo uishi vizuri kuliko uishi vibaya halafu ugundue yupo utakosa pa kukimbilia. Huo ndiyo wito wangu kwenu.

**SPIKA:** Huko Rwanda kuna nini kizuri kinafanyika?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Rwanda unaweza ukaona wametagaza *total lock down,* lakini kama haitoshi, wamewagawia vyakula watu ambao wana changamoto ya maisha.

**SPIKA:** Haya, basi nimekuelewa. Endelea na mchango wako, kumbe ni *total lock down.*

**MBUNGE FULANI:** Endelea.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ndiyo, nimekusikia Mheshimiwa Goodluck.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji anayezungumza kuwa Serikali hatua ambazo imechukua, siyo zote ambazo imezitangaza. Nataka nimpe mfano mmoja tu; agizo la Waziri Mkuu kwa Wakuu wa Mikoa wote, likaenda mpaka kwa Wakuu wa Wilaya, kila Wilaya katika Hospitali ya Wilaya imetengeneza *withholding rooms* na *treatment unit.* Hiyo *treatment unit* imegawanyika katika sehemu mbili; *high risks* na *low risk.*

Mheshimiwa Spika, vile vile kila wilaya ambayo iko mpakani, kuna sehemu maalum wametenga kwa wale wageni wanaoingia. Kwa mfano, Tunduma kuna wageni 84 mpaka sasa hivi wameifadhiwa mpaka zipite siku 14 ndiyo wataingia. Kwa hiyo, vitu vingine vizito siyo vya kuzungumzwa hadharani. Ahsante sana.

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, naendelea. Kwa sababu kama mambo hayazungumzwi hadharani, yatajulikanaje sasa? Si lazima yazungumzwe ili watu waweze kuchukua hatua! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee changamoto ya zao la kahawa. Zao la kahawa linachangia katika pato la Taifa zaidi ya asilimia tano, lakini ni moja kati ya mazao ambayo siyo tu yamesahaulika bali kuna mkakati unaonekana kama linataka kusukumwa pembeni. Changamoto ambazo wakulima wanapitia na hususan wakulima wa Mkoa wa Kagera, *specifically* Wilaya ya Kyerwa na Karagwe, yale ndiyo maeneo ambayo tunazalisha kahawa sana; na inaajiri karibia kila kaya. *Almost* kila kaya ni wakulima wa kahawa. Kipato chao kila siku ni kahawa.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambayo imewakuta wakulima ni kwamba soko limekuwa gumu. Wanalima bila kujua wanauza wapi? Wanalima bila Serikali kuonyesha *initiative* ni kiasi itaweza kusaidia ili waweze kuzalisha zaidi?

Mheshimiwa Spika, nimeipitia *Report* ya *Agricultural Non-State Actors Forum,* inaonyesha ni kiwango gani licha ya *research* kufanyika na kuainisha changamoto za kimfumo zinazowakuta wakulima wa zao la kahawa, bado changamoto hizo hazijatatuliwa ikiwa ni pamoja na Bodi ya Kahawa kuiwezesha kuwa msimamizi wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, pia Shirika la *TaCRI* ambalo linajihusisha na kufanya utafiti wa magonjwa yanayosumbua kahawa, kuzalisha kahawa mpya na mbinu za uzalishaji bora, limekuwa halipewi fedha au fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya hiyo kazi. Utaona kwamba ni juhudi za makusudi za kuhakikisha zao la kahawa mbali na kukosa soko, linazidi kudidimia.

Mheshimiwa Spika, pili, changamoto kubwa ambayo wananchi wamezidi kuiona, sijui ni kuzuia au nini kimefanyika mpaka Vyama vya Ushirika ndiyo vinaonekana kuwa mnunuzi pekee wa zao la kahawa. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameenda Wilaya ya Karagwe na Kyerwa mara kadhaa, lakini sasa ametusaidiaje kutatua changamoto ambayo tunaona chama cha msingi hakijawezesha wananchi kuuza mazao yao kwa thamani ambayo waliitarajia? Msimu uliopita walikuwa wananunua kilo moja kwa shilingi 1,100/=. Msimu huu ambao ni msimu mdogo, tunaita Ndagasa, walipaswa kununua kwa shilingi 700/= lakini vile vile hawajanunua.

Mheshimiwa Spika, watu wana mazao, hawawezi kuuza kokote, mashirika au makampuni binafsi hayawezi kununua, watu wako *stranded,* watu wanapaswa kupata fedha ya kupeleka watoto shule, wanapaswa kujiendeleza katika maisha yao, hayo mambo yote yamekuwa ni magumu. Changamoto ni kwamba watu wamezidi kuwa masikini na kuna msemo unasema, watu wa huku wanajikuta

wanabaki kuwa masikini, masikini na wa mwisho katika *trend* ya *ranks* za maendeleo yamekuwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sasa tunaweza kuona ni Serikali inafanya *deliberatively* kuhakikisha tunazidi kuwa masikini licha ya kwamba tuna nyenzo ya kujikwamua kama wakazi au kama wananchi wa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, nimepitia bajeti ya Chama cha Ushirika kwa *estimates* zao za mwaka 2020/2021...

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, umesema Serikali inafanya makusudi!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushindwa kubadilisha mifumo ambayo inaendelea kukandamiza wakulima wa kahawa ni sawasawa na kufanya makusudi ili wananchi wazidi kuwa masikini. Hakuna namna nyingine nitakayoitumia kwa sababu kama tutaondoa vikwazo, kama tutajaribu ku-*encourage*...

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Unapewa taarifa Mheshimiwa Anatropia. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza zao a kahawa, ni kweli kabisa wakulima wa Kagera wanalima vizuri sana na wanajitahidi sana kulima, Serikali kwa kuona changamoto za masoko ilichukua hatua za dhati kabisa za kuimarisha Vyama vya Ushirika ikiwa ni pamoja na kuwapatia fedha Vyama vya Ushirika ili viweze kununua kwa wakulima na kuhakikisha wanapata bei nzuri. Hii imefanyika vizuri sana na vyama vingi vimefanikiwa katika hilo eneo.

Mheshimiwa Spika, pia tuliweza kuhakikisha kwamba tunazuia wale walanguzi ambao walikuwa wanachukua

kahawa na kwenda kuipeleka nchi jirani. Zaidi ya hapo, tumeiwezesha Bodi ya Kahawa kuisimamia vizuri sana na ndiyo maana uzalishaji umeongezeka na bei imeimarika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya anayoyasema kwamba Bodi ya Kahawa imesahaulika, Vyama vya Ushirika havijasaidiwa, havina uwezo, labda atuambie ni chama gani ambacho hakina uwezo? Kwa sababu kwa takwimu za Serikali ni kwamba tumeviwezesha vya kutosha na kuna mchango mzuri sana ambao unaendelea.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kumpa hiyo taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia unapokea taarifa hiyo?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu ya ripoti niliyoisoma ambayo ukitaka nitakupatia na iko *online* inasema...

**SPIKA:** Ripoti hiyo kutoka wapi yaani? Ili tuweze kufuatilia wote maana hii ni ya Serikali. Hiyo yako ni ya kutoka wapi?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ni *ANSAF* ambao ni wadau.

**SPIKA:** *ANSAF* ndio…

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wanaita *Agriculture Non Sector Actors Forum.*

**SPIKA:** Sasa *forums* hizo, yaani wewe una...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, wamefanya utafiti, wana *data...*

**SPIKA:** Sasa upande huu umepewa taarifa halisi za Kiserikali.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nami ndiyo nataka niseme, utafiti walioufanya umeonyesha kwanza vyama vyenyewe vimekuwa havina wataalam hata wa kukidhi mahitaji ya vyama husika. Hiyo nitasema. Nilitaka niunganishe na taarifa ambayo niliyosoma *estimate* ya Chama cha Ushirika.

**SPIKA:** Huo utafiti umekuwa *vetted* na *TBS*? *Bureau of Statistics*?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, imekuwa *published*. Kwa hiyo, kama iko *published, assumption* ni kwamba imekuwa *satisfied. (Makofi)*

**SPIKA:** Haya bwana, kama hao *ANSAF* unawaamini, endelea tu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya kwanza eeh!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Ni kengele ya kwanza.

**SPIKA:** Ni ya kwanza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimjibu, wameonyesha changamoto iliyopo kwenye *management* halisi ya Vyama vya Ushirika, lakini hiyo imeonekana hata kwenye bajeti husika. Bajeti ya Chama cha Ushirika ambayo inaonekana *estimate* zaidi ya shilingi bilioni 1.5 itaenda kwenye *Managerial Activities* kulipa fidia, kuhamisha kutoka eneo moja kwenda lingine na hii naweza nikakupatia, ambayo inaonekana fedha nyingi inatumika kwenye *Managerial Activities* na siyo kulipa wale wakulima wenyewe.

Mheshimiwa Spika, hii inaonyesha kwamba *activities* za ku-*run* au *activities* za kuandaa zao la kahawa, *cost* moja ya kilo itakuwa ni zaidi ya shilingi 1,700/= wakati wakulima

wanaweza kuuza kwa shilingi 1,300/=. *You can imagine* kwamba anayelima kwa zaidi ya miaka mitano...

**SPIKA:** Hiyo ni bajeti ya Chama cha Ushirika cha Kagera ambako na wewe unatoka.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Ndiyo.

**SPIKA:** Nanyi ndio wanachama wa hicho Chama cha Ushirika.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Ndiyo, ndiyo, ndiyo.

**SPIKA:** Sasa unamlaumu nini Waziri wa Kilimo katika hilo kwa mfano?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika ninaiambia Serikali na huo ndiyo wito ninaoenda kuutoa kabla sijamaliza. Serikali ni lazima ifanye *study* kuona ni namna gani inaweza ikasaidia kwenye kuimarisha zao la kahawa badala ya mbinu tulizonazo leo za kutumia Vyama vya Ushirika ambavyo vimekuwa havina uwezo na uzoefu. Hiyo ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya pili, tunaposubiri madalali, *middle men* watoke Ulaya au wapatikane hapa katikati waende Ulaya watutafutie soko ili sisi tuuze, ni lazima Serikali iangalie, tunawezaje ku-*penetrate* kwenye soko husuka ili tuweze kuuza; Mheshimiwa Rais anasema *win win situation.* Kwa nini *win win situation* tunazitaka kwenye madini; tunazitaka kwenye dhahabu; hatuzitaki kwenye kahawa? Sasa ni lazima tutengeneze mkakati hata wakulima wetu wafaidike kama ambavyo tunataka wafaidike kwenye mazao mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wito wangu mwingine, kwa nini minada ifanyike kwenye Mikoa ya Kilimanjaro? Hii nairudia kwa mara nyingine. Hii ikifanyika kwenye mkoa husika kama Kagera, itasaidia kuondoa gharama za usafirishaji zinazohusika kwa ajili ya kufuata mnada wa Kilimanjaro.

**MHE: INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Unapewa taarifa na Mchungaji.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa mchangiaji anayechangia kwamba kuna jambo ambalo amesema kuwa Vyama vya Ushirika ndiyo wanunuzi wa kahawa. Vyama vya Ushirika siyo wanunuzi wa kahawa, ni wasimamizi; na suala la mnada limekuwa likifanyika Mkoa wa Kagera. Mwaka 2019 limefanyika na wanunuzi wote waliwatangazia wenye bei nzuri wakanunue. Pamoja na hizo changamoto zilizopo kwenye kahawa, lakini minada imefanyika Kagera, lakini Vyama vya Ushirika siyo wanunuzi, ni wasimamizi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nadhani anaji-*contradict.*

**SPIKA:** Anakwambia Jimbo limejaa. *(Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nami nataka kukwambia hii ni *pressure* ya Jimbo na nimelikalia hasa! *(Makofi/Kicheko)*

Hiyo ni *pressure* ya Jimbo na ninalikalia hasa!

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Tukutane kazini. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Malizia, malizia, bado dakika moja.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, bado kama Serikali mna nafasi ya kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Kagera. Msiwaletee fedha, msiwaletee dhahabu, tusaidieni kwenye zao letu la

kahawa, tupatieni soko, lakini ruhusuni biashara huria. Mbona maeneo mengine biashara huria inafanyika? Bodi ya Kahawa itabaki kama refa iangalie nani anacheza rafu; na lengo kubwa ni kuwasaidia wakulima wetu waweze kufaidika kwa mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma nilishakutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukubali kunipatia tena nafasi hii ili niweze kutoa michango yangu katika Bunge lako Tukufu. Kipekee kabisa ninaomba nikushukuru wewe binafsi kwa namna ambavyo unakuwa ukiwasaidia Waheshimiwa Wabunge na kuwaonesha moyo wa ubinadamu pale wanapokuwa wanapatwa na matatizo mbalimbali hususani ya msiba.

Mheshimiwa Spika, katika hili ninakushukuru wewe, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote ambao mliungana pamoja nami kipindi chote ambacho nilimuuguza baba yangu mpendwa na hatimaye Mwenyezi Mungu akampenda zaidi, lakini mlikuwa pamoja nami kwa kunifariji, mmenifariji sana na Mungu awabariki sana, ninawaombea kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo za utangulizi, ninaomba sasa nirejee katika kuchangia kuhusiana na hotuba ya bajeti ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yameongelewa masuala mengi; imegusa masuala ya afya, maji, majanga mbalimbali na imegusa maeneo mbalimbali ikionesha maendeleo makubwa ambayo yamefanywa na Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi kupitia Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imeendelea kuzifanya katika kuhakikisha kwamba Tanzania inasonga mbele. Tumeyaona maendeleo, tumeona mabadiliko mbalimbali katika sekta mbalimbali na leo ninaomba kuongelea sana katika Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Afya Serikali imejitahidi kadri ilivyoweza kwa kuhakikisha kwamba inakarabati Vituo vya Afya, Zahanati, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa lakini pia imeongeza ujenzi wa Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya katika maeneo mbalimbali na hata Hospitali za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kuna changamoto tu chache ambazo napenda kutoa ushauri wangu ili uweze kufanyiwa kazi. Kujenga Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na Vituo vya Afya ni jambo moja, lakini kuweka wataalam ambao wataenda kuhudumia katika Vituo hivyo vya Afya pamoja na Hospitali ni jambo lingine. Naishauri Serikali sasa, nguvu ambayo iliitumia na kuiwekeza katika ujenzi wa Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya na hata Hospitali za Mikoa, nguvu hiyo hiyo ambayo Serikali ilitumia, basi iitumie kuwekeza katika wataalam.

Mheshimiwa Spika, kujenga unaweza kutumia hata mwezi mmoja unapokuwa rasilimali fedha, lakini kuwaandaa wataalam inaweza ikakuchukuwa takribani miaka mitano ili kuwapata wataalam kuweza kutoa huduma za kiafya.

Mheshimiwa Spika, katika huduma za kiafya, tuna-*deal* na afya za wanadamu. Kwa maana hiyo, ninaishauri sana Serikali sasa iwekeze nguvu katika kuhakikisha kwamba inaandaa wataalam ili waweze kutoa huduma bora za kiafya na siyo bora huduma.

Mheshimiwa Spika, pia waliopo, wale wataalamu tulionao, basi naiomba Serikali itoe kibali ili iweze kutoa ajira katika Sekta hii ya Afya kwa sababu ninaamini kabisa yako maeneo mbalimbali na kwa sababu hapa tunajadili bajeti ya Waziri Mkuu ambayo inagusa maeneo mbalimbali katika

nchi ya Tanzania, sitapenda tu nijikite katika mkoa wangu wa mwanza ambao nao pia unahitaji wataalam katika sehemu mbalimbali. Kwa hiyo, ninaomba Serikali iwekeze katika kuandaa wataalam ili waweze kuzihudumia sehemu hizo ambazo nimezitaja.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta hiyo hiyo ya Afya kuna suala la hospitali hizi za kikanda, nilikuwa naishauri Serikali iwekeze nguvu kuhakikisha kwamba tunapata hospitali zenye hadhi ya kikanda sawa na Hospitali ya Muhimbili. Tunayo Hospitali ya *KCMC* ambayo iko Moshi, nashauri kwamba Serikali iweke nguvu ili hospitali hii na yenyewe iweze kuwa na hadhi zawa na Muhimbili ili kuondoa msongamano katika Hospitali ile ya Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna Hospitali ya Kanda ya Bungando; na yenyewe pia naomba ifanyiwe hivyo hivyo. Pia kuna Hospitali ya Mbeya, Hospitali ya *Dodoma General;* naomba hospitali hizi ambazo nimezitaja, Serikali iwekeze katika hospitali hizi ili na zenyewe ziweze kutoa huduma sawa sawa na huduma zinazotolewa Muhimbili.

Mheshimiwa Spika, Madaktari bingwa wanaishia kuwepo tu Muhimbili. Ukiwapeleka katika hizo Hospitali ambazo nimekwambia, wanaona kwamba utaalamu wao hauwezi kutumika kwa sababu hospitali zile hazina hadhi sawa na Hospitali ya Muhimbili. Kwa hiyo, ninaomba sana Serikali ijikite katika eneo hilo ili basi tuweze kuboresha huduma za afya katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika Vituo vyetu vya Afya na Zahanati zetu tunakosa wataalam wa meno na wataalam wa mionzi. Ninaomba pia Serikali iwekeze katika wataalam hao pamoja na wataalam wengine, lakini ijikite basi katika wataalam wa mionzi na wataalam wa meno ili kuendelea kuboresha huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa naongelea suala la afya na vile vile katika hotuba ya Waziri Mkuu ameongelea suala la janga hili la *Corona,* nami naomba niungane na

Waheshimiwa Wabunge kuendelea kuwasihi Watanzania kwamba tuweze kuzingatia yale maelekezo ambayo tunapewa na Wizara yetu ya Afya ili tusiweze kueneza ugonjwa huu wa *Corona.*

Mheshimia Spika, naomba niishauri Serikali na ninaamini kwa ushauri huu wataweza kunisikiliza na kuufanyia kazi. Pamoja na kwamba tumeendelea kutoa maelekezo mbalimbali, lakini ninaangalia sehemu ambazo kuna misongamano mikubwa ya watu, pale kukitokea mlipuko, hali itakuwa ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano kwenye *public transport,* ukiangalia pale Dar es Salaam katika haya mabasi ya mwendo kasi, msongamano ambao unakuwepo katika yale mabasi ni mkubwa na ni hatari sana. Ninashauri basi Serikali iangalie namna bora aidha kusitisha hizi *public transport* hasa ambazo zina msongamano mkubwa na kuangalia njia mbadala ambayo Watanzania wataitumia katika kusafiri kila siku kwenda kufanya majukumu yao mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine yenye msongamano mkubwa ni sehemu ya feri pale Dar es Salaam napo pia kuna msongamano mkubwa. Sehemu kama vile la soko la Kariakoo naomba sana Serikali yangu sikivu iangalie maeneo hayo na iweze kutoa tamko ambalo litaweza likawasaidia watanzania na kusaidia kupunguza *spreading* hii ya ugonjwa huu wa Corona na hata kuzuia vifo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hiyo naomba sasa niongelee suala la maji,suala la maji limekuwa likipigiwa kelele sana na Wabunge wengi hapa ndani, wakati wa kipindi cha maswali na majibu utaona wakati wa maswali ya nyongeza Wabunge wote husimama kuweza kuulizia masuala ya maji. Lakini pamoja na kwamba Serikali imejitahidi kuchukua mawazo ya Wabunge na kuanzisha wakala wa huduma za maji vijijini yaani RUASA na pia uko mfuko wa maji ambao mfuko huu chanzo chake cha fedha kinatokana na shilingi 50 ya kila lita moja ya petroli.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiiomba sana Serikali kwamba iongeze kiwango hiki cha tozo ya shilingi 50 hadi shilingi 100 nia ni njema sana. Nitaongea kama ifuatavyo nia na madhumuni tuweze kufikia walau mfuko huu kuwa na shilingi bilioni 300 zikipatikana shilingi bilioni 300 ina maana kila jimbo lina uwezo wa kupata shilingi bilioni 10. Kigugumizi kinatoka wapi, ninaiomba Serikali yangu kwa kuwa ni Serikali sikivu basi iliangalie na hili ili tuweze kumtua mwanamke ndoo kichwani lazima tuongee kwa vitendo na kwa sababu Waheshimiwa Wabunge tumeendelea kutoa ushauri huu wa kuongeza tozo hii ya shilingi 50 hadi 100 ili lengo letu la kufikia shilingi bilioni 300 na hatimaye kila jimbo kupata bilioni 10.Ninaamini kabisa hakuna mtu ambaye atasimama katika Bunge kulalamikia suala la maji, ninaamini kila jimbo litaweza kufanikiwa kuangalia kwamba masuala ya maji yametatuliwa.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kiteto.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na naamini kabisa kwamba ushauri ambao nimeutoa Serikali yangu sikivu itaweza kuuchukua nashukuru na naunga mkono hoja ahsante sana.*(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kiteto Koshuma tunakushukuru sana naomba niendelee kutoa ushauri kwamba tupunguze sana matumizi ya vikaratasi kama tulivyozoea kuvizungusha humu ndani karibu *page boys na page girls* tutawaaga. Sasa hivi ni vizuri zaidi unapokuwa humu ndani basi ukaweka kwenye sms anayetuma meseji akakutumia kwenye sms ukaipata ukamjibu nakadhalika. Kwa hiyo, ni vizuri kuwa na namba za Wabunge na Waheshimiwa basi tukawasiliana kwa utaratibu huu ili kupunguza kidogo matumizi ya vikaratasi kwa sababu zilezile ambazo ziko wazi kabisa. Nasema hili ni pamoja na huko Msekwa na maeneo mengine pengine.

Waheshimiwa Wabunge, pia natoa ushauri kwa Wabunge ambao wanakuja Bungeni lakini hawaingii kwenye

ukumbi huu mkubwa baadhi yao wanakuja wamevaa mavazi ambayo sii ya Kibunge na wengine wako na makobazi, wengine wako na majinsi nakadhalika tunawaona. Kwa hiyo, niwakumbushe tu kwamba kanuni za Bunge zina-*apply* hiki ni kipindi cha wakati wa Bunge na niwatake basi maofisa wangu wote magetini mtu ambaye hakuvaa katika taratibu za Kibunge wakati Bunge linapoendelea wakati wa siku za Bunge basi hatua zinazotakiwa ziweze kuchukuliwa kwa maana ya kumzuia asiyekuwa na mavazi rasmi Bungeni. Mheshimiwa Richard Mbogo halafu ndio Mheshimiwa Frank Mwakajoka, Mheshimiwa Richard kwanza Mheshimiwa Frank atachafua hali ya hewa ngoja nimsogeze kidogo.

**MHE. RICHARD S. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi, kwanza nianze kumshukuru Mungu na niombe tu watanzania tuendelee kumwomba aendelee kutuepusha na hili janga ambalo linasumbua dunia la *Covid 19.*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nipongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri ambayo anaifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye kazi ya kuendeleza nchi yetu na watanzania kiujumla. Pia naomba niwapongeze mawaziri wote watatu Waziri mwenyewe Mheshimiwa Jenista na Manaibu Mheshimiwa Anthony na dada yangu Ikupa na watendaji wote makatibu wakuu na watendaji wote chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni vyema tuseme kwa hii miaka mitano Waziri Mkuu kwenye hotuba yake ameweza kueleza vyema kila sekta na kila wizara kwa maana nyingine ni jinsi gani ambavyo tumeweza kufanya kazi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni kufatisha mpango wa maendeleo pamoja na ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inaelekeza nini kifanyike kwa wananchi. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa namna ambavyo wamefanya kazi kubwa sana ndani ya miaka mitano na takwimu zinajionyesha kwa vitu ambavyo vimefanyika vingi na vya

thamani kubwa tofauti na miaka iliyopita ikiwa ni mabadiliko yaliyotokana na uongozi ndani ya Chama Cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hilo naomba nianze na suala la majanga ambayo yametokea kwenye nchi hii. Mwaka huu 2020 na tangu mwaka jana 2019 Tanzania tumebarikiwa kuwa na mvua nyingi sana ambazo kwa miaka hii mitano kwa kweli haijapata kutokea. Kwa hiyo, mafuriko ambayo yametokea Rufiji kwa Mheshimiwa Mchengerwa na pia hata sisi Mkoa wa Katavi kuna baadhi ya maeneo yalipata mafuriko lakini siyo makubwa kama haya na yamepelekea baadhi ya nyumba za wananchi kuweza kubomoka.

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Waziri Mkuu natumainia taarifa imefika ofisi kwako sasa hivi usafiri wa njia ya reli haupo kwenye Wilaya Mpanda, au Mkoa wa Katavi kutokana na tuta la Mto Ugala takribani mita 120 kubomoka baada ya kuwa mto umejaa sana na mvua zilivyo nyingi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hiyo wito wa wananchi wa Mkoa wa Katavi wanaomba kwenye fedha za dharura na vyanzo vingine chini ya Wizara kwamba punde tu baada ya kuwa mvua zimesimama basi tuta liimarishwe kwa kuwa midomo mingi ambayo itaweza kupitisha maji na madhara haya yasitokee tena kwa masika zinazofata. Kwa hiyo, hiki ni kilio kikubwa sana kwa wananchi wa Katavi tunakumbuka miaka ya nyuma tumewahi kukulilia sana kuhusu njia hii ya reli ni msaada mkubwa sana kwa Mkoa wetu wa Katavi. Tunalima pamba, tunalima mazao ya chakula, Mkoa wa Katavi ni moja ya mikoa ile minne inayotoa sana chakula na kulisha nchi hii pia tunalima tumbaku sasa ubebaji wa haya mazao unahitaji sana hii njia ya reli na ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu na uchumi wa wananchi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kimsingi sasa hivi Mheshimiwa Waziri Mkuu njia zinazotumika kutoka nje ya Mkoa wa Katavi ni kupitia Sumbawanga kuja Mbeya na kupitia Uvinza kuja Kigoma kuja Tabora. Ni hizo tu kwa hiyo,

njia ya reli haipo nah ii njia ya kuja Tabora Sikonge na kwenye pale kwenye daraja la mto Ukoga na lenyewe limefungwa muda mrefu kutokana na kujaa sana na kuhatarisha maisha ya wananchi. Kwa hiyo, pia tunashukuru Mheshimiwa Rais mwaka jana alivyohimiza *Air* Tanzania na inafanya mara tatu kwa wiki na yenyewe pia ni njia ya usafiri inayotumika. Lakini hizi njia kuu mbili ni muhimu sana kwa Mkoa wa Katavi kwa hiyo tunaomba sana kwenye fedha za dharura mtuangalie tuweze kutengeneza hili tuta kwenye mto Ugana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la uwezeshaji. Kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri Mkuu umezungumza vizuri na hatua ambazo zimeweza kuchukuliwa na lakini pia kupitia halmashauri zetu na majiji na manispaa wametekeleza vyema kupeleka fedha zile zinazotengwa kutoka kwenye mapato ya hizi halmashauri mapato ya ndani asilimia 10 ambayo inaenda kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nikianza na vijana tunajua rika la vijana mwisho ni miaka 35 lakini changamoto ambayo tumekutana nayo ni kwamba kuna watu wanazidi umri huo kwa hiyo wanakuwa hawako kwenye sifa za kuunda vikundi na kupata mikopo hii. Sasa tunajua mna vyanzo takribani taasisi 19 ambazo zinafanya uwezeshaji na ukopeshaji katika nchi hii lakini kwenye hili la vyanzo vya halmashauri kwenye asilimia 10 ya mapato ya ndani tuliondoa pia riba ambayo mmeweka sana unafuu. Kwa hiyo, tuombe sasa Serikali tuangalie Mheshimiwa Waziri Mkuu ile mifuko iliyo chini ya Ofisi yako ni namna gani sasa iende ikasaidie kundi la wanaume ambako wanakuwa hawako kwenye kundi la vijana ambao wamezidi miaka 35.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ndio hao ambao wanakwama kwa sasa hivi kuwa na sifa ya kuweza kukopeshwa. Kwa hiyo, kama ule mfuko wa *self* na hii mifuko mingine ambayo ni ya kuwezesha vijana basi tunaomba tuongeze aidha tuongeze rika angalau tuweke kwamba vijana na watu wenye umri wa kati ambao labda wanafika hata miaka 50 hii itasaidia sana na ndio kizazi hichi ambacho

ndio cha uzalishaji ni kinachangia sana kwenye pato la Taifa. Kwa hiyo tunaomba marekebisho ya sera hii au sheria ili tuongeze umri kwa upande wa vijana tuwabebe na watu wanaofkisha mpaka umri wa miaka 50 au la tuwezeshwe kwenye mifuko mingine na iende kukopesha bila riba.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kwenye uwezeshaji hapa hapa kuna halmashauri ambazo zina mapato ambayo yako chini sana ni chini ya bilioni moja. Kwa hiyo, kile kiwango ambacho kinakuwa na uhitaji pia hakitoshi, kwa hiyo, tunahitaji sana hii mifuko pia iendelee.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la vikundi sasa hivi tunaambiwa idadi ya vikundi imeongezwa kutoka watu 5 mpaka 10 sasa imekuwa inaweka mkanganyiko kwa wananchi kwa sababu wingi wao pia ile fedha wanayokopeshwa ni ndogo halafu wanakuwa wako wengi na wengi hawana biashara ya pamoja wanachukua halafu wanagawana. Kwa hiyo, hiki kiwango kilichoongezwa cha watu 10 tunaomba kipunguzwe na angalau pia tuangalie sheria hii kama kuna uwezekano wa kukopeshwa mtu mmoja pia na yenyewe pia iweze kuangaliwa na ambayo itasadia sana. Kwa mfano kwa watu wenye ulemavu kuna wengine wana ulemavu viungo vinatofautiana na aina ya kazi ya kufanya. Kwa hiyo, watu wenye ulemavu iangaliwe kukopeshwa mtu mmoja mmoja kwa sababu wengine kuna kijiji wako wachache na aina ya ulemavu na kufanya biashara kila mmoja inatofautiana.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la uwekezaji, liko chini pia ya ofisi ya Waziri Mkuu lakini naomba turejee kwenye suala la tafiti mbalimbali na kwa nini tulikuwa tuna *SIDO* na kwa nini tulikuwa tuna *TIRDO*. Mpaka sasa hivi *SIDO* na *TIRDO* zimefanya, malengo yake wamefanya kwa asilimia gani kwa nini wamefeli na kama wamefeli tunawakwamua vipi ili waende mbele. Maana tunapozungumzia uwekezaji lazima tuangalie na taasisi ambazo zinaenda kusaidia uwekezaji hususani watu wa ndani na viwanda vikiwepo tunasaidia pia kutumia fedha zetu za kigeni ambazo tunazo kwa ajili ya manunuzi mengi kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la ajira. Tunaona kwenye kilimo tunaajiri watu wengi lakini ile kada ya vijana bado hatujachukulia vyema kwenye upande wa kilimo. Uwezeshaji wa mitaji, uwezeshaji wa elimu na ujuzi na uzoefu bado upo kwa kiwango cha chini kwa hiyo tuombe Serikali kwa mfano *PAMATEC* wana matrekta mengi sana pale na wana mkataba lakini namna gani ya kuyatoa moja ya nyenzo za kuwasaidia watu kwenye kilimo bado linasuasua. Kwa hiyo, tuombe Waziri Mkuu uliingilie hili matrekta yako pale wana mkataba na mzalishaji wa Poland kwa hiyo, hawajatimiza ile kiwango ili sasa kiwanda kiweze kujengwa hapa Tanzania. Kwa hiyo, tunaomba uingilie kati na uweze kusaidia suala hilo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo niligusie ni kuhusiana na Corona kama wenzetu ambavyo wamechangia Wabunge. Tunaomba sasa Serikali kwenye maeneo ya mikusanyiko kwenye vyomboo vya usafiri kabla abiria hawajaingia basi vipulizwe dawa na kikifika kipulizwe dawa pia *stand* zote kwa sababu zina mageti kwa nini maafisa wetu wa afya wasiwepo pale kama wanawapima kama sisi vile Wabunge tunavyoingia hapa ndani na tunapimwa. Ukienda Stand ya Ubungo, stand ya Usamvu zote hizo tuongeze usimamizi wa hali ya juu.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:**Mheshimiwa Spika, nashukuru naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Richard Mbogo sasa Mheshimiwa Frank George Mwakajoka atafatiwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kuwapongeza viongozi wangu wa chama hasa Mwenyekiti wetu wa Chama

cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa jinsi ambavyo anafanya kazi yake vizuri ya kukiongoza chama hiki lakini pia kuhakikisha chama kinasonga mbele na kinafanya vizuri zaidi na kuwa tishio kwa kweli kwenye Chama Cha Mapinduzi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana wananchi wangu wa mji wa Tunduma kwa jinsi ambavyo wanazidi kuniunga mkono, toka walivyoniamini mwaka 2015 mpaka sasa hivi wanaendelea kunihitaji niendelee kuwa Mbunge wao na mimi nasema kwamba nimejiandaa kuendelea kuwaongoza na kuwahakikishia kwamba nawawakilisha vizuri. Kwa hiyo, mambo yanakwenda vizuri Mheshimiwa Spika hakuna matatizo yoyote.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kikubwa tu...

**SPIKA:** Hutarajii kuita waandishi wa habari hivi karibuni?

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, narudi tu wala usiwe na wasiwasi.Kikubwa tu nilichotaka kuzungumza hapa nilikuwa nimefurahi sana kumsikia Mheshimiwa Rais anasema kwamba uchaguzi utakuwa kama ulivyopangwa na sisi kama Upinzani tulikuwa na masikitiko makubwa sana tulivyosikia kwamba kuna fununu Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi wanasema uchaguzi uhairishwe tulikuwa tunajisikia vibaya kwa sababu tumejiandaa vizuri na tumejipanga vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunafikiri uchaguzi huu ni uchaguzi ambao tunaamini kabisa utakuwa huru na haki lakini pia nimepata moyo zaidi baada ya kuona Mheshimiwa Rais amekutana na wabalozi wa nje na kuwaambia kwamba uchaguzi utakuwa huru na haki lakini Waziri wa Mambo ya Nje amekutana na mabalozi wa nje pia amewaambia utakuwa huru na haki. Nimemwona Simbachawene pia juzi amesema uchaguzi utakuwa hiuru na haki ninaamini

uchaguzi huu utakuwa huru na haki watanzania wanahitaji kuchagua kiongozi wanayemtaka na siyo kuchaguliwa kiongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu zipo tafsiri ambazo zimekuwa ni potofu sana sisi tunasema tunahitaji Tume huru ya uchaguzi wako watu wengine wanafikiri tunavyohitaji tume huru ya uchaguzi tunahitaji kushinda uchaguzi. Sisi hata tungekuwa na tume ambayo si huru tutashinda uchaguzi tu lakini ukweli tunahitaji tume huru ya uchaguzi kwa sababu ya amani ya nchi yetu kwa sababu tunajua kabisa kwamba kama kutakuwa na tume huru ya uchaguzi kutakuwa na uwazi na kila mmoja.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, atajua kabisa kwamba kura yake aliyopiga

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, na atakayeshinda ameshinda sawasawa...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**T A A R I F A**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nilindie muda wanachosha tu hawa

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji Wabunge wote humu ndani tumeapa kwa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tume huru imetajwa kwenye katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba patakuwepo na katiba na patakuwepo na Tume ya Uchaguzi ambayo itakuwa huru haitaingiliwa na chombo chochote sasa hiyo tume ambayo

yeye anaisema kwamba anaidai anataka itajwe vipi kwenye katiba ambayo yeye ataiona kwamba hii tume ni huru.

**SPIKA:** Taarifa hiyo unapewa Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, unajua hawa ambao sio CCM halisi hawa wana matatizo makubwa sana wanahitaji uhalali wakati CCM halisi wamekaa wanajua nini nachokizungumza tulia kwanza.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji tume huru nia na madhumuni ni kuhakikisha kwamba tunafanya uchaguzi ulio huru na haki na tunahitaji watanzania waweze kuona kwamba ndani ya chumba cha uchaguzi yale matokeo yanayotangazwa ni matokeo ambayo yako sahihi na wanaamini kwamba yametangazwa na aliyeshinda ameshinda uchaguzi, tunahitaji tume ya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, sisi hatuna wasiwasi na uchaguzi unaokuja tumejiandaa kushinda kwa asilimia 100 kabisa na safari hii tumesema hatutawaacha ni lazima kwa kweli mng'oke na muhakikishe kwamba mnang'oka kwa sababu zilizo sahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina sababu nyingi sana za kuzungumza kwa nini mtang'oka nataka sasa nianze kuchangia mchango wangu kwenye utakelezaji wa bajeti ya mwaka 2019/2020 na uone ni sababu tunasema mtang'oka kwenye uchaguzi unaokuja kwa sababu hamjafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka vipaumbele ambavyo mmeviweka kwenye mpango wa bajeti wa mwaka 2020/2021 mmeweka reli *standard gauge,* mmeweka *Stiegler's Gorge,* mmeweka ununuzi wa ndege na mmeweka bomba la mafuta.

Mheshimiwa Spika, asilimia 75 mpaka asilimia 80 ya watanzania ni wakulima na wafugaji cha kushangaza ni kwamba Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ambayo iliapa

kwamba itakuwa ni Serikali ya wanyonge huwezi kuamini kilimo hawaoni kama ni kipaumbele kabisa. Hawaoni ni kipaumbele kwa sababu wanazungumza kwa maneno lakini vitendo hawawezi kutekeleza.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi, walisema kwamba ndani ya miaka mitano watahakikisha kwamba kilimo kinakua kwa asilimia nane, lakini huwezi kuamini kilimo kimekua kwa chini ya asilimia tatu kila mwaka. Yale ambayo waliyazungumza kwa wananchi wakati wanaomba kura hawajatekeleza hata jambo moja.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe sababu za msingi; angalia Bajeti ya mwaka 2016/2017, tulitenga bilioni 101 wakatoa bilioni tatu peke yake kwenda kwenye kilimo, lakini mwaka 2017/2018 tulitenga bilioni 150 wakatoa bilioni 16 peke yake wakapeleka kwenye kilimo. Mwaka 2018/2019 tulitenga bilioni 95 mkatoa bilioni 42 peke yake.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia miaka yote ambayo tumekwenda kutenga bajeti hizi utaona kabisa kwamba utekelezaji wake miaka yote minne mmetekeleza kwa asilimia 17.55, miaka yote minne. Huu ni utani mkubwa sana kwa Watanzania. Nataka niseme, kama kweli wanataka kuondoa umaskini wa Watanzania ni lazima kuwekeza kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ukiangalia ukurasa wa 43 anasema Serikali imejikita kuhakikisha kwamba inainua kilimo na kuhakikisha kwamba umaskini unaondoka kwa Watanzania. Sasa kwa uwekezaji wa asilimia hizi ambazo zinawekezwa kwenye kilimo tusitegemee kabisa kwamba tunaweza tukawakomboa Watanzania na tukaondoa umaskini huu. Tunawatania Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachotaka kusema tu; kwa mwaka huu peke yake...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Frank, pokea taarifa; Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Atulie kwanza.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Frank; anapofanya uchambuzi wa bajeti na kuangalia bajeti ya kilimo, asijikite kwenye Wizara ya Kilimo peke yake. Bajeti ya kilimo ni bajeti mtambuka. Ukija kwenye *Vote* ya Waziri Mkuu tunao Mradi wa *MIVARF* na wenyewe unaji-*address* kwenye Sekta ya Kilimo, uongezaji thamani ya mazao, miundombinu ya masoko, lakini kutengeneza mfumo mzuri wa kilimo kwa wakulima mbalimbali. Kwa mfano mradi huo umefanyika kwa pande zote mbili; Bara na Visiwani. Ukienda TAMISEMI wanayo *vote* pia ambayo ina-*deal* na masuala ya kilimo kwa hiyo bajeti ya kilimo ni ya kisekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa namwomba anapofanya uchambuzi wa bajeti ya kilimo asi-*concentrate* tu na Wizara ya Kilimo, aende na kwenye sekta nyingine za kiwizara ambazo zina-*support* pia Sekta hiyo ya Kilimo na ndiyo atapata majibu sahihi ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimthibitishie kabisa kwamba Serikali ya Dkt. John Pombe Magufuli ni Serikali ya wanyonge, hayo ya kilimo ni machache tu lakini yapo mengine mengi ambayo yamekwisha kufanyika na mifano halisi imeelezwa kwenye hotuba ya Waziri Mkuu. Tumeshajenga zahanati, vituo vya afya, hospitali, kwa hiyo kwa vyote hivyo unaona kabisa ni Serikali ambayo inawajali wanyonge.

**SPIKA:** Nakufafanulia Mheshimiwa Mwakajoka, muda wako unatunzwa usiwe na wasiwasi; alichokuwa anasema

Mheshimiwa Waziri ni kwamba ukitaka kuichambua bajeti ya kilimo lazima uiangalie kwa mapana, sio *narrowly,* kwamba ukiwekeza katika Mradi wa *Stiegler's Gorge* ule wa Mwalimu Nyerere wa kuzalisha umeme, umeme ule utaenda kwenye viwanda ambavyo navyo ni katika mnyororo wa kuboresha *products* za kilimo. Ukijenga reli itasafirisha na mazao ya kilimo; ukichonga barabara ukaweka lami kuelekea kila mahali ndiyo unafungua kilimo huko; maana yake ni hiyo. Kitazame kilimo katika upana wake huo. Ndiyo ujumbe tu anakupa huo. Unapokea utaratibu huo?

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Mhagama angekuwa anatuambia kwanza hicho anachokizungumza ni asilimia ngapi. Sisi tunapitia randama za Kamati, tunaangalia utekelezaji na ndiyo maana tunachangia hapa, sasa Mheshimiwa akianza kutuambia kuna hela nyingine zimejificha, alipaswa kuziweka wazi. Vile vile akumbuke kabisa kwamba hizo fedha anazozizungumza ukienda kuangalia barabara vijijini ambako sasa tunafikiria wakulima wetu waweze kutoa mazao, barabara ni mbovu, hata mazao hayawezi kusafirishwa sasa hivi. Kwa hiyo anakokuzungumza huko fedha kwa kweli hazijaenda ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, tukumbuke Mkataba wa Maputo kwenye Nchi za Afrika, walishauri kwamba hizi nchi ili ziweze kuondoa umaskini katika nchi zao ni lazima wawekeze asilimia kumi ya bajeti zao kila mwaka ili kuhakikisha kwamba wananchi wao sasa wanalima vizuri, lakini pia wanapata masoko mazuri na baadaye wanaondokana na umasikini, lakini Serikali yetu haijawahi kufikia bajeti hiyo hata siku moja, mpaka tunavyozungumza leo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Mwakajoka; Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Hasunga mbona unaharibu sasa?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru mdogo wangu kwa mchango wake anaoendelea kuutoa, lakini nataka nimwelimishe kidogo, labda pengine anaweza akawa hajaelewa vizuri; tunapozungumzia asilimia kumi ya kilimo hatuna maana hizo fedha zote lazima ziwe kwenye bajeti ya kilimo.

Kwa hiyo kwa mradi mkubwa kama huu kwa mfano wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* maana yake tutasafirisha mazao. Kwa hiyo hela zote zilizoko kwenye uchukuzi zinakwenda kusaidia kilimo. Ukiangalia fedha zilizopo kwenye nishati zote zinasaidia kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hapo, nataka nimpe taarifa kwamba sisi kama Wizara hatulimi, kazi yetu ni kutengeneza miundombinu na kutengeneza sera za kilimo. Utekelezaji wa bajeti ya kilimo unafanywa kwa kiwango kikubwa na Sekta Binafsi. Kwa hiyo ukitaka kujua kwamba ni kiasi gani kimewekezwa kwenye kilimo maana yake tujue Sekta Binafsi imewekeza kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kumjulisha tu mdogo wangu kwamba uchambuzi wa bajeti kama ulivyokuwa umempa anatakiwa achambue kwa undani; ni zaidi ya asilimia 7.5 sasa hivi tumefikia na Tanzania ni nchi ya tatu katika Nchi za Afrika katika kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwenda kwenye Sekta ya Kilimo, ukiangalia katika upana wake kwa kuziangalia sekta zote ambazo zimetenga bajeti.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa hiyo.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, mimi nasema hivi; Serikali ilitenga bajeti ikaja Bungeni tukaipitisha Bungeni hapa. Hizi bajeti ninazozitaja mimi ni bajeti ambazo zimepitishwa ndani ya Bunge zikatekeleze shughuli za maendeleo kwenye Wizara ya Kilimo. Bajeti hizi hazijafanya kazi yoyote, ziko chini ya kiwango. Kuna moja imetekelezwa 2016/2017 kwa asilimia tatu; 2017/2018 kwa asilimia 11; 2018/2019 kwa asilimia 16 na 2019/2020 asilimia 15.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi?

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, tunazunguka nini badala ya kuzungumza uhalisia…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka kuna taarifa, ipokee.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana mzungumzaji, Mheshimiwa Mbunge Mwakajoka, lakini nataka nimpe taarifa. Anaonekana anapambana sana kwa kile anachodai kwamba Chama cha Mapinduzi kinakwenda kuondoka 2020.

Mheshimiwa Spika, nimwambie Chama cha Mapinduzi hakiwezi kuondoka kwa takwimu hizo, lakini Chama cha Mapinduzi wamehama mbele hapa, akina Mwakajoka wamekwenda kukaa nyuma kabisa kule, mbele wamewaacha akinamama hawa akinamama mnaowaachia chama hapa mbele peke yao hawawezi kukiondoa Chama cha Mapinduzi madarakani hawa akinamama. Akina Mwakajoka sogeeni mbele hapa maana yake chama kimeachiwa akina mama peke yao…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kuhusu Utaratibu.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** …mchanganyike, peke yenu chama hakiwezi kwenda.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, unamwachia anaropokaropoka huyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, Kaimu Kiongozi wa Upinzani amesimama, subiri kidogo; Mheshimiwa Halima nimekuona. *(Kicheko)*

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu; najua Kanuni zetu za Bunge zinakataza kutumia lugha za kuudhi, lugha za dharau, lugha za kibaguzi, lugha za kudhalilisha. Sasa nakuomba, kwa sababu tunakuheshimu kama Kiongozi wa Mhimili, kuna maeneo unaweza ukatania, halafu kuna maeneo mengine yanakera na yanachefua.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba umtake Mbunge wa Kinondoni aliyetangazwa kwa utaratibu anaoujua yeye, afute kauli yake.

**SPIKA:** Aliyefanyaje? *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa, tulieni basi…

Mheshimiwa Spika, naomba mtulie…

Mheshimiwa Spika, naomba umtake Mbunge wa Kinondoni afute kauli yake aliyoisema kwamba CHADEMA kwa kuwa hapa viti vya mbele kuna wanawake kwa hiyo hakina uwezo wa kushinda uchaguzi. Kwa hiyo anatuambia Mama Samia Suluhu, Makamu wa Rais wa Nchi hii, anatuambia Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mnadhimu wa Kambi ambaye yuko kiti cha mbele hana uwezo wa kukisaidia chama chake kushinda uchaguzi. Naomba umtake afute kauli yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Kaimu Kiongozi wa Upinzani.

Kama nimemsikia vizuri, tusubiriane kidogo, kama nimemsikia vizuri Mheshimiwa, amesema akina Mwakajoka mmerudi nyuma, mmeacha *front bench* yote akinamama watupu na kweli nikitazama naona akinamama watano wako mbele wao peke yao, akina Mwakajoka wamerudi nyuma, sasa ndiyo alikuwa anazungumzia hicho tu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kinondoni, weka sawa bwana ili tuweze kuendelea. *(Kicheko)*

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Eeh, weka sawa tu bwana tuendelee.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Naamini umenielewa vizuri kwelikweli kwa sababu mimi ninachojua chama cha watu wote na sio wakati wa mapambano wanaume wanarudi nyuma. Nilichotaka wanaume wasiwe wakati wa mapambano wanakimbia wanarudi nyuma, wanawaacha akinamama peke yao, sikusema kwa nia mbaya, nimesema kuwataka rafiki zangu akina Mheshimiwa Mwakajoka waje mbele washikane mkono kwa mkono, bega kwa bega pamoja washirikiane, isiwe wakati wa mapambano wanaanza kurudi nyuma taratibu mwisho watatoka kabisa. Ndiyo hicho tu nilichokisema, sikuwa na lengo la kubagua akinamama wala nini, nilikuwa nahimiza akinababa nao washirikiane na akinamama kuwa-*support,* sikusema kwa nia mbaya.

**SPIKA:** Ahsante. Amerekebisha jamani, amesema anataka bega kwa bega.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, endelea, dakika zako karibu zinaisha, weka sawa.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba unajua wanasema kwamba unapokuwa kiongozi ni vizuri sana ukawa na hekima. Sasa nina wasiwasi sana na Mbunge wa Kinondoni na inawezekana huyu Mbunge ndiyo maana alikimbia majukumu akatangazwa kwa njia anazojua yeye. Kwa sababu maneno haya sio ya mara moja, ni mara ya tatu sasa.

**SPIKA:** Sasa hapo na wewe unaharibu. Katoa wito tu kwamba uje mbele na wewe. Basi, hakusema zaidi ya hilo; endelea na hotuba yako ili umalize muda umeisha.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ngoja niendelee tu kusema kwamba, hiki ambacho nilikuwa nakizungumza humu ndani ya Bunge ni utekelezaji hafifu kabisa wa bajeti uliofanyika na Serikali ya Awamu ya Tano kwenye kilimo; hilo lieleweke hivyo.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Taarifa.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, lakini lingine, wakati huo kila mmoja...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, kuna taarifa; Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwakajoka ameendelea kusemea kwamba utekelezaji ni hafifu na anafanya *reference* ya Azimio la Maputo. Nataka nimwekee kumbukumbu sawa kwamba Wakuu wa Nchi walipokutana Maputo, asilimia kumi walizokuwa wanazisemea, aende akalisome lile Azimio, zinaongelea kilimo kwa maana ya *agriculture, forestryand fisheries.* Ukichukua hizo *components* za *agriculture in the broad sense* ya kilimo, misitu na mifugo, sisi hapa Tanzania tulishavuka hiyo asilimia kumi na hiki anachokifanya Mheshimiwa Rais na kama alivyosema Mheshimiwa Jenista, ukienda mpaka ngazi ya halmashauri tumeshavuka muda mrefu mno na tunaelekea kwingine kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa wasiwe na hii *temperate* ya uchaguzi, kwa haya mambo ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imeshafanya hata ile kusoma namba, sasa hivi hata *number plate* hamtaiona kwa sababu gari ya Dkt. Magufuli itakuwa mbali mno. Kwa maana hiyo hebu twendeni kwenye *facts* zilizopo kwenye *data* na tusiweke blah blah zingine hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe tu taarifa hiyo ili asiendelee kutumia vibaya muda wake.

**SPIKA:** Kabla sijairudisha *mic* kwa Mheshimiwa Mwakajoka ninayo mapendekezo kutoka kwa baadhi ya Wabunge. Wanasema kwa kuwa inaelekea uchaguzi ujao huenda hata Mbunge mmoja wa Upinzani asipatikane, patengwe viti maalum, tutengeneze utaratibu fulani maalum tuuandike kwenye Katiba pale ili tuweke hata viti kumi hivi kwamba hivi sasa tuwape bure, maana sasa kuna hatari kwamba itakuwa hakuna hata mmoja. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwakajoka, malizia bwana. *(Kicheko)*

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza sipokei taarifa ya Mheshimiwa Mwigulu kwa sababu naye ana *stress* sana, Kitila Mkumbo yuko anampumulia mgongoni. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa tu kingine ambacho nataka nimwambie ni kwamba Mheshimiwa amezungumza kuhusiana na ujumla wake kwenye bajeti ya kilimo, akiangalia kwenye mambo ya uvuvi ni miaka yote minne fedha hazijakwenda kabisa kwenye uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pia mliahidi meli tano ndani ya miaka mitano lakini mpaka leo meli ya uvuvi kwenye Bahari ya Hindi haijanunuliwa hata moja. Kwa hiyo yote anayozungumza tunajua nini tunachokizungumza ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo kwa kweli utekelezaji ni hafifu sana.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye afya; Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye ukurasa wa 26 ameonesha bilioni 256 zimetengwa badala ya bilioni 300 ambazo zilikuwa zinatengwa kipindi cha awamu ya nne lakini anasema utekelezai ni mzuri. Ukweli tu ni kwamba fedha iliyotengwa kwa mwaka huu ni bilioni 544, ndiyo iliyotengwa kwenye bajeti, lakini fedha iliyopelekwa sasa hivi ni bilioni 83 peke yake ambayo ni sawa na aslimia karibu 13. Sasa ukiangalia

unaona kabisa fedha zinatengwa lakini haziendi na Serikali hii inasema inakusanya. Juzi Waziri wa Fedha wamesema *TRA* kwamba wamekusanya 1.7 lakini hatuoni, utekelezaji wa bajeti umekuwa chini ya kiwango kabisa. Sasa nashangaa kama kweli wana uhakika wa kurudi mwaka 2020 kwenye uchaguzi unaokuja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. FRANK J. MWAKAJOKA:** ...mliowaona mwaka 2015 sio... niwaambie tu ni kwamba...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mwakajoka, nakushukuru sana kwa mchango wako; muda umeisha Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

Tunakushukuru sana. Nilikuwa nafikiria habari ya Tume huru ya Uchaguzi; kuna malalamiko hapa kuhusu uchaguzi ndani ya CHADEMA uliofanyika. Watu wanasema mbona hamkuweka tume huru ya uchaguzi ili iondoe malalamiko? Kama kweli mnaamini tume huru ya uchaguzi mbona hamkuweka?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Aah, tume huru ya uchaguzi kwenye CHADEMA maana yake mngealika CCM waje wasimamie uchaguzi wenu, ndiyo ungekuwa huru. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chegeni nilishakutaja; Mheshimiwa Dkt. Chegeni tafadhali, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia

katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mwakajoka amehamia mbele; tunakushukuru Mheshimiwa. *(Makofi/ Kicheko)*

Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Chegeni endelea.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na nafurahi kumuona rafiki yangu Mheshimiwa Mwakajoka amesogea mbele kwa wito wa Mheshimiwa Mtulia.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kweli mimi nampongeza sana yeye na timu yake na Mawaziri wa Nchi wawili ambao ni Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Angellah Kairuki na Naibu Mawaziri wawili; Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeangalia mambo mengi kwa upana mzuri sana, na kwa kweli ukiangalia jinsi ambavyo ameweza kuiainisha kwa kuangalia misingi ya bajeti yake, lakini mambo ambayo yamefanyika kama nchi, unaona kabisa kwamba hotuba hii imejikita katika kuelezea Watanzania nini azma ambayo Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, anayo kwa Watanznaia. Napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wakiwemo Makamu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na wale wote wanaomsaidia.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna janga la *Corona. Corona* hii imekuja kama magonjwa ya mlipuko, lakini magonjwa ya mlipuko yanakuwa na madhara yake kwa upande wa ugonjwa na upande wa uchumi. Napongeza sana jitihada ambazo Mheshimiwa Spika wewe binafsi pamoja na wasaidizi wako katika Bunge hili na Kamati ya Uongozi kwa kufikia katika maamuzi ambayo sasa Bunge tunaendelea na shughuli zetu kama mihimili mingine lakini

kwa kuangalia tahadhari zote na kuelimisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi namna sahihi ya kujiepusha na maambukizi ya Ugonjwa huu wa *Corona*.

Mheshimiwa Spika, huo ni upande mmoja, lakini pili najaribu kuangalia kwamba kama Serikali inafurahisha kuona kwamba mkakati wa Serikali daima, na hasa kufuata tamko la Mheshimiwa Rais kuwaambia Watanzania kwamba sasa tuko kwenye vita ya ugonjwa wa *Corona*, kila mmoja achukue tahadhari. Aliwasihi Watanzania, lakini pili akasema kwamba Watanzania lazima tukubali kwamba, tuko kwenye mapambano hatuwezi kufunga nchi yetu lazima tusonge mbele, uchumi wetu unahitaji kuwa-*supported* na Watanzania, lakini tuchukue tahadhari.

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo ambalo kwa kweli baadhi walibeza na hali inavyokwenda tunaimani kwamba, pamoja na kwamba ni suala la kisayansi lakini kama kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake ni sehemu kubwa sana ya kupata ushidni wa ugonjwa huu wa *Corona* kwa Tanzania kwa sababu mpaka leo kwa takwimu ambazo tumezipata bado tuko vizuri.

Naomba Mwenyezi Mungu naye atie mkono wake kwa Watanzania wote, tuheshimu maagizo ya Serikali, kila mmoja wetu tutii uamuzi na tuzingatie masharti ambayo yatatufanya sisi tujiepushe na ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, huo ni upande wa kwanza. Upande wa pili ni wa kiuchumi. Sasa hivi ni lazima tukubali duniani kote mambo ya uchumi yamepangaranyika, kila mahali mambo yamedorora na sisi hatuwezi kuwa *exceptional, we are part and parcel.*

Mheshimiwa Spika,mimi niombe kupitia Waziri wa Fedha na Ofisi ya Waziri Mkuu, tuone namna gani nzuri ya kutafuta *a rescue package* itakayowasaidia Watanzania tuendelee kupambana na janga hili lakini vilevile tukubali namna sahihi ya kuweza kuimarisha uchumi wetu. Tunahitaji kuishi pamoja na kwamba kuna tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii biashara nyingi zimedorora wala siyo siri lakini ni kwa sababu hali yenyewe duniani ime-*shut down.* Sisi tunaendelea kadiri tunavyoweza, tunaomba sasa kupata *support* ya Serikali ili sekta ambazo zitakuwa zimeathirika zaidi kuwe na *rescue package* ya kuweza kusaidia.

Mheshimiwa Spika, leo hii kuna watu ambao wana marejesho yao kila mwezi. Sasa hivi hali ilivyo mbaya watashindwa kurejesha. Nimeona jitihada za Serikali ambazo zinaendelea kufanyika lakini kuna haja ya kuona ni namna gani kuja na mkakati mzuri wa kuwawezesha Watanzania hawa waweze kupata nafasi nzuri ya kuweza kuondokana na tatizi hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ni tulivu, ni sikivu na yote haya inayafanyia kazi vizuri. Nakumbuka jana nilikutana na Mheshimiwa Mpango akasema Mheshimiwa Mbunge subiri, wala msipige kelele subiri. Akasema, nakuja na mkakati mzuri kwa namna gani kama Serikali tutajaribu kuhimili na kufufua uchumi wetu na kulinda mdororo huu wa uchumi kwa Watanzania wote. Napongeza sana mawazo ya Mheshimiwa Mpango na mawazo ya Serikali ambayo yatakuja hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala ambalo nilitaka nilizungumzie, tunapambana na *Corona* lakini kuna magonjwa mengine nyemelezi na magonjwa mengine ambayo yanaendana na tatizo hilo lazima tuyape kipaumbele, tusiyasahau. Kwa sababu Wizara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inasimamia mambo kama haya, ugonjwa wa *HIV* – UKIMWI, kuna *TB* na magonjwa mengine lazima yaendelee kupewa kipaumbele kwa sababu na yenyewe ni sehemu mojawapo ya tatizo hili la *Corona*.

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hapo nakuja kwenye suala la uwekezaji. Kwa vile Wizara ya uwekezaji iko chini ya Waziri Mkuu bado kuna tatizo na sintofahamu kubwa sana, namna gani ya kufanya *coordination* ya Wizara ya Uwekezaji

na Wizara nyingine ili iweze kuleta matokeo chanya kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, leo hii bado kuna kukinzana kati ya *TIC* - Kituo cha Uwekezaji na *TRA.* Mwekezaji anapokuja hapa nchini anapata *tax incentives* kupitia *TIC,* akienda *TRA* wanamwambia hapana kuna kodi lazima ulipe. Kwa hiyo, kuna haja ya ku-*harmonise* mambo kama haya na kupunguza *unnecessary delays* katika kufanya maamuzi kwa sababu haya yanatusababisha tunapoteza wawekezaji kwa sababu ya ukiritimba ambao hauna sababu wala tija. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu atusaidie ku-*harmonise TRA* na *TIC* ili ziweze ku-*facilitate* uwekezaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kila siku anazungumza lazima tuvutie uwekezaji wa ndani na nje ya nchi. Hata hivyo, leo hii ukitaka kutengeneza *working permit* ya mfanyakazi tozo la *labor* ni dola 1,100 ukipitia *TIC;* ukienda *Immigration* ni dola 2,050, kwa hiyo, utatumia dola 3,150 kupata *permit* ya mfanyakazi hapa nchini, *it is too expensive.* Mimi nashauri Serikali ijaribu ku-*review* hizi *fees* kusudi tuweze kupata wawekezaji wengi na wafanyakazi wengine ambao wana sifa za kufanya kazi hapa nchini ili iweze kuchangia katika uchumi wetu. Uchumi lazima uendeshwe na watu wote, tuchanganye *expertise* ya ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kingine ninachokiona ni kuhusu maamuzi, tatizo la maauzi bado ni ugonjwa. Mchuchuma na Liganga leo tuna miaka nenda rudi lakini hadithi na ngonjera zilezile, maamuzi hayafanyiki. Naomba kama Serikali tujitahidi sana kufanya maamuzi tusije tuka-*frustrate* uwekezaji ambao tunauhitaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kingine kuna *issue* ya *BRELA.* Leo hii ukienda *BRELA* ukitaka kusajili kampuni wanakambia lazima uwe na *NIDA,* ukienda *NIDA* hawatoi vitambulisho. Sasa unashindwa ku-*register* makampuni na kufungua biashara nyingine nyingi kwa sababu ya *NIDA.* Nashukuru kwamba Serikali imeweza kuweka utaratibu mzuri sasa

kwamba angalau *NIDA* wataweza kutoa vitambulisho kwa uharaka zaidi. Hii ni hatua moja muhimu ya Serikali kupongezwa; imetambua hilo na ni vema ilisimamie lifanyike kwa uharaka zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia vitambulisho vyetu ni vingi mno, tujaribu ku-*synchronize* vitambulisho. Leo una kitambulisho cha *NIDA, Driving License,* una sijui cha wapi ni vingi mno. Tujaribu kuwa na kitambulisho ambacho mtu akiwa nacho kimoja kina-*cover* kumpa *information* mtu yeyote na mahali popote pale, itasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine nachokiona ni suala la *returns* za *BRELA.* Sasa hivi ukienda *BRELA* kama una kampuni ina miaka mingi haijafanya *return* siku za nyuma unaambiwa ulipe *returns* za miaka 10 iliyopita...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili Mheshimiwa malizia.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Spika, namalizia. La kumalizia ni suala la wakulima wa pamba. Mimi kwangu katika Wilaya ya Busega wakulima wa pamba mpaka leo hii wanadai shilingi milioni 450 hawajalipwa. Hawa watu wameuza pamba toka mwezi Mei na Juni, 2019 mpaka leo hawajalipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu amefanya kazi kubwa sana ya kuwaunganisha wanunuzi wa pamba na hawa wakulima na kadhalika lakini bado Mheshimiwa Waziri Mkuu nikuombe chondechonde hawa wakulima wa pamba walipwe ni muhimu sana. Hawa wakulima toka mwezi Juni, 2019 pesa hajalipwa, hata tukisema wazalishe tena mwaka huu afanye vizuri, haiwezekani tunamnyonya mkulima. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu hili alisimamie. Najua anafanya kazi kubwa sana, aendelee kufanya kazi hiyo vizuri sana.

Mheshimiwa Spika,baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Dalali Kafumu ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami niungane na wasemaji walionitangulia kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana hapa na kuweza kujadili masuala yanayohusu Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri iliyojaa weledi mkubwa sana. Kwa namna alivyoiwasilisha jana hapa, mimi nasema hotuba ile ilistahili kuandikwa kwa wino wa dhahabu.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze sana na wewe mwenyewe. Kama ingekuwa ndiyo ile miaka ya nyuma ile, sisi wengine ni *form one* humu, saa kama hizi hapa umezungukwa na milima ya ma-*volume,* tukianza kuperuzi, kutafuta *votes* na vitu kama hivyo, lakini mwaka huu mambo mazuri kabisa hapa, tuko ki-digitali zaidi. Hili ni matunda yako wewe na tunakushukuru sana kwa kweli, umetuwezesha sasa tunaweza tukatekeleza majukumu yetu humu kisasa zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi pia nitie neno kwenye hili janga la *Corona*. Hili janga ni kubwa na katika muda ambao Watanzania tunatakiwa tuwe na mshikamano wa hali ya juu basi ni katika kipindi kama hiki cha sasa. Hili jambo si dogo, rai yangu ni katika maeneo makubwa mawili. Eneo la kwanza tuendelee kufuata maelekezo ya wenye mamlaka, viongozi wetu namna gani tutakavyoweza kufuata miiko na makatazo mbalimbali, kupeana mikono, kukumbatiana, kuepuka mikusanyiko isiyokuwa na lazima na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hapo naomba sana Serikali sasa ianze kuyafanyia kazi yale ambayo yanasemwasemwa kwamba ni *lapse* ndogondogo kwenye

*system* zetu. Kwa mfano, sasa hivi kuna habari zinasemwa kidogo kwenye mipaka yetu, hususan kwenye kiwanja cha ndege bado panaonekana kama kuna ulegevu kidogo. Kuna watu wanapenya, watu wanasema kwamba kuna watu wengine wanapelekwa hoteli kwenye *quarantine* kuna wengine wanapita. Mambo kama haya katika kipindi kama hiki ni vizuri sana wenye mamlaka sasa wakatupia macho kwa sababu kila aina ya habari si ya kuidharau katika nyakati kama hizi, tuko katika nyakati ngumu sana.

Mheshimiwa Spika, mimi niingie kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwenye hotuba hii ukurasa wa 10 tu mwanzoni pale imeelezea mafanikio mbalimbali ya Serikali ya Awamu ya Tano. Yamezungumzwa mengi, mimi nitazungumza moja tu hapa, suala la *Standard Gauge Rail.*Nalizungumzia hili kwa sababu Kamati yetu ilipata fursa ya kutembelea pale na tukaangalia toka pale mwanzo, Dar-es-Salaam kwenye *station* kubwa mpaka huku Soga. Tulipita na gari sambamba na zinapojengwa zile *track,* tumeona uwekezaji ule ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli katika namna ya kipekee sana tumpelekee pongezi Mheshimiwa Rais, hili wazo kwa kweli ni kubwa na mradi ule ni mkubwa na hali inayokwenda pale kwa kweli *isvery promising.* Niseme tu kwamba yale masuala mengine ambayo tuliyaona kwenye Kamati na tukatoa ushauri pale na namuona Mheshimiwa Naibu Waziri basi muyafanyie kazi kwa sababu, *by July* tumeambiwa kwamba kipande cha Dar-es-Salaam – Morogoro kitaanza kazi, lakini bado masuala ya kununua vile vichwa vya treni na mabehewa bado halijakaa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine nitachanganya kwa sababu naona kengele imeshaanza kuni-*alert, u*kurasa wa 14, 50 na 57, nitayazungumza kwa pamoja. Limezungumzwa suala la utalii na miundombinu ya usafirishaji. Suala la utalii, mimi natokea katika Kisiwa cha Mafia, ni kisiwa cha utalii. Suala la utalii linakwenda sambamba na miundombinu yake, pale tuna miundombinu mbalimbali ikiwemo ya gati pamoja

na Kivuko kile cha Nyamisati. Naishukuru sana Serikali gati lile limekamilika na kivuko kile kinajengwa. Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ametoka lakini Mheshimiwa Naibu Waziri namwona, tuna tatizo pale kwenye kile Kivuko kinachoundwa cha Nyamisati kazi ilikuwa inakwenda kwa kasi sana lakini ghafla kasi imepungua.

Mheshimiwa Spika,mimi pale Mheshimiwa Waziri aliniambia kwamba ninakupa jukumu kila mwezi uje hapa kufuatilia na mimi ninakwenda pale kila baada ya wiki mbili. Mara ya mwisho mkandarasi analalamika pale fedha zake hajalipwa lakini nimekwenda kufuatilia kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tayari fedha zile ameshazitoa ziko Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa hiyo, naomba mharakishe tu kumlipa yule mkandarasi ili amalizie kile kivuko tuwe ndani ya muda na tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Spika, kwa harakaharaka kule Mafia tuna barabara inayotoka pale Kiwanja cha Ndege pale Kilindoni kwenda mpaka Rasi Mkumbiambayo ni kama kilometa 55. Barabara ile imo ndani ya ahadi ya CCM na ni ahadi pia za Rais Mstaafu. Hata hivyo, hivi sasa tuna changamoto pale, tunaona nia ya Serikali na Wizara kuhakikisha kwamba barabara ile inawekwa lami na sasa hivi pale yupo yule *consultancy* anamalizia suala la usanifu na kuangalia namna watakavyowalipa watu fidia, imeleta sintofahamu kubwa sana kule Mafia, sasa hivi wananchi wengi wameondolewa kwenye hili sakata la kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Spika, siyo kwa kiburi wala jeuri tunachosema kwamba sisi Mafia tuko tayari barabara hii ichelewe kwanza lakini masuala ya malipo ya wananchi hawa yazingatiwe. Kwa sababu mimi nina uzoefu barabara ambayo nimeirithi kutoka kwa mwenzangu ambayo ilijengwa kwa lami mpaka leo ofisini kwangu kuna mafaili na mafaili ya madai mbalimbali ya wananchi ambao fidia zao walikuwa hawajapata.

Mheshimiwa Spika, sisi tunaishukuru Serikali kwa nia njema kabisa na naiona nia ya Mheshimiwa Waziri mwaka ujao wa fedha kuanza kuweka lami barabara ile lakini suala hili la fidia la wananchi wangu inaniuma sana kuona kwamba hata kama tutapata barabara ya lami lakini mwananchi wangu akakosa kulipwa fidia yake kwangu mimi haitanipa *comfort* sana. Nipo tayari kusubiri lakini tuhakikishe kwamba suala hili linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jitu Soni nilishakutaja, utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kunipa afya na kupata uwezo wa kuchangia. Pia nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na timu yake nzima kwa kazi nzuri na ambayo inaonekana. Ndoto za Watanzania sasa zinaendelea kukaribia kutimia na kila sekta imefanya juhudi kubwa. Lengo letu sisi kama Wabunge ni kuendelea kuishauri Serikali na pia kutoa maoni ili yaweze kufanyiwa kazi na tuendelee kuboresha maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa pamoja na Mawaziri wenzake wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya kwa kuratibu shughuli zote za uendeshaji mzima wa Serikali, lakini pia shughuli za sera na masuala ya Bungeni.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa kutimiza ile ndoto ya kuwa na Bunge mtandao ambayo sasa wote tumeona mafanikio yake. Ingekuwa hiki kipindi ambapo ugonjwa wa *Corona* umekuja na hatuko katika masuala ya Bunge mtandao naamini Bunge hili lingekuwa limeahirishwa. Hongera sana na pongezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi langu moja, tunaomba sasa na Serikali ijitahidi kuweka katika mtandao huu sheria zote ambazo tayari tumezipitishaili tukihitaji kupitia sheria mbalimbali basi tukiingia kwenye *tablet* zetu tuweze ku-*downlod* zile sheria tuweze kufanya *reference* mbalimbali kama kuna kuleta mabadiliko au kuangalia *reference* mahali ambapo tunahitaji kufanya hivyo. Hiyo itatusaidia sana na itarahisisha mambo mengi ya uendeshaji wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia niipongeze timu nzima ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa suala zima hili la *Corona* na namna wanavyolisimamia. Kuna mengi ambayo yanafanyika, wengi wanaendelea kulaumu lakini mimi najua. Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Kilimo Taifa na tayari sekta ya kilimo inaandaa athari mbalimbali ambazo zinatokana na jambo zima hili kiuchumi kwenye sekta ya kilimo, lakini hivyohivyo kila sekta, ya viwanda na wengine wote wamepewa hayo maagizo. Sekta zote zikishaleta hizo taarifa zao naamini Serikali sasa ndiyo itapata tathmini kamili kutoka kwa wadau wenyewe ndiyo waweze kupanga nini kifanyike ili tuweze kuona hii athari ya kiuchumi na namna ya kusonga mbele, kwa hiyo, hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu lingine moja kutokana na suala hili la *Corona*, kama inawezekana Serikali iangalie namna ya kupata vifaa tiba vile ambavyo vinahitajika basi Serikali ingeweza kuondoa kodi ili vifaa hivyo viweze kuingizwa nchini kwa gharama nafuu bila kodi yoyote. Tunajua kabisa Serikali peke yake haitaweza lakini sekta binafsi na wadau mbalimbali wako tayari kusaidia. Kwa hiyo, bidhaa hizi zikiwa zimeondolewa kodi zitakuja kutusaidia hata baada ya janga hili kupita tuna uhakika vifaa hivyo vitaendelea kutumika kwenye shughuli mbalimbali katika sekta nzima ya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze Serikali kwa ujenzi wa vituo vya afya na zahanati mbalimbali pamoja na hospitali. Nishukuru kwamba sasa hivi tumeona matangazo na madaktari wengi wameomba nafasi zile 1,000; 700 zitakuwa katika ngazi hii ya TAMISEMI lakini 300 zitakuwa ngazi

ya Taifa. Tunawapongeza sana, tunaomba hizo ajira mzi-*fast track,* tunajua wameshaomba ili waende kwa sababu zahanati na vituo vya afya viko tayari ili tuweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pia nilikuwa naomba kwa upande wa *TARURA* hali ni mbaya, barabara nyingi zimeharibika nchi nzima na siyo jambo la kawaida bali ni kutokana na mvua kubwa zilizojitokeza. Tunaomba mruhusu kwa mwaka huu kwenye fedha zote zitakazoenda *TARURA* itumike *force account* ili tuweze kukodisha mitambo kwa gharama nafuu ili angalau tuweze kurekebisha barabara zetu ziweze kupitika wakati wote lakini pia kutengeneza makalvati na madaraja ambayo hayahitaji utaalamu wa hali ya juu ili mawasiliano yaweze kurudi. Pia tuangalie namna ya kuongeza bajeti kwa upande wa *TARURA.*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba amezungumzia suala la kilimo na hilo nitalizungumza wakati wa bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mapana yake lakini niongelee suala la lishe. Siku zote naamini kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Tungewekeza zaidi kwenye upande wa sekta hii ya kilimo kwa mapana yake na watu wakaendelea kupata elimu juu ya lishe hata hili gonjwa la *Corona* tusingekuwa tunaliogopa sana kwa sababu miili yetu ingekuwa na kinga na hata yale magonjwa mengine, miili ikiwa na kinga nzuri hii gharama tutayotumia kwenye dawa za kutibu itapungua. Kwa hiyo, tuwekeze zaidi huko kwenye sekta ya kilimo kwa mapana yake ili tuweze kujenga afya zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kwenye Sekta ya Ajira na Vijana, naomba kwenye Sekta ya Kukuza Ujuzi tungeendelea kuwekeza. Ile asilimia mbili tuliyopitisha kwenye sheria wakati wa dharura ambayo inakwenda Bodi ya Mikopo, nashauri irudi kwenye *VETA (Skills Development)* ili vijana wote sasa waweze kuboreshwa kwenye ujuzi kwa kupitia *VETA.*

Mheshimiwa Spika, kwenye *VETA* nashauri twende na mfumo wa *Builder Apprenticeship Painting System (BAPS)* ambapo Mkoa wa Manyarara pale Babati ndiyo ya kwanza

Tanzania tumeanza kufanya majaribio. Ni mfumo ambao mwanafunzi anasoma miezi miwili au mitatu, anaenda kutekeleza yale ambayo amefundishwa katika viwanda au katika karakana mbalimbali. Akitoka pale baada ya miaka miwili ni fundi kamili ambaye ni *hands on.*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wengi sasa hivi wanahitaji *blue collar jobs,* siyo *white collar jobs* ambapo ana *degree* yake haimsaidii, hapati ajira. Ingewezekana tungebadilisha sheria kama nchi nyingine, badala ya kwenda *JKT* ukimaliza *Form Four,* kila mtu apitie kwenye mfumo huu wa *VETA* wa kupata *skills* za aina fulani ili katika maisha kama huna ajira, angalau unajua kitu kingine cha kufanya ambacho kitakupa ajira kwa wakati huo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nashauri, nashukuru kwamba Ofisi ya Uwekezaji sasa iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, wanaendelea kuratibu vizuri sana. Tunaomba suala zima kwa kupitia ile *road map* tumepata hii *blue print,* tunaomba sasa sheria ile ya *blue print* ije kwa haraka zaidi ili itekelezwe kusudi gharama za uzalishaji hapa nchini ziteremke, bidhaa zetu ziweze kushindana kwenye soko la ndani na la nje kwa gharama. Hiyo inawezekana kwa kupitia hiyo sheria ya *blue print* kutekeleza yale yote ambayo yako kwenye *blue print.*

Mheshimiwa Spika, pia ombi lingine ambalo ni muhimu sana lifanyiwe kazi kwa kupitia uwekezaji, ni suala hili la BRELA, kampuni nyingi zinadaiwa *penalty* na *interest* kutokana na kutokuwasilisha *returns* kwa miaka mingi. Naomba kama mlivyofanya kwenye Kodi ya Mapato, mngewapa msamaha ili tuanze moja. Kwa sababu zile *penalty* kwa tozo za shilingi 14,000/=, yaani hakuwasilisha kipindi kile, leo ni shilingi milioni 10. Sasa mtu anaona kuanzisha kampuni ni shilingi 300,000/= kwa nini nifufue ile kampuni inadaiwa shilingi milioni 10? Ni vizuri tukafuta yale madeni tuanze *fresh...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Malizia.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dalaly Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nichangie kidogo hoja ya Waziri Mkuu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, *speech* yake kwa kweli imeeleza juhudi ambazo Serikali imezifanya, ni juhudi nzuri. Kwa kweli mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Serikali imefanya kazi kubwa. Nikiangalia kwenye Jimbo langu, Serikali imetuletea maji kutoka Ziwa Victoria. Kata zaidi ya 11 sasa zina maji. Tumepata fedha shilingi bilioni mbili na zaidi tunajengewa *VETA* pale.

Mheshimiwa Spika, tumejengewa Kituo cha Afya cha Igurubi, tuna daraja la Ngutu ambalo tulijengewa. Kwa kweli ni mambo mengi mazuri wananchi wa Igunga wanashukuru. Kwa niaba yao, naomba niseme ahsante sana kwa Serikali kutufanyia haya mambo mazuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala la umeme nisilisahau, bado nina kata tano tu ambazo hazijapata umeme. Naomba basi itakapofika wakati ziweze kupewa umeme. Kwa maana hii, naomba niishukuru sana Serikali, nimshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali yote kwa kazi nzuri hii. Bado tuna changamoto kidogo kidogo ambazo kwa kweli ndiyo wajibu wetu Wabunge kusema. Kama Wabunge wengi walivyosema, nami naomba niseme, hizi changamoto basi tuzifanyie utaratibu.

Mheshimiwa Spika, nianzie na janga hili ambalo liko pamoja nasi, Waheshimiwa Wabunge wamesema, nami naomba kuishauri Serikali kwamba kwa sababu limetukuta tuko kwenye bajeti, ni lazima tunapoendelea kuchakata bajeti yetu tuendelee kuiangalia. Hatujafika mwisho, ikiwezekana tuweke utararibu wa kibajeti kupambana nalo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelekezo yote haya ambayo wananchi tunaendelea kuyafuata lakini tusisahau kama Serikali kwamba janga hili ni kubwa na hata ikibidi kubadilisha bajeti yetu kidogo, tusione aibu kwa sababu ni jambo kubwa limetukuta.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu kilimo. Sisi ni wakulima wa pamba kule Igunga, tunazalisha mbegu kwa ajili ya wakulima wa pamba wote Tanzania. Mwaka 2019 tumepata taabu sana ya kuuza zao la pamba na mpaka sasa kuna baadhi ya wananchi bado wanadai hawajalipwa. Zaidi ya shilingi milioni 200 hazijapelekwa kwa wananchi. Tunaomba basi kama inawezekana Serikali imalizie, nadhani siyo Igunga tu, lakini wakulima wa pamba wote hii taabu iliwapata sana. Tukumbukeni Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi wetu wanakata tama kidogo. Mwaka huu nadhani nilizungumza na Naibu Waziri, kuna marekebisho kidogo kwenye jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kusema ni madhara ya mvua ambazo zimenyesha. Tunashukuru tumepata mvua na chakula ni kingi kama ulivyosema. Tuna chakula kule kwetu kingi sana, mahindi na kadhalika. Sehemu chache ambazo zilikuwa za chini kule, maji yamechukua mpunga na nini, lakini sehemu nyingi wamepata chakula, ila imeleta madhara makubwa sana. Kweye Jimbo langu kuna barabara ambayo huwa nalalamika kila siku, tulipata fedha, lakini wameshindwa kujenga kwa sababu mvua imenyesha kubwa. Nilikuwa naomba basi tuangalie utaratibu wa kubadilisha, kuongeza bajeti kwenye hizo barabara kwa sababu zimekatika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la umeme kama nilivyosema, wananchi wa Igunga wanashukuru sana. Bado Kata tano tu; Kata ya Mtungulu, Kinungu, Kininginila, Mwamashiga na Kata ya Isakamaliwa, bado hazijapata umeme hata kidogo. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, tunaomba basi mtutazame kwa namna ya pekee.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kutoka mwisho ni usala la uwekezaji katika nchi yetu. Tunataka kwenda kwenye nchi ya viwanda na Mheshimiwa Chegeni amesema kidogo kwamba tunahitaji sana tuhahamasishe uwekezaji wa ndani na wa nje. *Blueprint* ile hebu tuitekeleze kama alivyosema Mheshimiwa Soni, ni muhimu sana. Kwa sababu tusipofanya hivyo, tunaweza tusiifikie nchi ya viwanda kwa sababu wawekezaji wengi wanakata tamaa. Wengine wanaondoka, wengine wanaogopa kwa sababu ya matatizo ambayo yako katika kuendesha biashara na kuanzisha biashara katika nchi yetu imekuwa taabu sana.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nizungumze kuhusu Sekta ya Madini ambapo kwa kweli naipongeza sana Serikali. Wamejitahidi wamefanikiwa jambo moja kubwa ambalo sisi lilitushinda la kuwapatia machimbaji wadogo masoko. Serikali imefanikiwa sana na ninawashukuru sana. Jambo moja dogo limebaki ni kuhamasiha Sekta ya Uchimbaji Mkubwa. Sekta ya Uchimbaji Mkubwa imekufa kwa sababu utafutaji umepotea kabisa. Utafutaji ndiyo *engine* ya kuleta migodi mingine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali na Waziri wa Nishati na Madini, tutazungumza kwenye Wizara yake, ahamasishe utafutaji mkubwa wa madini kwa watafutaji wa ndani na wa nje ili migodi iweze kuanzishwa siku za usoni. Hii migodi mitatu iliyobaki, ikifungwa hatutakuwa na migodi tena na migodi inaleta ajira kweli. Inaleta zile *effects* za watu ku-*supply* migodini, kufanya kazi kule ni muhimu sana. Kuna nchi zinaendeshwa na uchumi wa migodi. Kwa hiyo, nasi tukihamasisha utafutaji, tutakuwa na hali nzuri sana ya kuweza kupata uchumi kutoka katika madini yetu haya. Tumeweza kuya-*control,* tumeweza kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo hawayatoroshi ovyo ovyo. Kwa hiyo, lazima tuyachimbe kwa ku-*benefit* uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naishukuru tena Serikali, endeleeni kufanya hivyo, nasi wananchi tunapokea na tutafanya kazi pamoja nanyi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Kafumu kwa kutumia muda vizuri. Sasa mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mbunge wa Liwale.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami jioni hii niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha mimi na ninyi kuwepo hapa tukiwa na afya njema. Vile vile nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyoweza kuiongoza nchi hii kwa miaka minne mfululizo na hii ni bajeti ya nne ambayo haina ukakasi, tunakwenda kifua mbele.

Mheshimiwa Spika, yaliyofanywa nchi hii ni makubwa sana. Vile vile nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu wa timu yake yote. Mheshimiwa Waziri Mkuu, pongezi za pekee kwanza kwa kumudu *speed* ya Mheshimiwa Rais. Kwa sababu najua mlianza wengi, lakini wengine wameteremka, watu ambao *speed* iliwashinda, lakini wewe mwenyewe umebaki katika kiti hicho muda mrefu. Kwa hiyo, nakupa pongezi binafsi kwa kumudu kwenda na *speed* ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba hii naomba nijikite sana kwenye upande wa kilimo. Ni ukweli usiopingika, kwenye nchi yetu asilimia 65 ya Watanzania ni wakulima na hapa napenda kuipongeza Serikali, imechukua juhudi mbalimbali za kuimarisha kilimo hasa katika kuwekeza katika tafiti na kuwekeza katika upande wa pembejeo.

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa ambalo naomba niendelee kuisisitiza Serikali, kuliangalia kwenye Sekta ya Kilimo hasa kwenye upande wa masoko, tunayo shida kubwa sana ya masoko ya mazao yetu. Nafikiri hapa hata Mheshimiwa Chegeni ametoka kusema hapa, kila mtu anayetoka huko Mwanza anazungumzia pamba na shida kubwa

anayozungumzia ni upatikanaji wa fedha kwa wakulima wetu. Upatikanaji huu wa fedha unakwenda sambamba na upatikanaji wa masoko ya mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunawekeza kwa kiasi kikubwa sana kwenye pembejeo na kwenye tafiti, lakini tusipokuwa na uhakika wa upatikanaji wa masoko ya mazao yetu, shida kwa wakulima wetu bado itakuwa kubwa sana. Ninapozungumzia soko, naomba nijielekeze vile vile kwenye ushirika. Kwenye ushirika kuna matatizo makubwa na mazito sana. Kuanzia kwenye sheria yenyewe ya ushirika. Hii ni mara ya pili nasema kwamba naiomba Serikali walete Sheria ya Vyama vya Ushirika ifanyiwe mapitio. Pamoja na kwamba hili ni Bunge la mwisho, basi hata kwenye Bunge lijalo hili jambo lifanyiwe mkakati. Sheria ya Vyama vya Ushirika bado ina upungufu mkubwa sana. Hata wenyewe Vyama vya Ushirika ukikaa nao wanakubali kwamba kweli kuna tatizo kwenye Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Spika, siku moja nilikaa na Afisa Ushirika wa Wilaya, namwuliza vipi bwana, haya mambo yanakwendaje kwenye Vyama vya Ushirika? Mbona vinapoteza fedha za wakulima, wanapoteza mazao, inakuwaje? Anakwambia kwamba hata yeye hana *mandate* kubwa ya kuingia kwenye Vyama vya Ushirika na kukagua. Mwenye *mandate* hiyo ya kukagua ni *COASCO.* Sasa ni lini *COASCO* inavifikia vyama vya msingi? Ni lini *COASCO* inafikia vyama vikuu vya ushirika? Kwa hiyo, utakuwa *COASCO* yenyewe tayari ni mzigo.

Mheshimiwa Spika, hivi leo mimi ninavyozungumza hapa, katika Mkoa wa Lindi hasa Wilaya ya Liwale tuna tani 800 za korosho zimekosa soko, wakulima wanapeleka zile korosho mwezi wa Kumi na Moja, mpaka leo hawajui hatima yao. Kwa hiyo, naomba Serikali ichukulie jambo hili kwa umakini sana, kwamba Vyama vya Ushirika badala ya kuwa msaada kwa wakulima vimekuwa ni mzigo kwa wakulima. Kwa hiyo, naomba Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Ushirika yafanyike.

Mheshimiwa Spika, halafu kwenye hiyo hiyo sheria, Vyama vya Ushirika vimeruhusiwa kuanzishwa na watu 20, sijui watu15; matokeo yake unakwenda kwenye Halmashauri unakuta Vyama vya Ushirika lukuki na vyama vyenyewe vinafanya kazi wakati wa mazao tu. Ina maana wao wakati wa kununua mazao, wananunua mazao, yakiisha wanafunga milango na chama kinaishia pale. Wanasubiri msimu mwingine uje, wanafungua milango, wanachukua korosho za watu, wanauza, wanawaibia, msimu ukiisha wanafunga.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi vyama vya namna hii, sheria iansemaje? Hivi ni wakati gani chama kinatakiwa kifutwe? Yaani chama kisipofikia malengo yake, miaka mitatu, minne chama kinatangaza hasara, wakulima wanadaiwa, mpaka TAKUKURU wanaingia kwenda kudai fedha za wakulima, hicho chama kweli bado kina sababu ya kuishi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nijike hapo kwenye Vyama vya Ushirika. Kwa kweli Vyama vya Ushirika sheria iletwe, viangaliwe ili kama kweli lengo la Vyama vya Ushirika ni kuwasaidia wakulima, zamani ilisemwa Vyama vya Ushirika vilikuwa vinaweza kusomesha mpaka vijana wa shule wanachama wa Vyama vya Ushirika, lakini leo Chama cha Ushirika kimekuwa ni mzigo kwa mkulima, ndiyo kinachomfanya ashindwe kusomesha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ilichukue hili, Vyama vya Ushirika ni mzigo. Pamoja na nia njema ya kuundwa kwake, lakini Vyama vya Ushirika kwenye sheria, inasema Vyama vya Ushirika vitasaidia wakulima kupata pembejeo na kupata masoko, lakini hivi vyama kweli vinafanya hiyo kazi?

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aje na tathmini. Lazima tufanye tathmini tuhakikishe vyama vingapi vinakidhi vigezo na vile ambavyo havikidhi vigezo vifutwe kwa sababu utitiri wa vyama hauna maana kwa wakulima kama wakulima watapoteza mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili naomba nizungumzie suala la ardhi. Ardhi haiongezeki, wanadamu tunaongezeka. Ukienda kule kijijni kuna sheria kwamba kijiji kinaruhusiwa kuuza heka 50, lakini hao mliowapa hiyo *mandate* ya kuuza heka 50, elimu hiyo wanayo? Ardhi inauzwa sana nchi hii sasa hivi. Uuzwaji wa ardhi umekuwa ni wa holela sana. Ukienda huko vijijini, ardhi inaondoka kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali, pamoja na kwamba tumeruhusu vijiji kuuza heka 50, lakini bado wataalam tulionao ni wachache hawakwenda kuwapa elimu wale wanaouza ardhi. Kule vijijini watu hawawezi kuona thamani ya ardhi, wanauza tu; lakini sisi tunaoishi mijini tunajua thamani ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kabla Taifa hili halijaingia kwenye janga la kupoteza ardhi, Serikali mtupie macho kwenye uuzwaji wa ardhi. *(Makofi))*

Mheshimiwa Spika, liko suala lingine huko kwenye ardhi. Kuna hili suala la urasimishaji. Ndugu zangu, urasimishaji ulikwenda Manzese, ulikwenda Kinondoni kwa sababu tulishindwa kuwapanga wale watu, tayari walishajazana. Leo urasimishaji uko mpaka vijijini. Watu wanakaa holela halafu mtu anakuja anakwambia kuna urasimishaji. Mji unakaa hovyo; hakuna mtaa, hakuna barabara; yaani kuna vijiji ambavyo havina hata sababu ya kuingia kwenye urasimishaji. Ni suala tu la mtendaji kuwahamasisha wananchi wajipange, wapimiwe maeneo yale wakae, kama ni kugawiwa; tena upimaji wenyewe siku hizi ni wa kuchangia.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba tuachane na mambo ya urasimishaji hasa kwenye Halmashauri hizi za Wilaya na Vijijini. Tubaki na huu urasimishaji wa Dar es Salaam na Dodoma pengine kama tulichelewa kujipanga.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante, malizia.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Napongeza sana Serikali kwa kazi kubwa tunayoifanya, inayotukuka na inayoonekana.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana, nakushukuru sana Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale. Utupelekee salamu huko Mtawatawa, Mpigamiti, Mkundi na maeneo mengine ya Liwale.

Waheshimiwa Wabunge, uchangiaji wetu umekuwa mzuri. Jioni ya leo walitarajiwa wachangie jumla ya Wabunge 23 na wote wamepata nafasi ya kuzungumza kwa uhuru kabisa. Tunaendelea na Wizara hii siku ya kesho. Tuendelee kujiandaa wale ambao tutakuwa na fursa ya kufanya hivyo na tutapata nafasi ya kuchangia kama ilivyo kawaida yetu, kwa uhuru kabisa.

Basi kwa vile shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zote zimekamilika, sasa nichukue nafasi hii kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa nane kamili mchana.

*(Saa 12.00 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 3 Aprili, 2020 Saa 8.00 Mchana)*